**15 APRILI, 2025**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Sita – Tarehe 15 Aprili, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tuketi.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):**

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 69

**Ujenzi wa Majengo Kituo cha Afya Kazuramimba – Uvinza**

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha za kujenga majengo katika Kituo cha Afya Kazuramimba - Uvinza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha afya Kazuramimba katika Halmashauri ya Uvinza kinahudumia wananchi wapatao 40,711.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imetenga shilingi milioni 625 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wazazi, jengo la upasuaji, jengo la maabara, jengo la kuhifadhi maiti na kichomea taka katika Kituo cha Afya Kazuramimba katika Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninaomba kuuliza maswali mawili. Swali la kwanza; Serikali iliahidi hapa Bungeni kupeleka shilingi milioni 50 kwenye Kituo cha Afya pale Nguruka ambacho kimechakaa. Mheshimiwa Waziri Mkuu alishafika pale kuhakikisha. Je, ni lini fedha hizi zitapelekwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; nina vituo vinne vya Kalya, Buhingu, Ilagala pamoja na Uvinza, vyote miundombinu haijakamilika kwa maana ya wodi pamoja na majengo mengine. Ni lini fedha zitapelekwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Nguruka katika Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza ni moja ya vituo vya afya ambavyo vinahitaji kuongezewa majengo na ninafahamu kwamba lilikuwa ni agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu na sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kama ilivyo ada maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa ni kipaumbele namba moja. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Bidyanguze kwamba tayari tumeshaliweka kwenye mpango wa fedha za Benki ya Dunia *(World Bank)* na tunatarajia kupeleka fedha hizo Nguruka mapema iwezekanavyo mwishoni mwa mwaka huu wa fedha au mwanzoni sana mwa mwaka ujao wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusiana na hivyo vituo vya afya vinne ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja, ninafahamu ni kweli tuna vituo vya afya ambavyo vina miundombinu pungufu kwa kadiri ya *standard* ya vituo vya afya na tumeweka mpango tulianza na awamu ya kwanza ya ujenzi tumekamilisha, huduma za msingi zinatolewa. Tutakwenda na awamu ya pili na tutahakikisha pia vituo hivyo tunavipa kipaumbele kwa ajili ya kumalizia majengo hayo yanayohitajika. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wananchi wa Kata ya Kimochi wana hamu kubwa sana ya kupandisha Zahanati ya Shia iwe kituo cha afya. Je, Serikali iko tayari kusaidia wananchi hawa kufikia azma yao hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali tuliweka utaratibu kwa kila zahanati ambayo menejimenti ya wilaya inaona kuna sababu ya kuipandisha hadhi kuwa kituo cha afya kuna utaratibu ambao wanatakiwa kuufuata. Kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kwamba wafanye tathmini kwenye hiyo Zahanati ya Shia kwa maana ya idadi ya wananchi waliopo, lakini pia ukubwa wa eneo na walete maombi ya kupandisha hadhi kuwa kituo cha afya ili Serikali ifanye tathmini na kutenga fedha kwa kushirikiana na halmashauri na Serikali Kuu kwa ajili ya kupandisha hadhi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ku-*declare interest,* Baba mkwe, juzi nilikuwa pale kwenye msiba na nikushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Mbunge pamoja na Mheshimiwa Diwani walilileta jambo hili kwa njia hiyo hiyo. Niseme tu kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri basi Mkurugenzi aharakishe kukamilisha taratibu hizo ili Wizara yetu, Wizara ya TAMISEMI, Mheshimiwa Mbunge pamoja na Diwani wake walivyolileta Serikali iweze kulifanyia kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa majibu ya nyongeza na *commitment* ya Serikali kwenye hoja ya Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Niseme kwamba ninaishukuru sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kwa kunijengea Kituo cha Afya cha Mtii na Kituo cha Afya cha Myamba, lakini vituo hivi vya afya vyote viwili vimeletewa vitanda vya kulalia wagonjwa, lakini wodi kwa

ajili ya kulala wagonjwa bado hazijajengewa. Mheshimiwa Waziri, utawaambia nini hawa wananchi ambao wana hamu ya kuona kwamba wale wanaozidiwa wanalala hospitalini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwahakikishie wananchi wa Jimbo la Same Mashariki kwamba Serikali imeshapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivyo vya afya vya Mtii na Myamba na tunafahamu kwamba wameshaanza kupata huduma katika vituo vile, lakini tunafahamu kwamba kuna upungufu wa majengo hususan wodi, wodi za wanaume, wanawake na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwahakikishie kwamba Serikali imeweka mpango mkakati wa kwenda kujenga majengo hayo katika hivyo vituo viwili, lakini pia katika vituo vingine vyote hapa nchini ambavyo vina upungufu wa miundombinu hiyo tutakwenda kujenga kwa awamu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Omari Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sensa ya mwaka juzi Kata ya Kibirashi ina watu takribani 34,000, lakini wananchi wao hawana kituo cha afya. Je, nini mpango wa Serikali wa kuwajengea kituo cha afya? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Kibirashi tayari imeshaingizwa kwenye kipaumbele cha vituo vya afya vya kimkakati kwa sababu inakidhi vigezo kwa idadi ya wananchi 34,000 *plus*. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Kigua kwamba tuko kwenye utaratibu wa kutafuta fedha kwa ajili ya kwenda kujenga kituo hicho cha afya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Magessa.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itaongeza majengo kwenye Kituo cha Afya cha Chikobe ambacho kilijengwa mwaka 1977? Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilifanya tathmini na kuorodhesha vituo vya afya vyote vikongwe hapa nchini ambavyo vimejengwa miaka ya 1980 kurudi chini kikiwemo Kituo cha Afya cha Chikobe ambacho kimejengwa mwaka 1974 na Serikali inatambua kwamba miundombinu ile ni chakavu, lakini pia ni pungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeshaorodhesha vituo vya afya 215 ambavyo ni vikongwe na chakavu kikiwemo Kituo hicho cha Afya cha Chikobe. Baada ya kukamilisha ukarabati wa hospitali za halmashauri zilizosalia tutatenga fedha na tutakwenda kukarabati na kuongeza miundombinu hiyo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kituo cha Afya cha Mwangalanga kina upungufu mkubwa wa majengo ya wodi kwa ajili ya akinamama, watoto na akinababa. Ni lini sasa Serikali itakwenda kujenga majengo hayo muhimu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaanza utekelezaji wa awamu ya pili wa ujenzi wa miundombinu katika vituo vya afya vyenye majengo pungufu na tutatoa kipaumbele katika kituo hicho cha afya katika Jimbo la Kishapu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 70

**Ujenzi wa Stendi ya Kisasa Jiji la Arusha**

**MHE. MRISHO M. GAMBO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza na kumaliza ujenzi wa stendi ya kisasa ya Jiji la Arusha katika eneo la *Bondeni City*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Jiji la Arusha ni miongoni mwa Miji 45 wanufaika wa Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Miji ya Tanzania *(TACTIC)*. Jiji hili lipo katika kundi la kwanza ya utekelezaji yenye Miji 12 ambapo tayari miradi ya awamu ya kwanza ya barabara na mitaro yenye thamani ya takriban shilingi bilioni 20 ilianza kutekelezwa kwa kusaini mikataba ya Ujenzi Septemba, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa wakandarasi wenye vigezo kupitia zabuni zilizotangazwa Machi, 2024, katika miji minne ikiwemo Halmashauri ya Jiji la Arusha, Serikali imetangaza zabuni ya kumpata mkandarasi kwa mara ya pili *(Re-advertisement)* tarehe 11 Machi, 2025. Mchakato huu unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Aprili, 2025 ambapo mshindi atatangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji unatarajiwa kuanza mwezi Mei, 2025 ambapo ujenzi huu unatarajiwa kuwa wa mwaka mmoja na unatarajiwa kukamilika ifikapo Mei, 2026. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gambo.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametutafutia Mradi wa *TACTIC* kwa ajili ya kujenga stendi hii na fedha zipo. Sasa nina maswali yangu mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; tumekuwa tukipata majibu ya Serikali ndani ya Bunge hili ambayo hayatekelezeki zaidi ya mara nne. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kujiuzulu endapo ikifika Mwezi Mei mwaka huu mkandarasi hajakwenda *site* kule *Bondeni City* kwa ajili ya kuanza ujenzi wa stendi ya kisasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kumekuwa na baadhi ya viongozi wamekuwa wanatoa kauli ya kwamba mchakato wa ujenzi wa stendi umekwama kwa sababu ya Mbunge. Je, Serikali iko tayari kutoa majibu kwa wananchi wa Jimbo la Arusha Mjini, ni nini hasa kinakwamisha kuanza kwa ujenzi wa stendi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumhakikishia Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini, kwamba tunafahamu ni kweli Serikali imekuwa na dhamira ya dhati kama ilivyo dhamira ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kutenga mabilioni ya fedha kwa ajili ya ujenzi wa stendi na miundombinu mbalimbali katika Jiji la Arusha. Ni kweli kwamba baadhi ya miundombinu kazi imeanza, lakini tunafahamu sana umuhimu wa stendi ya *Bondeni City* katika Jiji la Arusha, ila lazima taratibu za manunuzi zifuatwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitangaza zabuni, wazabuni walipatikana, lakini hawakukidhi vigezo kwa mujibu wa Sheria na Taratibu za Manunuzi na Serikali isingeweza kuendelea kumpa mkandarasi ambaye hajakidhi vigezo, ingekuwa ni ukiukaji wa sheria. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali ni thabiti iko palepale na sasa tuko hatua za mwisho za kumpata mkandarasi na tunaamini ifikapo mwezi Mei mwaka huu ujenzi utaanza na utakamilika ndani ya wakati ifikapo mwezi Mei, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, si kweli kwamba Mheshimiwa Mbunge wa Arusha Mjini ndiye anayekwamisha ujenzi wa Stendi ya *Bondeni City*. Si kweli kwa sababu taratibu za manunuzi zimekuwa zikiendelea na kumekuwa na upungufu kwa wakandarasi waliopatikana na Serikali imeendelea kuhakikisha kwamba inafanya *re-advertisement* ili mkandarasi sahihi kwa mujibu wa sheria apatikane. Kwa hiyo, ninaomba niwahakikishie wananchi wa Jiji la Arusha kwamba Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo hilo amekuwa akifuatilia mara kwa mara na Serikali hii sikivu ya Awamu ya Sita itahakikisha inatekeleza mradi huo kwa wakati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mkoa wa Mbeya ni Jiji, lakini hauna stendi yenye hadhi ya jiji. Niliuliza swali hili na wananchi wa Mkoa wa Mbeya wamenituma niulize tena kwa sababu majibu yale hawayakuelewa vizuri. Je, ni lini Serikali itajenga stendi ambayo ina hadhi ya Jiji la Mbeya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli na ni muhimu sana Jiji la Mbeya kuwa na stendi ya kisasa inayofanana na hadhi ya jiji na Serikali hii imeweka kipaumbele na imeweka mipango ya kwenda kutekeleza ujenzi wa stendi ya kisasa katika Jiji la Mbeya. Ninafahamu kwamba Jiji la Meya ni moja ya majiji ambayo yako kwenye mpango wa *TACTIC* na ninafahamu katika *package* ya *TACTIC* tutahakikisha pia tunaweka utaratibu wa kuanza ujenzi wa stendi hiyo mapema iwezekanavyo na kwa wakati ili Jiji la Mbeya na wananchi wake wapate huduma bora za usafiri. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fatma Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Je, lini Serikali

itajenga stendi ya kisasa katika Jiji la Dodoma hasa kwa ajili ya daladala kwani eneo la *Nyerere Square* limekuwa na msongamano mkubwa sana na kuleta karaha kwenye nchi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie tu Mama yangu Mheshimiwa Toufiq kwamba Serikali hii moja ya kipaumbele kilichowekwa kwenye miundombinu ya usafiri ni kujenga stendi za kisasa za mabasi lakini pia stendi za kisasa za magari madogomadogo kwa maana ya daladala. Jiji la Dodoma ni Makao Makuu ya nchi na ni Jiji linalokua kwa kasi, nimhakikishie tu kwamba, tayari mipango imeshawekwa kwa ajili ya kwenda kujenga stendi hizo kwa awamu. Kwa hiyo, tutakwenda kujenga stendi hiyo ili usafiri huo pia uwe katika mazingira bora zaidi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata namba 71. Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 71

**Mikopo Kutolewa kwa Uwiano Unaozingatia Usawa**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA** aliuliza:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika kuhakikisha fursa zote za mikopo zinatolewa kwa uwiano unaozingatia usawa katika halmashauri zote?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imesanifu mfumo wa kidijiti wa *WEZESHA Portal*, Mfumo wa Kugawa Mapato ya 10% ya Halmashauri kwa Makundi Maalumu ili kuhakikisha kuwa taarifa za mikopo zinachakatwa na kusimamiwa kwa uwazi na kwa usawa ili kuondoa dosari mbalimbali wakati wa utoaji wa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imeweka utaratibu ambao maombi yote ya mikopo hujadiliwa katika Kamati ya Huduma ya Mikopo ngazi ya kata; Kamati hiyo ngazi ya halmashauri na Kamati hiyo ngazi ya wilaya kufanya uhakiki wa mikopo, lakini timu ya menejimenti, Kamati ya Kudumu ya Fedha, Uongozi na Mipango na Kamati ya Kudumu ya Fedha na Utawala; Baraza la Madiwani; Kamati ya Bajeti ya Halmashauri; na mwisho Kamati ya Uratibu wa Mikopo ngazi ya mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu uliofanywa na kuidhinishwa na Serikali unatoa fursa kwa mikopo inayotolewa na Halmashauri kwa wajasiriamali wa makundi maalum kuwa na usawa na kuwezesha kufanya shughuli za kiuchumi na kujiongezea kipato. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mwandabila.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kufahamu wamechukua hatua gani kuhakikisha halmashauri zote zinakuwa na Maafisa Mikopo kwa kuwa wanatoa mikopo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, nataka kufahamu kwa kuwa Wizara mbalimbali zimekuwa zinatoa mikopo kupitia halmashauri zetu na kumekuwa na halmashauri ambazo mpaka leo zinadaiwa kwa muda wa miaka mingi. Je, wao kama Wizara wamefanya hatua gani kuhakikisha halmashauri zinazodaiwa na Wizara zinalipa mikopo yao? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, ni kweli kwamba tunafahamu katika halmashauri zetu tunatoa mikopo ya 10% kwa makundi maalum. Maafisa Maendeleo wa Halmashauri na maafisa wengine wa halmashauri ni viongozi ambao wanasimamia mikopo hii ya 10% na wanafanya kazi kama Maafisa Mikopo katika halmashauri hizi. Kazi inayofanyika ni kuendelea kuwajengea uwezo wa kifedha wa kusimamia na kuratibu vizuri shughuli za mikopo ya 10%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, mpaka sasa tangu tumeanza mikopo hiyo tunakwenda vizuri na Serikali inaendelea kufanya uratibu na usimamizi wa karibu ili Maafisa Maendeleo ya Jamii na maafisa wengine wa halmashauri waweze kusimamia vizuri mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kwamba, kweli kuna halmashauri zinakopeshwa na Wizara mbalimbali (Wizara ya Ardhi na Wizara nyingine). Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumeendelea kusisitiza na kusimamia marejesho ya fedha hizo kwenye Wizara husika kutoka kwenye halmashauri na tutaendelea kufanya hivyo. Pia, marejesho yanatia moyo kwa sababu kwa kiasi kikubwa halmashauri zimeendelea kurejesha mikopo yao. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Josepha Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wengi katika kata zetu hawajanufaika na mikopo hii. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kufikisha hiyo huduma ya elimu kwa wanawake pamoja na hao Maafisa Mikopo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maboresho ya mfumo wa mikopo ya 10%, tofauti na huko nyuma sasa tuna Kamati za Mikopo kuanzia ngazi za vijiji na mitaa. Moja ya kazi za Kamati zile za mikopo ni kuwatambua akinamama, vijana na watu wenye ulemavu wenye sifa za kupata mikopo hiyo ili kuwapa elimu na mbinu za ujazaji

wa maombi yao kupitia mfumo wa kielektroniki ili waweze kupata mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ngazi ya mikoa pia kuna kamati ambazo zinahusika na elimu, uhamasishaji na usimamizi kuanzia ngazi ya halmashauri mpaka ngazi ya wilaya. Kwa hiyo, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, bado tunahitaji kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie pia, nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kuwaelekeza Wakurugenzi wa Halmashauri kote nchini, Maafisa Mikopo (Maafisa Maendeleo) na Kamati zote zinazoratibu mikopo kwa ngazi ya vijiji, kata na halmashauri zihakikishe zinaendelea kuwaelimisha wananchi na kuwawezesha kujaza maombi ya mikopo hii ili wengi waweze kunufaika kama ilivyo dhamira ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kumekuwa na changamoto nyingi sana kwa akinamama, vijana na watu wenye ulemavu kupata hizo fedha. Kabla hawajapata hizo fedha kumekuwa na mtiririko mkubwa wa utoaji fedha kwa maana ya kwamba, kuandikiwa maandiko na hayo mambo mengine ambayo ni changamoto. Kwa nini Serikali isiweke utaratibu mzuri wa hawa akinamama, vijana na watu wenye ulemavu kupata fedha hizo kabla hawajatumia fedha nyingi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tuna mikopo hii ya 10% na mahitaji ni makubwa zaidi kuliko upatikanaji wa fedha zenyewe. Pia, uzoefu unaonesha kwamba, vikundi vingi vinaomba mikopo hiyo kwa pamoja na halmashauri inatoa kwa awamu kutokana na upatikanaji wa fedha. Ndiyo maana kuna baadhi ya vikundi vinakuwa vimeomba mikopo hiyo vinasubiri kwa muda mrefu

kidogo, kwa sababu baada ya kutoa ile mikopo kunakuwa kunahitajika muda wa kukusanya yale mapato mengine ili kuweza kuwakopesha. Kwa hiyo, ni moja ya sababu ambayo inachelewesha baadhi ya vikundi kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, sababu nyingine ni kweli kwamba kuna baadhi ya maafisa wetu hawasimamii kwa uthabiti na kuwawezesha vikundi kupata mikopo kwa wakati. Pia, Serikali ilishatoa maelekezo kwamba Maafisa Mikopo (Maafisa Maendeleo ya Jamii) kote nchini na Wakurugenzi wa Halmashauri zetu wahakikishe vikundi vyenye sifa vilivyokidhi vigezo na ambavyo tayari fedha ipo wapate mikopo mapema iwezekanavyo ili waendelee na shughuli zao badala ya kwenda na kurudi mara kwa mara. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu ya Serikali kwa hoja za Wabunge.

Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 72

**Malipo ya Waliokuwa Wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawalipa wastaafu waliokuwa wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjwa mwaka 1977?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba.

**WAZIRI WA FEDHA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mipango na Uwekezaji, ninaomba kujibu swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliokuwa wafanyakazi wa lililokuwa Shirika la Posta na Simu Tanzania *(Tanzania Posts and Telecoms Corporation)* pamoja na Shirika la Reli la iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, walilipwa mafao yao ya mkupuo kupitia Ofisi ya Mlipaji Mkuu wa Serikali mwaka 2005. Hata hivyo, baada ya malipo hayo, baadhi yao walirudi kudai mapunjo ambapo Wizara iliyafanyia kazi kulingana na taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009 Serikali iliwarejesha wastaafu hao kwenye daftari la pensheni ambapo wanalipwa kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina. Wastaafu hao kwa sasa wanalipwa pensheni yao ya kila mwezi kwa utaratibu wa miezi mitatu, mitatu. Aidha, hadi sasa Serikali imelipa pensheni ya kipindi cha Aprili, 2025 hadi Juni, 2025 kiasi cha shilingi bilioni 1,085 kwa wafanyakazi 1,794 kama ambavyo imetengwa na yaliyokuwa mashirika ya *EAC, TTCL, TRC, TPC* pamoja na *TPA*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Restituta Mbogo.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Jumuiya ya Afrika Mashariki ilikuwa na taasisi mbalimbali ambazo zilikuwa ni *Telecommunication, Cargo Handling, Railway, Airways* na *Harbors,* lakini majibu ya Serikali ni kwa taasisi mbili. Je, Serikali iko tayari kukaa na taasisi nyingine ambazo zilikuwa kwenye *East African Community* ili kuangalia madai yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa waliokuwa wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika mwaka 1977, wanadai kwamba Serikali iliwalipa pesa zao pungufu na kwamba Serikali haikufuata tathmini iliyotolewa na *liquidator*. Je, Serikali iko tayari kuunda tume na kukaa na wafanyakazi hawa ili kupata muafaka na waweze kulipwa pesa zao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza

nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia masuala haya ya wazee wetu. Niseme kwamba kwa niaba ya Serikali tunapokea wazo lake kwamba kuna baadhi ya taasisi nyingine ambazo bado wanahitaji kukaa na Serikali na Serikali imekuwa ikifanya hivyo na hivyo ndivyo ilivyovifikia hatua hii kwenye hizi taasisi nilizozitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wale wengine ambao wameongelea kama alivyotoa hoja ya mapunjo pamoja na taratibu alizozisema ili ziweze kufuatwa kikamilifu, tumelichukua. Pia, utaratibu wa Serikali wa kulipa madai na madeni punde yanapojitokeza kama hivi ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema, huwa yanafanyiwa uhakiki na hoja hizo zinaangaliwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, zinaangaliwa na Ofisi ya *Attorney General*, zinaangaliwa na Mkaguzi wa Ndani pamoja na idara nyingine zinazoshughulikia masuala ya aina hiyo. Kwa hiyo, tumelipokea, lakini Serikali itafanyia kazi maeneo hayo yote mawili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa hoja za Mheshimiwa Mbunge. Tunaendelea na swali linalofuata, swali namba 73. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Abdi Hija Mkasha, Mbunge wa Micheweni, sasa aulize swali lake.

Na. 73

**Kamera Zilizofungwa Mji Mkongwe Zanzibar**
**Kusaidia Kudhibiti Uhalifu**

**MHE. ABDI HIJA MKASHA** aliuliza:-

Je, Kamera zilizofungwa Mji Mkongwe Zanzibar zinasaidiaje katika kupambana na kudhibiti uhalifu kwenye maeneo haya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mji Mkongwe Zanzibar zimewekwa kamera na zilianza kufanya kazi kuanzia tarehe 3 Oktoba, 2018. Matumizi na usimamizi wake unaratibiwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Lengo la kuwekwa kamera ni kudhibiti uhalifu na kufuatilia matukio ya kihalifu yanayotendeka. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2018 hadi 2025 kamera hizo zimesaidia kutambua, kufuatilia na kukamatwa matukio 1,177 ya uhalifu. Uwepo wa kamera hizo, umesaidia sana kudhibiti uhalifu na matukio ya kihalifu katika maeneo ya mji Mkongwe. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdi Hija Mkasha, swali la nyongeza.

**MHE. ABDI HIJA MKASHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina swali dogo moja la nyongeza. Je, ni lini Serikali itafunga kamera za usalama katika Miji ya Pemba ikiwemo na Wilaya ya Micheweni? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdi Hija Mkasha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kwa upande wa Pemba, tayari kamera zimeshafungwa kwenye Mji wa Chakechake, Mkoani pamoja na Wete. Vilevile, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, tumetenga fedha kwa ajili ya kumalizia maeneo yaliyobaki ikiwepo Mji wa Micheweni.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri.

Tunaenda Wizara ya Ujenzi, swali namba 74. Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 74

**Kuboresha Barabara ya Kiranjeranje – Nanjirinji – Ruangwa**

**MHE. ALLY M. KASSINGE** aliuliza:-

Je, nini mpango wa kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Kiranjeranje – Nanjirinji hadi Ruangwa kwa kuanza kipande cha Kiranjeranje – Makangaga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza ujenzi wa Barabara ya Kiranjeranje – Makangaga – Nanjirinji hadi Ruangwa yenye urefu wa kilometa 120 kwa kuanza na ujenzi wa madaraja makubwa matatu (3) kwa kutumia fedha za dharura zilizotoka kwenye mkopo nafuu wa Benki ya Dunia. Madaraja haya ni Kigombo lenye urefu wa mita 25, utekelezaji wake umefikia 25%, Daraja la Nakiu lenye urefu wa mita 70, kandarasi yake ipo kwenye maandalizi ya ujenzi na Daraja la Mbwemkuru III lenye urefu wa mita 100 lipo katika hatua ya mapitio ya usanifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ujenzi wa madaraja haya matatu unaendelea, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu ya Serikali. Hata hivyo, nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa ujenzi wa madaraja haya matatu ambayo Mheshimiwa Waziri amezungumza, kasi yake ni ndogo; je, Serikali haioni umuhimu wa kuharakisha ujenzi wa madaraja haya ili barabara hii iweze kupitika kipindi chote cha mwaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kipande cha kutoka Kiranjeranje mpaka Makangaga ni kipande ambacho kimejengwa kwa mawe, kitu ambacho kinaathiri sana magari yetu ambayo yanakwenda kuchukua madini ya *gypsum* kule Makangaga. Je, kwa nini Serikali isione umuhimu wa kujenga kipande hiki angalau kwa kiwango cha changarawe wakati tunatafuta fedha kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba ujenzi wa haya madaraja yote matatu kwa sasa, kwanza tunakamilisha usanifu. Pia, madaraja haya mengine ni kati ya madaraja ambayo tunajua mito mingi sasa hivi inapeleka maji baharini na ni kati ya madaraja ambayo maji hayo yanapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna uhakika kwamba, mvua itakapokuwa imepungua na kwa sababu tuna uhakika sana na wakandarasi na chanzo cha fedha, mara tu mvua zitakapokatika, tutahakikisha kwamba madaraja haya yanakamilika. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, madaraja haya mkataba ni yakamilike ndani ya mwaka mmoja. Kwa hiyo, tutahakikisha kwamba, tunasimamia ili madaraja haya yaweze kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa hiki kipande alichokitaja, tunatambua kwamba ni kweli huku ndiko kunakotoka *gypsum* kwa sehemu kubwa na magari yanayopita kule ni magari mazito sana. Wizara imeendelea kulifanyia mchakato ili tuone kujenga barabara ambayo itakuwa na uwezo wa kubeba hayo magari mazito ambako kunatoka hiyo *gypsum*.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Kitonga ni muhimu sana kwa Uchumi wa Nchi hii kwa sababu inaunganisha Tanzania na lango la *SADC*. Hata hivyo, hii barabara ujenzi wake unasuasua kiasi kwamba magari yana-*park*

pale mpaka saa tatu hadi nne. Je, nini mkakakti wa Serikali ili kuhakikisha kwamba barabara hii haina mkwamo na inapitisha magari kila wakati? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, tutambue kuwa hii barabara ndiyo kati ya Barabara Kuu (T1) ya kutoka Dar es Salaam kwenda Tunduma na ni kati ya barabara ambazo zinashikilia uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tuna *option* mbili. Moja, ni kuipanua hiyo barabara (hicho kipande) kuwa walau njia tatu. Ni eneo ambalo lina milima na miamba na tunaendelea na mkandarasi na tunategema pengine tuongeze mkandarasi mwingine ili tuweze kuongeza kasi ya kutengeneza. Vilevile, suala lingine tunaangalia uwezekano kama tunaweza tukajenga barabara nyingine ya mchepuko ili *incase* panafunga, basi tuwe na namna nyingine ya kupita lile eneo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri. Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula, Mbunge wa Ilemela, sasa aulize swali lake.

Na. 75

**Kuanza kwa Safari za Anga za Dodoma – Mwanza - Mbeya – Arusha**

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA** aliuliza:-

Je, lini *ATCL* itaanzisha usafiri wa Ndege kutoka Dodoma – Mwanza - Mbeya na Arusha ili kupunguza gharama kwa wasafiri wanaokwenda mikoa hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ATCL* inaendelea kupanua mtandao wa safari kwa kuzingatia mpango mkakati wake na mahitaji ya soko. Kwa sasa, *ATCL* inahudumia vituo 26 kutokea Dar es Salaam vikiwemo vituo 14 vya ndani ya nchi. Safari za Dodoma – Mwanza zinatarajiwa kuanza Desemba 2025, huku tathmini ikiendelea kwa safari za Dodoma – Mbeya na Dodoma – Arusha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Angeline.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nishukuru kwa majibu ya Serikali. Hata hivyo, nisikitike tu kwamba majibu haya yamekuwa kila siku yakitia faraja kwamba zitaanza, zitaanza kwa sababu hii ni mara ya tatu nauliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya kwanza walisema wanasubiri ndege ikija. Ikaja ile ndege, lakini hawakubadilisha *route*, imekuja nyingine hawakubadilisha na leo wanasema mpaka Desemba, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba Uwanja wa Ndege wa Mwanza ni lango la Miji ya Maziwa Makuu na Makau Makuu sasa hivi Dodoma. Ili kurahisisha pia mawasiliano, hawaoni kama ni usumbufu wa watu kutoka Mwanza kwenda Dar es Salaam halafu wanakuja Dodoma wakati Mwanza pia ni Mji ambao ni wa pili kwa ukuaji wa uchumi na unazalisha sana na abiria wengi wanatoka Kanda ya Ziwa? Swali langu la kwanza; ni lini kwa uhakika usafiri huo utaanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; tunayo mashirika mengi ya binafsi ya ndege yakiwemo haya ya *AURIC* ana ndege ndogo na wanaweza kuwa pia na ndege kubwa; tunayo *Coastal line* na tunayo pia *Precision*.  Je, Serikali haioni ni muda muafaka sasa wa kuzungumza nao ili waweze kuwa na ndege kubwa zitakazoweza kufanya kazi hiyo kama tulivyoomba, Mwanza – Dodoma, Dodoma - Arusha, Dodoma – Mbeya na mambo mengine kama hayo ili kukuza uchumi wa Taifa hili katika usafiri wa anga? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Mabula kwa ufuatiliaji wake kwenye upande wa *ATCL*, lakini nimhakikishie kwamba, Serikali hii imefanya jitihada kubwa sana ya kuongeza au kuboresha usafiri nchini. Sote ni mashahidi, miaka tisa nyuma tulikuwa na ndege moja tu. Serikali imenunua ndege zimefika 16 ikiwemo ndege ya mizigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ni makubwa. Hivi ninavyozungumza hapa, tunaboresha viwanja vya ndege ambavyo havijakamilika karibu nchi nzima. Vitakapokamilika nina uhakika Wabunge wa maeneo hayo nao watakuwa wakisimama hapa wanahitaji ndege. Kwa hiyo, nichukue ushauri wake wa pili alioutoa Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa mashirika binafsi yote yanayo-*operate,* yaliyopo ndani ya nchi yetu pamoja na nje ya nchi yetu ili kutazama fursa ambayo Serikali imewekeza kwenye kujenga miundombinu ya viwanja vya ndege karibu kila mkoa, waone namna gani wanaweza kuleta ndege zao ili kuboresha usafiri, lakini na wao watafanya biashara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, kwa kifupi.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itapeleka usafiri wa ndege kuanzia Dodoma – Tabora mpaka Kigoma? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inamhakikishia Mheshimiwa Genzabuke na Wabunge wote itapeleka ndege katika maeneo mbalimbali nchini baada ya kukamilisha manunuzi kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu. Tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 76

**Athari za Mabadiliko ya Sera za Fedha kwa Mataifa Yaliyoendelea**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA** aliuliza: -

Je, hatua gani zimechukuliwa kupunguza makali ya mabadiliko ya sera za nje katika masuala ya fedha za maendeleo kimataifa kwa mataifa yaliyoendelea?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Neema Lugangira, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha tathmini ya athari zitakazojitokeza kwa miradi ambayo ilikuwa ikipata ufadhili kupitia Serikali ya Marekani. Maeneo yaliyoathirika kwa kiasi kikubwa ni pamoja na Sekta ya Afya. Aidha, miradi mikubwa iliyokuwa inagharamiwa kupitia mshirika huyo imetengewa bajeti kupitia fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na tathmini kwa maeneo mengine yanayoweza kuathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na mabadiliko ya sera hizo za nje katika masuala ya fedha kwa kuangalia washirika wengine wa maendeleo ambao Serikali ya Marekani imekuwa ikitoa mchango wao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali ninaomba kwa ufupi sana nieleze, miradi ambayo ilikuwa inafadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia *USAID* ni zaidi ya shilingi trilioni mbili, lakini pia tukiacha Serikali ya Marekani, Serikali ya Ufaransa, Serikali ya Sweden, Finland, Canada, Belgium, Netherland pamoja na *EU* zimetangaza kupunguza misaada. Sasa kwa kuzingatia mabadiliko haya ni dhahiri kwamba ni zaidi ya Sekta ya Afya ambayo inaweza ikaathirika: Sekta ya Elimu, Tehama, Kilimo, Mifugo na kadhalika. Kwa hiyo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuzingatia sasa hivi tuko kwenye bajeti, je, Serikali haioni iko haya ya kufanya tathmini ya kuondoa *non-essential costs* ili tuweze kuokoa fedha na fedha hizo zikaelekezwa kufidia hizi *gap*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ninatambua wiki ijayo Mheshimiwa Waziri ambaye ni mbobezi kabisa katika uchumi unakwenda Marekani katika mkutano wa Benki ya Dunia na Shirika la Fedha Duniani. Je, Serikali haioni iko haja ya ku-*negotiate* na Benki ya Dunia na *IMF* ili ile fedha ambayo tunalipa kwenye mikopo badala ya kulipa *principle* na *interest* tulipe tu *principal amount,* ile *interest amount* iwe *frozen* ili fedha hizo zielekezwe kwenye kufidia *gap* la hii athari ambayo imejitokeza? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake na ningekuwa na mimi natokea Kagera ningesema *in fact* yuko *current* sana. Haya anayoyaongelea ni mambo ya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumefanya tathmini hiyo na katika tathmini hiyo tayari tumeshaanza kufanyia kazi, mapendekezo haya ya kuangalia namna ya kufanya *restructuring* ya matumizi ili kuweza ku-*cover* fedha hizo ambazo zinahitajika ni jambo ambalo tumeliweka kwenye mkakati kama Serikali na tayari tumeanza utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ni jambo ambalo tutaendelea kulifanyia kazi kama ambavyo Serikali tayari iliunda timu ambayo ilikuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia sekta zote na hii ambayo tumei-*cite* ni ile ambayo ilionekana kwamba kuna eneo linahitaji kuchukua hatua za haraka kwa sababu ni afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wazo la pili la kujadiliana na taasisi ambazo tuna madeni nazo, kwamba tulipe *principal* peke yake, ni wazo zuri, tumelipokea na tunaendelea kufanyia kazi taratibu ambazo huwa zinafanyika kwenye masuala haya ya mikopo ili kuweza kunufaika na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka nchi yetu iliwahi kunufaika wakati ule kwenye mpango wa *EPIC,* lakini hata baada ya hapo kuna taratibu ambazo huwa tunaendelea nazo zikiwemo *Dedswap* pamoja na maeneo mengine. Kwa hiyo, na hili nalo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaufanyia kazi utaratibu huu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, aulize swali lake. Tafadhali Mheshimiwa Asya kwa niaba.

Na. 77

### Usimamizi wa Taasisi Zisizo za Kiserikali *(NGOs)*

**MHE. ASYA SHARIF OMAR K.n.y. MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha Taasisi zisizo za Kiserikali *(NGOs)* zinakuwa hai na zinaleta matokeo chanya kwa Taifa letu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA) K.n.y. WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuimarisha mazingira wezeshi ya utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Hatua hizo ni pamoja na:-

(a) Kuandaliwa kwa Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara (2020), Toleo la Mwaka 2024, unaoelekeza vikao kazi vya robo mwaka na ushiriki wa mashirika katika vikao vya ushauri ngazi ya Kata *(WDC)*, Tarafa, Wilaya na Mkoa;

(b) Kuandaliwa kwa Mfumo wa Kieletroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali *(NIS)* na Ramani ya Kidijiti ya Utambuzi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kurahisisha usajili, uwasilishaji wa taarifa na ulipaji wa ada;

(c) Kuanzishwa kwa Madawati ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Wizara za Kisekta ili kuboresha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi;

(d) Kuandaliwa kwa Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 2022 hadi 2027 ili kupunguza utegemezi na kuimarisha uendelevu wa mashirika. Mkakati huo utapelekea kuanzishwa kwa Mfuko wa Pamoja wa Ruzuku kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; na

(e) Kushirikiana na Wasajili Wasaidizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ngazi za Mikoa na Halmashauri. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za mashirika yasiyo ya Kiserikali kwa mujibu wa Kifungu cha 4(1)(J) cha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asya Sharif Omar.

**MHE. ASYA SHARIF OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina swali moja la nyongeza. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweka mazingira wezeshi ya kuzisaidia nchi iweze kupata fedha kutoka katika taasisi mbalimbali za Kikanda na Kimataifa? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA) K.n.y. WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Asya kwa kazi nzuri na kwa swali lake. Kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi, Serikali inaendelea kufanya kazi kwa ukaribu na *NGOs* na kwa niaba ya Serikali niendelee kuzishukuru *NGOs* zote za Tanzania kwa namna ambavyo tunashirikiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona hata mikutanao mikubwa ya kimataifa ya kikanda ambayo viongozi wetu wakuu wamekuwa wakishiriki hususan Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweza kuwakutanisha wadau mbalimbali ambao wameweza kuleta fedha kwa ajili ya kusaidia sekta ya *NGOs* ili kuweze kuleta mchango. Tunashirikiana nao na hata tunapo-*table* bajeti ya Serikali tunaweka fedha za ndani na za nje. Pia, zipo *NGOs* Kimataifa ambazo zinapata fedha kupitia mazungumzo ya ubia ya *bilateral* na mengine, tunapata fedha hizo zinaingia kwenye *NGO* kusaidia wananchi wetu katika maeneo mbalimbali. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Omar.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, je, Serikali ina mkakati gani wa kila mwezi kuzisaidia hizi asasi za kiraia ambazo sasa hivi zinapumulia mashine kutokana na hali zao za kiuchumi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA) K.n.y. WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inaomba nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Omar kwa swali lake. Hapa nimpongeze na kumshukuru Dada yetu Mkurugenzi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Ndugu Vickness Mayao kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tumesema tunaenda kufanya tathmini ya kina kuona namna tunaweza kusaidia. Kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi kule kwa Mheshimiwa Waziri Ridhiwani tumeanza upande wa Serikali kuzipa asasi zisizo za Kiserikali hususan mashirikika ya watu wenye ulemavu kupitia Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu kuwasaidia fedha ambayo inaweza kuendelea kuwasaidia, kwa hiyo, Serikali tayari tuna mkakati huo wa kuanza

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana kama una mchango wa namna nzuri tunayoweza kuyasaidia mashirika haya unaweza kutuona Serikali, lakini kwa sasa tunaenda hivyo na Waziri Mama Gwajima kwenye sekta yake anafanya vizuri, anatusaidia kuona namna ya kwenda vizuri. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali Namba 78, swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

Na. 78

**Ujenzi wa Viwanda vya Kuchakata Chumvi Mtwara**

**MHE. ESTHER N. MATIKO K.n.y MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kujenga viwanda vya kuchakata chumvi Mkoani Mtwara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI K.n.y WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutekeleza Mkakati wa Ujenzi wa Viwanda nchini ikiwemo viwanda vya chumvi. Mkakati huo unahusisha uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji, utengenezaji wa maeneo ya biashara na viwanda na uhamasishaji wa uongezaji wa thamani kwa bidhaa/malighafi kote nchini ikiwemo Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa Mikoa ya Lindi na Mtwara haikuwa na Kiwanda cha Kuchakata Chumvi, Serikali kupitia Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* inaendelea na ujenzi wa Kiwanda cha Kuchakata Chumvi Mkoani Lindi. Kiwanda hicho kitakapokamilika kitakuwa kinapokea chumvi ghafi kutoka kwa wazalishaji wadogo wakiwemo wa Mkoa wa Mtwara. Aidha, Serikali kupitia *SIDO* inaendelea kubuni teknolojia rahisi za kuchakata chumvi ikiwemo kusaga na kurutubisha chumvi kwa ajili ya kusaidia masuala ya lishe. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; sote tunakubali kwamba chumvi ni kati ya bidhaa ambazo zinatumika kila siku nyumbani na kwa asilimia kubwa chumvi ambazo zinatumika Tanzania ni *imported.* Ninataka kujua Serikali hiki kiwanda ambacho wanajenga Lindi kina uwezo kiasi gani wa kuweza kuzalisha chumvi ambayo pia tunaweza kuuza nje ya nchi na kuongeza fedha za kigeni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri pale, ni kweli kwamba sasa hivi

wananchi wa Lindi na Mtwara wanauza chumvi ile kama malighafi na thamani yake ni ndogo sana. Sasa ninataka kujua ni lini kiwanda hiki kinaenda kukamilika ili kuweza kuongeza thamani ya chumvi ile na kuleta ajira kwa wananchi hao wa Mtwara na Lindi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninampongeza Mheshimiwa Matiko kwa kuuliza haya maswali mawili ya nyongeza ambayo ni ya msingi sana katika kuielewa sekta ya chumvi inavyofanya kazi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la uwezo wa kiwanda kinachojengwa, ni kiwanda kidogo cha mfano ambacho Wizara ya Madini imewekeza katika kutafuta teknolojia rahisi ya kuwasaidia wawekezaji wengine wadogo nchini kuanzisha mitambo ya aina hiyo. Kwa hiyo, uwezo wake ni tani 15,000 mpaka tani 25,000 kwa mwaka. Kitakwenda kununua chumvi za wazalishaji wadogo wa chumvi na kuiongezea thamani ili iweze kuingia katika masoko ya ndani na hata nje pale ambapo watakuwa wamepata masoko ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa swali lake la pili kwamba ni lini kitakamilika. Kiwanda hiki ambacho sasa hivi kiko katika hatua za awali za ujenzi, msingi utakaobeba ile mitambo umefikia 70%. Kufikia mwezi Agosti, 2025 mitambo itakuwa imesimikwa na uzalishaji utakuwa umeanza na kiwanda hiki kitatumika kama kiwanda darasa kwa ajili ya vikundi mbalimbali na wazalishaji wa chumvi nchini kwenda kujifunza kutoka kule kabla Serikali haijaweza kuanzisha vituo vingine vya mfano sehemu mbalimbali nchini ambapo chumvi inapatikana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Ninaomba kumuuliza Waziri wa

Viwanda na Biashara, Wilaya ya Mbogwe ina maeneo yanye viwanda lakini tuna kiwanda kimoja tu kinachofanya kazi. Ni mpango upi wa Serikali kwenye hili eneo la viwanda ili na yale maeneo tuliyoyatenga kwa ajili ya viwanda kuwawezesha wazawa ambao wanajishughulisha na shughuli zile ili waweze kukaa kwenye shughuli za viwanda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye majibu ya swali la msingi, Wizara ya Viwanda ina mkakati mahsusi wa kuendelea kuwekeza katika ujenzi wa viwanda katika maeneo mbalimbali nchini zinapopatikana malighafi ambazo zina *warrant* au zinaruhusu kuanzisha kiwanda kwa ajili ya zao au bidhaa yoyote ambayo inaweza ikachakatwa katika viwanda ambavyo Wizara hii inaendelea kuasisi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Swali Namba 79, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Momba, sasa aulize swali lake.

Na. 79

**Kusambaza Mitambo ya Kutengeneza Gongo kwa Wananchi**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE** aliuliza:-

Je, Mitambo mingapi ya kutengeneza Gongo imesambazwa kwa wananchi wanaojishughulisha na uzalishaji wa pombe ya gongo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa viwanda vya kutengeneza pombe kali nchini inayokidhi viwango, vinaendelea kuanzishwa kwa kupata mafunzo na ushauri wa kitaalam kutoka Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo *(SIDO),* Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali *(GCLA)* na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* na miongoni mwao wako watengenezaji wanaoendelea kupata alama ya ubora kwa kukidhi vigezo.

Mheshimiwa Spika, *SIDO* itaendelea kushirikiana na taasisi nyingine za maendeleo ya teknolojia ikiwemo Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo *(TEMDO),* Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini *(CAMARTEC)* na kwa ushirikiano wa karibu wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali *(GCLA)* na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS),* kwa kuboresho teknolojia za kuchakata pombe kali kwa teknolojia rahisi ili watengenezaji wengi waweze kutengeneza pombe bora inayostahili kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, gongo ni pombe yenye kilevi ambayo imekuwa ikitengenezwa kienyeji. Aidha, Serikali haijahalalisha pombe ya gongo kwa sababu ya kuwa na madhara makubwa katika mwili wa binadamu. Kwa msingi huo, mpaka sasa hakuna mitambo ya kutengeneza kinywaji hicho iliyosambazwa kwa wananchi. Kwa sasa, Serikali haijaanzisha mpango wa kusambaza mitambo ya gongo kwa wananchi wanaojishughulisha na uzalishaji wa pombe ya gongo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Condester.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Hivi karibuni ndani ya nchi yetu tumeshuhudia kuna pombe nyingi sana ambazo ni kali zinaingizwa na zimeendelea kuwaharibu vijana na nguvu kazi ya Taifa, vijana wengi wanaendelea kuharibikiwa kwa kunywa hizo pombe kali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ikiwa hizo pombe kali zinaweza zikaingizwa zikiwa zimetengenezwa kutoka nchi nyingine, zikaingia nchini kwetu na vijana wetu wakaendelea kuharibikiwa. Serikali

imeshindwaje kuwafundisha wananchi wetu wa chini ambako huko gongo inatengenezwa na inapendwa na mpaka hivi tunavyoongea inaendelea kutumika, tumeshindwaje kuboresha gongo yetu ambayo inategenezwa na mazao ambayo yako ndani ya nchi yetu, dhidi ya kuingiza pombe kali ambazo zinawaharibu vijana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; kwa kuwa ambacho kinazidi kwenye gongo ni zile kemikali kati ya *ethanol* na *methanol.* Ni kweli kwa kuwatumia wataalam wetu kuwafuata Maprofesa pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambao wameshafanya utafiti, tumeshindwa kuendelea na zoezi hili ili kwenda kuwafundisha wananchi walioko kule chini ambao wanatengeneza kinywaji hiki, ili waweze kupata pombe bora ya gongo mfano wa Konyagi ambayo inazalishwa hapa nchini kwetu, ili kutokuendelea kuifanya gongo ni kinywaji haramu na kuendelea kukimbizana na wananchi, ilhali wananchi kinywaji hiki wanakipenda na hivi tunavyoongea wanaendelea kunywa? Ahsante. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kutetea jinsi ambavyo pombe za kienyeji zinaweza zikachakatwa kwa viwango vinavyofaa kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba siyo binadamu wote hutumia pombe, lakini kwa wale wanaotumia ni dhamira njema ya Serikali kwamba watumie pombe ambayo inafikia viwango visivyoweza kudhuru afya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kusema hayo kwa suala lake la vijana wetu kuharibiwa na pombe zinazotoka nje na pamoja na kwamba ni pombe zinazokidhi vigezo, hili suala la ulevi wa vijana linasababishwa na mambo mbalimbali ambayo ni wajibu wa jamii na malezi kufanyika kuhakikisha kwamba vijana wetu wanatambua madhara ya pombe, kwa sababu hata

gongo leo ikihalalishwa haina maana kwamba vijana watakunywa na watabakia wakiwa wastaarabu wasipoweza kunywa kwa kiasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la pili, la wajibu wa taasisi zetu za kitafiti kuweza kuchakata na kutengeneza *formula* ya kutengeneza pombe salama kutokana na pombe za kienyeji, zoezi hili linaendelea. Nimejibu katika majibu ya swali la msingi kwamba, kuna taasisi za Serikali *TBS, SIDO* na *CAMARTEC* wameendelea kufanya utafiti na kutengeneza mitambo ambayo inatengeneza pombe kali za kienyeji, ambazo zinakidhi vigezo vinavyoruhusiwa sokoni na wajibu wa kila mnywaji ni kunywa kwa kiasi asiharibu afya yake, maana hakuna pombe ambayo itakuacha salama hata kama inafikia viwango, kama utakunywa bila ustaarabu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil David Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba, mabaki ya korosho yanatengeneza pombe inaitwa *nipa*, lakini ndio gongo hiyo hiyo. Mabaki ya miwa, molasisi, yanatengeneza pombe inatumika sana kwao huko, kwa akina Mheshimiwa Saashisha na maeneo mengine inaitwa *piwa*. Tanga wanatumia miwa muhogo pamoja na mafenesi kutengeneza pombe hizo hizo. Sumbawanga wanatumia mahindi na maeneo mengine. Sasa wakulima wana nia ya kutaka kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa endapo Serikali inasema haijahalalisha pombe ya gongo kwa sasa kwa sababu ya madhara hayo yaliyotajwa na sisi tumetoa mifano pombe zinazoingizwa kutoka nje zenye madhara yanayofanana. Shirika la Viwango *TBS,* miaka mitatu, minne, iliyopita Mkuu wa Mkoa wa Mtwara alipeleka aina, *sample,* ya gongo kutoka vijiji mbalimbali vya Jimbo la Ndanda kwenda kupima na kuona uhalali wake. Walisema kwamba, haina madhara makubwa ya kibinadamu, lakini pia, *alcohol percentage* yake ilikuwa ni *moderate,* haifanani hata na pombe zinazoingizwa kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo Serikali haioni haja ya kununua mazao haya ya ziada kutoka kwa wakulima ambayo yangefaa kutengeneza *alcohol, methanol* pamoja na *spirit,* ili waweze kuyaangamiza na kufanya wananchi wasipike hizo gongo ambazo sasa haziruhusiwi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza ndugu yangu, Mheshimiwa Mwambe, kwa swali lake la msingi sana na ambalo amelipangilia kwa namna ambayo sehemu ya pili, ametoa ushauri kwamba, kwa nini Serikali isiangalie bidhaa ambayo inaweza ikatengeneza pombe isiyo na madhara na kuitengenezea viwango, ili iweze kutengenezwa na kuuzwa kibiashara kunufaisha jamii kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tunalichukua, kama Serikali, lakini hili la bidhaa zingine ambazo zinatengeneza pombe; ili uweze kutengeneza kitu chenye kiwango na salama kwa mwili wa binadamu ni lazima tuangalie *ingredients* zinazowekwa mule. Nadhani shida ya gongo, maana ndio lilikuwa swali la msingi ni kwamba, vitu vinavyotumika kutengeneza gongo hauwezi kulinganisha na vitu vinavyotumika kutengeneza pombe inayotokana na korosho, miwa au hata asali. Kwa ile jamii ya watu wanaokaa misituni ambao pia, wanatengeneza pombe ya asali na kuchanganya na mitishamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni wajibu wa Serikali. Serikali imesikia ushauri wa Mheshimiwa kufanya utafiti zaidi na kugundua aina mbalimbali ya pombe za kienyeji ambazo zinafikia viwango vya usalama viweze kutengenezwa bila pingamizi na wananchi waweze kutumia kwa manufaa yao.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, sasa aulize swali lake.

Na. 80

**Ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji Mughamo, Singida Kaskazini**

**MHE. ABEID R. IGHONDO** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji katika Jimbo la Singida Kaskazini utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji ambayo imefikia hatua mbalimbali. Mradi wa Skimu ya Mughamo kwa sasa upo katika hatua ya kukamilisha usanifu. Usanifu huo utakapokamilika, taratibu za kutangaza, kwa ajili ya kupata mkandarasi zitaanza mara moja. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ighondo Ramadhani.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu hayo mazuri ya Serikali, ambayo naomba kasi isiongezeke, ili *scheme* hiyo iweze kuanza utekelezaji wake mara moja, ninayo maswali mengine mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; ni hatua gani ambayo imefikiwa ya kuwezesha miundombinu ya umwagiliaji katika Mabwawa ya Kisisi, Masoheda, Mwahirimbi, Ntambuko, Endeshi pamoja na Mgori, ambayo niliwahi kuuliza swali la msingi hapa, kwamba, kungeanza utekelezaji, lakini mpaka sasa sijaona?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; katika Jimbo la Singida Kaskazini tuliahidiwa na Serikali kwamba, tutapatiwa visima virefu 150 vya umwagiliaji katika vijiji mbalimbali, ambavyo vina mabonde mazuri yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, lakini

mpaka sasa hakuna kinachoendelea. Je, ni hatua gani sasa ambayo Serikali inawaahidi wananchi wa Singida Kaskazini ambao walisubiri visima hivyo kwa hamu sana? Ninashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika maeneo yote ambayo ameyataja ikiwemo Kisisi, Migori najua kwamba, miradi hii ipo katika hatua mbalimbali. Moja ya wajibu wetu sisi, kama Wizara, ni kuendelea kutafuta fedha, ili kuitekeleza na mingine tunaendelea kuifanyia usanifu, ili kuhakikisha tunapata gharama halisi ya mradi, ili twende katika hatua ya mwisho ya kutafuta mkandarasi. Kwa hiyo iko katika hatua mbalimbali na ninaweza kukupa takwimu zake baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu visima 150 ni kwamba, tutatekeleza miradi hiyo kama tulivyoahidi. Sasa hivi Wizara ya Kilimo tayari tumenunua magari ya uchimbaji wa visima manne, mawili yameshafika yapo pale Wizarani na mawili yako kwenye meli, kwa ajili ya kuja hapa nchini, ambayo ni ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Kwa hiyo, tunataka kuhakikisha kwamba, ile ahadi ya visima 10,000 ambayo tumeahidi kupeleka katika majimbo inatekelezeka kwa vitendo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tuna Wabunge zaidi ya saba ambao wangependa kuuliza haya maswali. Ninaomba nimwelekeze tu Mheshimiwa Naibu Waziri awasiliane na Mheshimiwa Asia Halamga, Mheshimiwa Mashimba Ndaki, Mheshimiwa Maimuna Pathan, Mheshimiwa Flatei Massay, Mheshimiwa Daktari Samweli Hhayuma pamoja na Mheshimiwa Kakoso, kwa ajili ya kufafanua miradi ambayo inaendelea kwenye maeneo yao.

Waheshimiwa Wabunge, swali namba 80.

Na wale wote ambao hawajaleta *memo* wawasiliane na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa ajili ya majibu.

Tunaendelea na Wizara ya Mifugo, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, sasa aulize swali lake.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Boniphace Getere, naomba swali lake lipate majibu.

**MWENYEKITI:** *Order, order. Order please.*

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Boniphace Getere, naomba swali lake lipate majibu ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kuhusu Utaratibu.

Ni lazima utajwe na Meza kabla hujauliza swali. Mheshimiwa Ester Bulaya. *(Makofi)*

Na. 81

**Ujenzi wa Mnada wa Mifugo - Bunda**

**MHE. ESTER A. BULAYA K.n.y. MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ahadi ya ujenzi wa Mnada wa Mifugo Mngeta, Bunda?

**MWENYEKITI:** Swali Namba?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Swali Namba 81.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mifugo na Uvuvi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali haikuweka kwenye mpango ujenzi wa minada mipya hapa nchini ili kutoa fursa ya ukamilishwaji wa minada 23 ya awali

iliyopo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Serikali ina jukumu la moja kwa moja la kujenga na kuendesha minada ya upili na mpakani, hivyo Wizara itaendelea kuweka katika mpango wa bajeti ujenzi wa minada ya awali nchini, ikiwemo mnada wa Mifugo Mngeta kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika bajeti ya mwaka 2023/2024, Serikali ilitenga jumla ya shilingi 435,238,870, kwa ajili ya ujenzi wa mnada wa Bitalaguro uliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda. Aidha, Mwezi Februari, 2025 ujenzi wa mnada huo ulikamilika. Hivyo, kukamilika kwa ujenzi wa Mnada wa Bitalaguro utatoa fursa kwa wananchi wa Halmashauri ya Bunda kuuza na kununua mifugo katika mnada huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; suala la Mnada wa Mngeta ni la muda mrefu, tunaitaka Serikali ihakikishe inatujengea Mnada wa Mngeta. Ni lini Serikali mtahakikisha mnajenga Mnada wa Mngeta?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ni kweli, Serikali imejenga Mnada wa Bitalaguro katika Jimbo la Bunda Mjini, lakini ule mnada uko kwenye hali mbaya na mazingira ni mabovu. Je, ni lini Serikali itahakikisha inaweka mazingira rafiki ya Mradi wa Bitalaguro ili wafugaji wetu waweze kwenda kuuza mifugo yao kwenye mnada wenye staha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hili la kwanza, la ujenzi wa Mnada wa Mngeta. Utakumbuka kwamba, Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakichangia mada mbalimbali humu Bungeni na tumekwishapokea maelekezo ya Kamati yetu ya Mifugo wakielekeza kwamba, minada hii tunapoianzisha, tuhakikishe kwamba, inakamilika. Sasa hatuwezi kuwa tunaanzisha minada, tunajenga kwa 20% tunauacha, tunajenga tena mwingine, 30%

tunauacha. Ndiyo maana tukasema kwanza tukamilishe miradi yote ya minada iliyoko ndani ya nchi yetu, ikishakamilika hiyo, basi ndiyo tunaweza tukaanza kujenga minada mipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huu wa Mngeta nimwombe sana Mheshimiwa Mbunge, kwa niaba ya Mheshimiwa Getere kwamba, asubiri tutakapokamilisha minada yote 23 tunayoijenga nchini ndipo tutaanza kujenga mnada mpya na ndiyo imekuwa ni maelekezo ya Bunge na Wabunge wengi wameshauri hivyo kwamba, tujenge minada, tukiikamilisha ndiyo tuanze minada mipya. Kwa hiyo, huu wa Mngeta tutaujenga kama tutakuwa tumekamilisha miradi yote ya maendeleo iliyopo ndani ya Wizara yetu ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii miundombinu ya Bitalaguro; miundombinu tutaendelea kuikarabati, tumeshajenga choo, tumeshajenga ofisi, tumejenga uzio. Kwa hiyo, tunaendelea kukarabati taratibu kadri ya upatikanaji wa fedha. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mara fedha zinapopatikana tutapeleka kwenda kukarabati. Pia, niiombe na halmashauri, kwa sababu inapata mapato huko, iweze kukarabati katika miundombinu midogo midogo ambayo inahusiana na maeneo yao. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Hai tulileta maombi maalum ya ukarabati wa majosho katika Kata ya Kia, Weruweru na Rundugai. Je, lini Serikali itaanza kufanya ukarabati wa majosho haya? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tulipokea maombi ya Mheshimiwa Mbunge na nitumie nafasi hii kumpongeza sana. Majosho haya tumeshayaingiza kwenye utaratibu, mara tutakapopata fedha tutakwenda kuyakarabati, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edward Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Bajeti ya 2024/2025 walitenga pesa, shilingi milioni 500, kwa ajili ya Mnada wa Dosidosi. Ni lini mradi huu utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya *mobilization* ya fedha. Mara tutakapopata fedha tutakwenda kumalizia Mradi huo wa Dosidosi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru. Tumemaliza eneo linalohusu maswali, lakini kwanza naomba tukumbushane maelekezo ya Mheshimiwa Spika kwamba maswali yawe kwa ufupi na majibu pia, yawe kwa ufupi na kwa umahususi. Leo tumewanyima fursa Wabunge wengi kwa sababu, maswali yamekuwa marefu sana na majibu pia, yamekuwa marefu.

Ninaomba nirejee kwenye swali namba 80 la Wizara ya Kilimo na Mheshimiwa Naibu Waziri yuko hapa, linahusu masuala ya umwagiliaji. Wabunge ambao walisimama ni wengi sana na vikaratasi ambavyo vilikuja hapa mbele ni vingi sana, inaashiria kuna maswali mengi kwenye eneo hilo. Ninaomba Mheshimiwa Waziri alisimamie hilo jambo kwa ukaribu zaidi na awasiliane na Waheshimiwa Wabunge kuona ni namna gani litakamilika kwa wakati.

Waheshimiwa Wabunge, tunayo matangazo ya wageni waliopo Bungeni:-

Wageni waliokaa kwenye Jukwaa la Spika; tunaye mgeni wa Mheshimiwa Waziri Ndugu Joyce Mapunjo, ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na Watumishi wa Umma *(PSSSF)*. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge, Mgeni wa Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani

ya Nchi, ambaye ni mpiga kura wake kutoka Babati Vijijini, Mkoani Manyara. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 13 wa Mheshimiwa David Ernest Silinde, Naibu Waziri wa Kilimo, ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Utawala kutoka Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

Vilevile wapo Wageni 26 wa Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, ambao ni wanafunzi 22 na Walimu wanne wa Shule ya Msingi Haki kutoka Jijini Dar es Salaam.

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, ambaye ni Ndugu Hafsa Ramadhani, mtoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibu sana mtoto wetu, karibu sana Bungeni.

Wapo wageni 11 wa Mheshimiwa Felister Deogratius Njau, ambao ni Wanawake Wafanyabiashara (*Team No Excuse*) kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, ambaye ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Arusha. Karibu sana Mwalimu. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Omar Ali Omar, ambao ni Ndugu zake kutoka Zanzibar. Karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Sylvia Sigula Nyanda, ambaye ni Meneja wa *Vodacom* kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 34 wa Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, ambao ni Kwaya ya Wanafunzi na Wanamaombi wa UKWATA kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wapo wanafunzi 80 na Walimu tisa kutoka Shule ya Msingi Precious, kutoka Wilaya ya Arumeru, Mkoani Arusha. Karibuni sana, ahsante vijana wetu. *(Makofi)*

Kuna wanafunzi 20 na Walimu saba wa Shule ya Sekondari Tubuyu, kutoka Mkoani Morogoro. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tuna vilevile wanafunzi 12 na Mwalimu mmoja wa Shule ya Sekondari Shaban Robert ya Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Hoja za Serikali. Tutaendelea na uchangiaji, tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, atafuata Mheshimiwa Najma Murtaza Giga na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda ajiandae.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii kukupongeza wewe kwa kazi kubwa ambayo unaifanya. Hili ni Bunge letu la mwisho, lazima tukupongeze wewe kwa sababu, tulikuchagua na umetuwakilisha vyema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kazi wanayoifanya. Pia, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwa miaka hii minne. Wote ni mashahidi tulianza naye, lakini Mungu amesaidia tunamalizanaye na kazi kubwa imefanyika Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimpongeze Waziri Mkuu wetu kwa kweli, umemsaidia vizuri sana Mheshimiwa Rais. Umekuja kwenye majimbo yetu, umemsemea vizuri Rais,

umekitetea Chama Cha Mapinduzi, vilevile umetusemea sisi Wabunge wako vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hilo, Waziri Mkuu vilevile wakati anazunguka kwenye majimbo yetu kwa kweli, alitekeleza vizuri sana kazi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu tuliona alikuwa akishughulikia mambo mengi ya Serikali, hususani kwenye matumizi ya fedha, miradi ya maendeleo na mambo mengine. Kwa hiyo, nimpongeze sana kwa kuwa mwakilishi mwema wa Mheshimiwa Rais na kwa kweli ameitendea haki nafasi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maeneo machache ya kuchangia katika Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Eneo la kwanza ni upande wa *SGR*. Kwanza, niipongeze sana Serikali na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais ambaye alichukua ujenzi wa reli ya kisasa ukiwa takribani 30% kwa kipande cha kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma mpaka Makutupora. Ninyi ni mashahidi, kwamba Mheshimiwa Rais aliweka *commitment* kubwa na sasa hivi tumeshuhudia, wananchi wameshudia, ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma umekamilika na kazi imeanza kuonekana. Ninaomba tumpongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hilo *data* zinatuonyesha kuwa ndani ya miezi saba tangu *SGR* ilipoanza kufanya kazi wamekusanya si chini ya bilioni 54. Wastani wa wasafiri kwa miezi saba ni takribani milioni moja na laki nane na kwa mwezi takribani wasafiri laki mbili na nusu wanatumia usafiri wa *SGR,* haya ni mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hilo pia wote ni mashahidi, mbali ya usafiri wa ndege ambao wachache walikuwa wana uwezo wa kutumia sasa tumepunguza sana mwendo wa kukaa barabarani, kutoka masaa tisa hadi kumi hadi masaa matatu na manne. Haya ni mafanikio makubwa sana kwa Serikali ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna *lots* ambazo tulishasaini mkataba. Kipande cha Dodoma hadi Makutupora kipo zaidi ya

asilimia 90 kuna *lot* ya kutoka Makutupora hadi Kigoma, *lot* ya kutoka Makutupora hadi Mwanza. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, tumetembelea tumeona kazi ambayo inaendelea na ni kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sasa Serikali kwa sababu tayari tumeona tija ya uwekezaji kwenye *SGR* ni vizuri sasa bajeti inayokuja ikaweka nguvu kubwa kwenye ujenzi wa *SGR* ili tukamilishe reli ya kwenda Kigoma na ya kwenda Mwanza; hilo niliona niishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni kilimo. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais na vilevile Mheshimiwa Bashe kwa kuweka nguvu kubwa sana kwenye kilimo. Sisi sote ni mashahidi bajeti ya kilimo ime-*triple* kwa hii miaka minne, vilevile bajeti ya umwagiliaji ime-*triple* kwa hii miaka minne. Katika Jimbo langu la Manyoni Mashariki tumepata miradi mikubwa ya umwagiliaji. Tuna Mradi wa Umwagiliaji wa Mbwasa wa bilioni 18 ambao tayari mkandarasi alishasaini mkataba, amekwishakabidhiwa *site* na wakati wowote ule ataanza kufanya kazi; haya ni mafanikio makubwa. Pia tuna miradi mingine ya umwagiliaji Manyoni, Mradi wa Udimaa pamoja na Ngaiti, Msemembwa na kwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu hapa ni kwamba, mwaka huu tumeona wenyewe Waheshimiwa Wabunge kwamba mvua hakuna. Sasa Serikali kupitia Wizara ya Kilimo ijikite kwenye kilimo cha umwagiliaji. Tuangalie nchi za wenzetu ambao wamejikita kwenye kilimo kama vile Australia, Ugiriki na maeneo mengine. Hawa hawategemei mvua na badala yake wanategemea kilimo cha umwagiliaji. Kwa sababu hiyo ningeshauri sasa Serikali iweke *commitment* kubwa kwenye bajeti hii na bajeti ya Wizara ya kuhakikisha kwamba tunapeleka fedha nyingi kwenye kilimo cha umwagiliaji ili wananchi wetu waweze kulima mara tatu hadi mara nne kwa mwaka. Kwa kupitia hilo tutakuwa tumemkomboa mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kama nilivyosema, kwamba mwaka huu ni mwaka wa ukame sana. Sasa je, Serikali imejipanga vipi kuhusiana na kuwasogezea wananchi mahindi ya

bei nafuu? Kama mwaka jana tulivyofanya, Mheshimiwa Rais kwa kweli alitusaidia sana Waheshimiwa Wabunge; mahindi ya bei nafuu yalifika kwenye Majimbo yetu. Wananchi wanauliza Serikali imejipangaje mwaka huu kupeleka mahindi ya bei nafuu kwa kupitia *NFRA* kwa sababu mwaka huu siyo mwaka mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nirudie kuipongeza sana Serikali, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameifanya. Kwenye jimbo langu tumepata fedha nyingi sana; tuna ujenzi wa shule ya wasichana ya bilioni 4.5 ambayo imekwishakamilika na inadahili watoto, haya ni mafanikio makubwa sana. Tulipata pia 1.9 *billion* ya kujenga na kukarabati Hospitali ya Wilaya; ilikwishakamilika na inafanya kazi vizuri. Haya ni mafanikio makubwa; na kwa kupitia hili ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana daktari, tunakushuru. Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, atafuatiwa na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda na Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo ajiandae.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii. Kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ndiye muweza wa kila jambo. Nitumie fursa hii kwa dhati ya moyo wangu kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kazi kubwa walizozifanya katika kipindi hiki chote cha uongozi wao. Mengi yametajwa. Mambo makubwa yamefanyika; yote hayo ni mafanikio ya Serikali yetu ya Awamu ya Sita na Awamu ya Nane ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upekee kabisa ninatoa pongezi za dhati sana kwa Serikali yetu katika Sekta ya Muungano. Tunaona na tunaelewa wote kwamba Muungano ni miongoni mwa tunu kuu za nchi yetu ambayo ni urithi kutoka kwa Baba yetu wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Samia Suluhu Hassan na timu yake ya Serikali pamoja na Mawaziri wote waliokuwa katika Sekta ya Muungano wameweza kuimarisha na kuudumisha Muungano kwa namna ya kipekee katika kipindi hiki. Wakati wanaingia madarakani kulikuwa na hoja 18 za Muungano ambazo zilikuwa hazikufanyiwa kazi, lakini ndani ya kipindi kimoja cha mwaka 2021/2022 hoja 11 za Muungano ambazo zilikuwa ni kero ziliweza kufanyiwa kazi ndani ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi tunazungumza mwaka jana 2024 katika hizo hoja 18, hoja 15 tayari zimepatiwa ufumbuzi. Hili ni jambo la kujivunia kwa sababu Muungano wetu ndio umoja wetu na ndiyo amani yetu. Hayo mengine yote yanayofanyika yanayoleta maendeleo katika Taifa letu bila umoja na amani vilivyopo tusingeweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze kwa dhati ya moyo wangu namna ambavyo Serikali imeweza kuimarisha Muungano kwa namna hii. Hizo hoja tatu ambazo zimebaki nina imani kubwa sana kwa Mheshimiwa Rais kwa sababu ya uzoefu wake mkubwa alionao katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha miaka 10 na vilevile akiwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais Tanzania kwa muda wa miaka mitano na pia Makamu wa Rais na sasa ni Rais, ninaamini kabisa kwamba tukimwongezea miaka mitano yeye na Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Muungano wetu utakuwa imara kuliko tunavyofikiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, leo sitozungumzia kuhusu udhalilishaji wa watoto wala suala la madawa ya kulevya. Nimepata wasemaji wengi kuanzia Bunge la Kumi na Moja hadi sasa wakiwemo askari wamepaza sauti zao, kazi inafanyika, lakini bado changamoto ipo. Ninaomba Serikali iendelee kufuatilia, hasa suala la madawa ya kulevya. Ninashauri sana Serikali tukazane na wale ambao wanaleta na kuuza na siyo watumiaji wa chini kabisa. Huo ni ushauri wangu kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo kubwa la ushauri wangu kwa Serikali nitaanza kwenye suala la kujitegemea, dhana ambayo imetoka kwa mwasisi wetu wa Taifa letu. Dhana ya kujitegemea haitakiwi kwenda kwenye Serikali peke yake, inaanza na wazazi na walezi. Tunapowapa watoto elimu, tunapokuwa tayari kupoteza gharama kubwa kuwasomesha watoto wetu mpaka vyuo vikuu tusitegemee kwamba wale ndio watakaoleta utajiri katika familia zetu. Dhana hiyo tuiondoe katika vichwa vya Watanzania. Elimu ndio ufunguo wa maisha, elimu ni kuondoa ujinga na elimu ndiyo itakayotuwezesha kufanya kazi ya kuweza kujiletea maendeleo katika Taifa letu, lakini si kigezo pekee cha kuleta utajiri katika familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili tuweze kwenda na maendeleo ya sasa ni lazima dhana hii ya kujitegemea iwe katika vichwa vya Watanzania. Kwa upande wa Serikali ninaomba nishauri na ninaomba nirudi kwenye maeneo mengi ambayo watu wameshauri, ambayo pia ni urithi wa mababu na mababu zetu; kilimo, ufugaji na uvuvi inaimbwa kila siku ni mali ambayo tunayo na itaendelea kuwepo Tanzania haitokwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuweka mazingira wezeshi vijana wetu hawatokithamini kilimo, hawatouthamini ufugaji wala hawatouthamini uvuvi. Kwa hiyo Serikali tuna wajibu wa kuweka mazingira rafiki. Kwanza Wizara ya Ardhi; nipo mwenyewe kule Makamu Mwenyekiti, ninawashukuru sana kwa kazi inayoendelea kufanyika, lakini lazima tuweke mazingira na maeneo maalum kwa ajili ya wafugaji pamoja na wakulima; kila mmoja ajue yuko katika eneo gani ili migogoro iondoke. Migogoro itakapoondoka tutaweza kufika mahali ambapo tunataka kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo ni ushauri wangu kwa Serikali; tuna vijana wengi wako maeneo ya nje ya miji; wengine wamesoma na wengine hawakusoma sana. Bila kuwapa mazingira rafiki ya kuwatafutia masoko kwa mali zinazopatikana katika eneo husika kwa kuwawekea viwanda vya kuchakata mali au malighafi za mazao ya kilimo, ufugaji na uvuvi hatutoweza kuwashawishi vijana wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunaweza kutengeneza miradi mikubwa katika nchi yetu ya mabilioni tunashindwaje kuwezesha maeneo yanayoweza kufikika kwa kutengeneza viwanda vya kutengeneza *juice*? Tuna matunda mengi katika nchi yetu, tuna samaki wa aina nyingi katika maziwa na bahari zetu, au bahari yetu na mito mingine. Tunashindwaje kuwa na viwanda? Tunaagizia samaki wa makopo wanauzwa *shoppers* au madukani mengine, tunashindwa sisi wenyewe kuwanavyo. Kwa hiyo ninaomba sana Serikali, hata kama sisi wenyewe kama Serikali tutaona kuwa bado hali ngumu tutafute wawekezaji ili waweze kuja kufanya kazi hiyo; tuwawekee mazingira rafiki, tusiwawekee mlolongo wa mambo mengi na masharti ambayo yatawashinda waende nchi za jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mifugo mingi sana ambayo inatakiwa nje ya nchi, lakini tukiwa na masharti magumu ambayo hayana tija kwa Taifa letu wananchi wetu watashindwa kufanya kazi ya ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo eneo hilo tu, eneo la madini, Sekta ya Madini, ni sekta kubwa; na hii sekta tukiweza kuifuatilia tunasafirisha madini yetu ya dhahabu yanakwenda nchi nyingine. Kule wanachakata wanarudisha Tanzania tunakuja kuvaa wanawake ili turembeke, Hilo ni jambo ambalo Serikali yetu inapaswa kulitafakari. Kama sisi hatuwezi tumtafute mwekezaji kutoka Dubai aje hapa afungue kiwanda atengeneze malighafi ili tuweze kupata kutumia nchini kwetu, huo ni ushauri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, mpaka sasa hivi ninaamini kabisa kwamba tukiwa na dhamira njema ya kutaka kuisaidia nchi yetu ni lazima turudi kwenye kilimo, ufugaji na uvuvi. Taifa letu lina eneo kubwa sana kuliko nchi zote za Afrika Mashariki, Taifa letu lina eneo lenye rutuba, lina wanyama wa kutosha ukiacha mbali na Sekta ya Utalii ambayo ni hazina kubwa ambayo tumeachiwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, ninaiomba sana Serikali iweze kufikiria zaidi njia mbadala ya dhana ya

kujitegemea ili vijana wetu waondokane na changamoto ya ajira. Hakuna hata Serikali moja duniani inayoweza kuwasomesha watoto wake wote na kuwapa kazi za Serikali. Hiyo tusijidanganye na haitowezekana, kwa sababu nafasi za Serikali ni chache kuliko wananchi wanaotegemea kupata ajira. Bila ya kurudi kwenye dhana ya kujitegemea ya Baba wa Taifa hatuwezi kuondoa changamoto ya ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Ninawaombea kila la kheri Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Ninawaomba Watanzania tuendelee kuwaunga mkono ili mwaka huu warudi tena kwa ajili ya kuendeleza mazuri waliyoyafanya na kuendelea ushauri wetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Najma Murtaza Giga. Ninamwita sasa Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Butondo na Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka ajiandae.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ninaungana na wenzangu kwa kukupongeza kuendelea kufanya kazi hiyo ya kuongoza Bunge letu kwa weledi na Mungu aendelee kukuangazia katika kila hatua zako na uchaguliwe kwa nyingi tena na wananchi wa jimbo lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza mchango wangu ningependa kuitumia nafasi hii kama Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kutoa pole kwa Waziri wa Nishati na Serikali kwa ujumla kwa kumpoteza mwanamapinduzi na mfanyakazi hodari ambaye alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* kufuatia ajali ya gari iliyotokea. Mungu aweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia nafasi hiyo ninampongeza Mheshimiwa Spika wetu kwa busara zake. Ametuelekeza na

Mwenyekiti wetu sasa yuko njiani kwenda kushiriki mazishi ya kiongozi huyo kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na kwa niaba ya Bunge zima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii nyeti, ambayo ni Ofisi ya Waziri Mkuu inayokusanya taasisi nyingi na muhimu katika utendaji kazi na ambayo ndiyo Wizara inayosimamia kazi za Mawaziri wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kabla ya kuanza nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kusimamia vizuri uongozi wa nchi yetu na kumfanya Waziri Mkuu wake kuendelea kusimamia kazi za Serikali na za Mawaziri wote na kuweza kuleta tija kubwa sana katika maendeleo ya Watanzania. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ningependa nitumie nafasi hii pia kumpongeza Waziri Mkuu mwenyewe na Naibu Waziri Mkuu kama msaidizi wake wa karibu kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya; na sisi Wabunge tumekuwa ni mashahidi wa viongozi hawa kuwa viongozi wa mfano kwa tabia njema na kuwa mfano wa kuigwa katika kazi yao ya uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaanza shughuli za Bunge niliji-*address* kama Mbunge ninayepiga vita sana riba kubwa katika mabenki na suala la mikopo ya kausha damu. Nilisema maneno haya kila eneo nilipokwenda na hapa Bungeni nilizungumza kwa kiasi kikubwa. Ningependa kuitumia nafasi ya leo kuishukuru Serikali; sauti yangu niliyopaza kwa kiasi wameisikiliza na hatua kadhaa zimechukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninazungumza riba za mabenki zilikuwa kati ya 16% mpaka 23%, leo riba za mabenki ziko kati ya 14% mpaka asilimia 21%. Kuna kiasi cha mafanikio ambayo tumeyapata katika kupaza sauti. Hata hivyo, leo ninasimama kuiomba tena Serikali kwamba bado na ninaiomba Serikali wakati na Serikali yenyewe mara nyingi ninaisikia ikilalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewahi kumsikia Mheshimiwa Waziri Bashe, Waziri wa Kilimo akisisitiza kuzitaka benki ziwakopeshe wakulima kwa *single digit,* maana yake kuanzia asilimia tisa kushuka chini. Nimepata kuwasikia viongozi mbalimbali wa Serikali wakizungumzia jinsi wanavyoona riba za benki zilivyo na athari kwa maendeleo ya wafanyabiashara na wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninataka sisitize tena kwamba bado Serikali ina kazi ya kujielekeza katika kuhakikisha kuwa riba za benki zinashuka. Katika jambo hili sijui mgogoro unatoka wapi? Kila ukiuliza unaambiwa kuwa hatutaki ku-*disturb* uchumi, tumewaacha benki ziwe huria. Sidhani kama hoja hii inakubalika. Uhuria huu unatoka wapi? Kwenye maji, kwenye umeme, kwenye nishati nyingine tumeweka *EWURA* kuwa *regulatory authority* ya kusimamia bei za mafuta, kwani kwenye mafuta hakuna wafanyabiashara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona wafanyabiashara wa mafuta tunawapangia bei na wana-*survive?* Kwa nini benki tusizipangie riba zika-*survive?* Kwenye insurance tumeweka *TIRA (Tanzania Insurance Regulatory Authority)* ili kuhakikisha kwamba viwango vya bima vinasimamiwa, kwamba mtu asijipangie mwenyewe viwango vya bima; mbona hakuna kampuni za bima zinazotetereka? Kwa nini benki hatutaki kuziwekea mwongozo maalum wa riba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo ambapo Benki Kuu haitaki kutoa mwongozo wa riba inatoa mwongozo wa miamala. Imeweka viwango maalum vya kulipa kama ada ya miamala; sasa, inashindwa nini kuweka viwango maalum vya kulipa kama riba? Jambo hili limeathiri sana uchumi wa Watanzania, wafanyabiashara wengi wameumia na wengine wametoka katika mkondo wa biashara. Huku Serikalini wanachelewa kulipwa madai yao, huku benki zinaendelea kuwahesabia riba kubwa. Kwa hiyo, ninasimama tena kupaza sauti kuitaka Serikali ifike mahali iamue na kuhakikisha kwamba kwenye suala la riba inaipa nguvu Benki Kuu ili iwe na viwango elekezi vya riba kwa benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni hili la hizi *microfinances* ambalo nimekuwa nikilizungumzia. Ninataka niipongeze sana Serikali na *BOT* kwa sababu wamefunga *microfinances* nyingi ambazo zilionekana kwa kweli zimekuwa mzigo mkubwa kwa Watanzania hata hivyo kazi bado. Nitatoa mfano, *microfinance* inakwenda kukopa kwenye benki mkopo ambao riba yake ni 14%, 15%, 16%, 17% na 18%, lakini riba hii inahesabiwa kwa mwaka. Wao wanamkopesha mfanyabiashara mdogo kwa riba ya 10% hadi 20% kwa mwezi. Kwa maana nyingine ni kwamba ukii-*calculate* kwa mwaka ni kama hawa wafanyabiashara wadogo wanaenda kutozwa riba ya 240% hadi 120% huu ni mzigo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado ninaitaka Serikali ihakikishe kwamba inaipatia nguvu kubwa *BOT* ili iendelee kusimamia hizi *microfinances* nazo ziwekewe viwango vya riba ambavyo ni himilivu kwa wafanyabiashara hawa wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ninaomba nimalizie ni suala la leseni za madereva wa bodaboda. Tumesema hapa, tunaishukuru Serikali, tulizungumza tukaieleza kwamba haiwezekani malipo ya faini ya makosa ya barabarani ya gari na pikipiki yawe sawasawa. Serikali hii sikivu ya Mama Samia Suluhu Hassan, ikateremsha kutoka shilingi 30,000 ikaleta shilingi 10,000 kwa makosa ya pikipiki ya barabarani, ninashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado pia tuna tatizo la leseni na nilisema hapa kwenye Bunge hili kwamba, mpaka leo hatuna leseni za waendesha pikipiki. *Driving license* ni kwa ajili ya magari lakini tunatakiwa tuwe na *riding license* kwa ajili ya waendesha pikipiki na hii iwe shilingi 20,000. Sasa hivi inakadiriwa tuna bodaboda 2,000,000 zinazofanya kazi, lakini kati ya hawa bodaboda 2,000,000 ni kama 15% ya waendeshaji wa bodaboda ndio wana leseni. Wengine 85% hawana leseni kwa sababu imekuwa ni mzigo kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali ishushe hizi leseni za bodaboda kutoka hiyo shilingi 70,000 hadi shilingi 20,000. Hawa 85% wakilipa ambao ni kama madereva bodaboda 1,700,000 tunaweza tukaingiza shilingi bilioni 34 za Kitanzania kwenye Mfuko wa Hazina ya Serikali. Tusing'ang'anie kiwango kikubwa ambacho hakikusanywi, tunaacha kuweka kiwango kidogo ambacho tutakusanya kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaendelea kuipongeza sana Serikali na ninaunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda. Ninamwita sasa Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka na Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, ajiandae.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili kutoa mchango wangu katika Ofisi ya Waziri Mkuu, ambayo kimsingi inabeba mambo makubwa. Kama tunavyofahamu Ofisi ya Waziri Mkuu kimsingi ndiyo ofisi inayoshughulikia masuala ya kila siku ama majukumu ya Serikali kama majukumu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kwanza kwa kumpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo anavyoiendesha vizuri na hasa katika mafanikio ya kimaendeleo nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sote kwa pamoja tunakiri kwamba, mabadiliko yapo makubwa ya kimaendeleo na hasa katika eneo la miradi yetu ya kimikakati ambayo inakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunaona *SGR* maendeleo yake ni mazuri na sasa imeanza kutoa huduma na bahati nzuri miradi katika maeneo ambayo kuna mikataba zaidi ya tisa inaendelea kutekelezwa katika nchi hii. Bahati nzuri si miradi hiyo tu, kwa pamoja na miradi mingine Mradi wa *REA* na ujenzi wa

Daraja la Busisi. Hii ni moja kati ya miradi mikubwa ambayo inaendelea katika nchi yetu. Vilevile, Bwawa la Mwalimu Nyerere sote ni mashahidi kwamba lipo katika hatua ya mwisho kabisa na bahati nzuri sasa tunapata huduma ya umeme ambayo ilikuwa ni adha na kero kwa wananchi katika ubora unaotakiwa, kukatika umeme na mambo mengine hakupo tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi pia hii ya *REA* imekwenda vizuri, nchi nzima sasa inawaka na jitihada kubwa inaendelea kuhakikisha kwamba Serikali yetu inaanza kusambaza umeme katika ngazi ya vitongoji, ilimradi wananchi waendelee kupata hii huduma ya umeme ambayo ni muhimu sana katika kuchachusha maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna ambavyo kwa kweli amekuwa akifanya kazi kubwa ya kuhakikisha anaisimamia Serikali vizuri na hasa shughuli za kila siku za Serikali. Tumeshuhudia ziara zake katika mikoa mbalimbali, lakini ufuatiliaji wa utekelezaji wa ilani, anafanya kazi kubwa sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Haya yote kwa kweli tunasema Mwenyezi Mungu aendelee kumpatia afya njema ilimradi mambo yaende kufanyika vizuri katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Lukuvi na Mheshimiwa Ridhiwani pamoja na Manaibu Mawaziri wao wote kwa namna ambavyo wanamsaidia sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Rais wa Jamhuri ya Muungano katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nianze mchango wangu hasa katika eneo la vita dhidi ya madawa ya kulevya. Tunaye Kamishna Jenerali Lyimo ambaye kwa kweli ninaomba nitumie fursa hii kwanza kumpongeza kwa namna ya moyo wa uzalendo mkubwa anaouonesha kwa Taifa letu na Watanzania kwa ujumla. Kamishna Jenerali Lyimo ni Kamishna ambaye ambaye kwa kweli anatekeleza majukumu yake kabisa kwa usahihi chini ya Waziri Lukuvi; tunaona namna ambavyo anatoa ushirikiano mkubwa

lakini tunaona matokeo chanya katika eneo hili la kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya ikiwemo suala zima la kuingiza madawa ya kulevya katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote ni mashahidi kwamba, tumeshuhudia kilo nyingi za dawa zikikamatwa katika hii Nchi yetu ya Tanzania hasa katika viwanja vyetu vya ndege na mipaka ya nchi yetu, jitihada ambazo zinafanyika ni kubwa sana. Tunaona jitihada kubwa inayofanyika katika uteketezaji wa mashamba makubwa ya bangi unaofanyika katika nchi yetu hii. Bahati nzuri katika kila hatua anayokuwa anaifanya amekuwa wazi kabisa na kwamba amekuwa akionesha Watanzania namna gani jitihada hizi zinafanyika pamoja na kuonesha rekodi zote na namna ambavyo Serikali inafanya jitihada kubwa kuhakikisha kwamba mtandao huu wa dawa za kulevya unashughulikiwa kwa karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiona shughuli nzima ya urekebu ikiwa inafanyika katika nchi hii. Pamoja na kwamba tumekuwa na waathirika kadhaa wa dawa za kulevya, chini ya Jenerali Lyimo upo usimamizi wa karibu sana kuona kwamba hawa waathirika wa dawa hizi wanapata huduma ipasavyo katika maeneo mbalimbali. Hii tumekuwa tukiona katika Jiji letu la Arusha, Dar es Salaam na hata hapa Dodoma. Jitihada ni kubwa kuhakikisha kwamba urekebu unafanyika kwa karibu sana, ili kuona kwamba jamii hii iliyokuwa imeangamia na dawa za kulevya inarejea na kuanza kuungana na wanajamii wengine kutekeleza majukumu ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa sababu tumekuwa tukitenga fedha katika eneo hili ili kuona kwamba wananchi hawa wanarudishwa katika hali yao ya kawaida, lakini wakati huohuo wakiwa katika urejeshwaji wa hali ya kawaida. Pia, zimekuwa zikitengwa fedha kwa ajili ya kuhakikisha tunawawezesha walau waweze kufanya majukumu yao wale walio na fani mbalimbali katika maeneo hayo ambayo urekebu umekuwa ukifanyika. Jitihada hizi kubwa zinazofanyika hatuna budi kwa kweli kumpongeza sana Jenerali Lyimo na Wizara

kiujumla kwa namna ambavyo imekuwa ikiratibu mambo haya, na shughuli hizi zimekwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu nitoe mfano mdogo sana. Tumeweza kwa ujumla kukamata kilogramu milioni 4.3, ambazo zimekamatwa katika kipindi cha miaka miwili tu (2023 na 2024). Hii ni zaidi ya mara sita ya kiasi hicho kilichokamatwa katika mwaka 2021 na mwaka 2022. Unaweza ukaona ni jitihada kubwa ambazo kwa kweli idara hii imekuwa ikifanya kazi kubwa sana ya kuvunja mtandao mkubwa ambao umekuwa ukiingiza haya dawa ya kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada zinafanyika hapa kubwa sana. Tumeshuhudia mapapa na wafanyabiashara nguli wakubwa wakikamatwa badala ya kukamata vidagaa. Hii ni jitihada kubwa ambayo ni lazima tumpongeze Jenerali Lyimo kwa sababu anafanya kazi ya kiuzalendo kabisa. Tumeshuhudia jitihada hizi kubwa zikifanyika na sisi tunashukuru. Kama Kamati kwa kweli hili tuliliona na tunamtakia kila la kheri aendelee kufanya kazi kubwa kwa ajili ya kuwaokoa Watanzania ambao wamekuwa wakiathirika pakubwa sana na dawa za kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, operesheni kubwa hizi zimekuwa zikifanyika maeneo mbalimbali hata katika maeneo yetu ya mashamba ya bangi hasa kule Mara zaidi ya ekari 4,733 zimeteketezwa, hii ni hatua kubwa sana. Haya maeneo makubwa hasa ni huko Mkoa wa Mara pamoja na kule Morogoro. Hivi tumekuwa tukiyashuhudia mambo haya *live* kabisa katika vyombo mbalimbali vya habari. Hizi ni jitihada kubwa ambazo zimekuwa zikifanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala kubwa vilevile ambalo limekuwa likifanyika pakubwa sana la kuhakikisha jitihada zinatolewa hasa katika maeneo maalum ya mipakani na *airport*. Hizi ni jitihada kubwa ambazo zimekuwa zikifanyika na ndiyo maana sisi kama Kamati tumekubaliana kwamba ni lazima waongezewe fedha na zitolewe kwa wakati, ilimradi waweze kupata vifaa vya kisasa na hasa maeneo yale ya mipakani,

waweze kufanya kazi vizuri. Kwa sababu kama hawana vifaa vya kuchunguza, kupembua na kuona wale watu wanaovuka na wanaoingia kwamba, wanatoka na nini na wanaingia na nini? Hatuwezi tukafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii pamoja na kuongeza bajeti yao ambayo imeenda takribani mara mbili katika upande wa maendeleo na *OC*, itakwenda kusaidia sana wafanyakazi waongeze ari na wafanye kazi ya doria vizuri, ilimradi kazi hii iendelee kufanyika sawasawa. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa ajili ya usalama wa nchi yetu, tunaomba sana Idara hii itazamwe kwa macho mawili, ili operesheni na kazi kubwa inayoweza kufanyika iende kukamilishwa inavyopaswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nielekee eneo la miradi ya kimaendeleo ambayo imefanyika katika Jimbo la Kishapu. Ninashukuru sana Serikali yetu imetoa fedha nyingi sana Sekta ya Elimu, Afya, Miundombinu, Barabara na Maji, ni hatua kubwa sana iliyofanyika. Nitoe mfano tu, Wilaya ya Kishapu wakati ninaingia kuwa Mbunge mwaka 2020 ni kata nne peke yake zilikuwa zimepata maji safi na salama, lakini hivi ninavyozungumza kata 21 zinapata maji safi na salama. Hii ni kutokana na vyanzo mbalimbali, maji ya Ziwa Victoria kata 17, pia kata karibu sita zinapata maji kutokana na vyanzo vingine vya visima virefu na mito tuliyonayo. Hii ni jitihada kubwa sana ya Serikali na hasa ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Aweso kwa namna ambavyo ananipatia ushirikiano katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo machache ambayo yapo katika Tarafa ya Mondo yanahitaji maji na sehemu kame ni kubwa sana. Kata ya Mondo, Sekebugolo, Busangwa na Mwasubi, hizi ni kata ambazo zinahitaji huduma ya haraka ya maji na ninafurahi kwa sababu kuna bomba kubwa linalotoka Mwanza na kupita katika Wilaya ya Kishapu ambalo litagusa Tarafa hii ya Mondo. Nina hakika kwamba sasa kata hizi zitakwenda kupata huduma ya maji haraka iwezekanavyo. Ninaiomba Serikali wakati wa zoezi hilo ikumbuke kuweka matoleo

kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kata hizo zinapata huduma kwa sababu zipo ndani ya kilometa 12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali kwa sababu barabara sasa katika Wilaya ya Kishapu zimeshafunguliwa vizuri, kata zote zinapitika. Yapo maeneo machache sana ambayo yamebaki yana changamoto, lakini tumepata fedha zaidi, kila mwaka tumekuwa tukipata shilingi bilioni 2.5. Ukilinganisha na kipindi cha nyuma, tulikuwa tukipata shilingi milioni 900 mpaka 950. Hizi ni jitihada kubwa sana za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niwaambie Watanzania na hasa wananchi wa Jimbo la Kishapu, Mama Samia tunaye na tunatamba naye. Ninaomba sana Watanzania tubaki na imani na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan. Huyu mama atatuvusha, kwa sababu kazi anayofanya ni kubwa na ninaomba Watanzania miaka mitano inayokuja tumpe nafasi tena Rais wetu aendelee kupeperusha bendera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Butondo. Tunaendelea na Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka. Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi asubuhi hii ya leo niweze kutoa mchango wangu kwenye hii Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hii hotuba nzuri. Siyo hotuba peke yake na kazi kuwa anayoifanya kwa Taifa hili. Kwa nafasi yake kama Waziri Mkuu tunayo kila sababu ya kumpongeza na kumshukuru kwa namna anavyolitendea wema Taifa hili kwa nafasi yake kama Waziri Mkuu. Ninasema hili si kwa sababu tu ni

Waziri ambaye ametoka Mkoa wa Lindi, lakini nyote humu ndani ni mashahidi kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kweli anafanya kazi inayotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba hii ninaomba nianze na Wizara ya Ujenzi. Kwenye Wizara ya Ujenzi ninaomba nianze na sera ya kuunganisha mikoa kwa barabara *either* ziwe za lami au changarawe. Huko nyuma nilishawahi kusema kama sera hii imekuwa ngumu kutekelezeka basi ni bora tuiondoe kwenye makaratasi kwa sababu mpaka leo hii Mkoa wa Lindi bado haujaunganishwa na Mkoa wa Morogoro. Hapa ninapotaka kuongea mwelewe kwamba Barabara ya Morogoro ninayoizungumza kwa kweli kama ingechukuliwa hatua ingekuwa ni barabara ya ukombozi kwa hali kama hii tuliyonayo leo Barabara yetu ya Kibiti – Lindi inavyoendelea kutusumbua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Watu wa Lindi na Mtwara wanaambiwa watoke Lindi, Songea, Njombe, Iringa, Morogoro, Pwani ndio wafike Dar es Salaam au waende Dodoma. Barabara ile ya Morogoro – Lindi ingetengenezwa ina maana mtu wa Lindi na Mtwara angepita Morogoro – Pwani yupo Dar es Salaam, ina maana inaingia mikoa miwili tu. Barabara hii kwanza siyo tu inapunguza gharama kwa watumiaji, lakini hata kwa Serikali kutumia mafuta kutoka Lindi – Songea – Njombe – Iringa – Morogoro – Pwani mpaka Dar es Salaam au Dodoma gharama ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuliko tungetoka tu Lindi unakuja Morogoro unakuja hapa Dumila upo Dodoma. Kwa hiyo, Wizara waone umuhimu wa *back up* ya hii barabara badala ya kutumia hiyo barabara ndefu ambayo kila siku tunaizungumza. Ninapoisema hii Barabara ya Morogoro sina maana kwamba nimeridhika sana na kile kizungumkuti cha ile Barabara yetu ya Nangurukuru – Liwale na Nachingwea – Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa napo ninaomba niipongeze Serikali kwa kuonesha nia angalau tupate hizo kilometa 10 za Barabara yetu ya Nangurukuru – Liwale na kilometa 50 ile ya

Nachingwea. Kwa hiyo, kwa jambo hilo ninapendelea kuipongeza sana Serikali na iwe hivyo. Vilevile, Barabara ya Mogororo ni barabara muhimu sana kama umuhimu huo niliouonesha hapo nilivyoizungumzia hiyo barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niende upande wa *TARURA*. Kwa kweli katika taasisi tano au 10 katika nchi yetu ni *TARURA*. Shida kubwa ya taasisi hii ya *TARURA* ni upelekeji wa fedha. Mimi kama nipo sawasawa zipo fedha ambazo zimetengwa Kizungu wanaita *ring fenced,* lakini hizo fedha nazo mbona haziendi huko *TARURA?* Kwa sababu miradi mingi ya *TARURA* imekwama kwa sababu ya fedha. Leo hii *TARURA* wanadaiwa kila kona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi wa Liwale nilijaribu kumwuliza Mtendaji Mkuu wa *TARURA* na watumishi wengine; hivi ni wilaya gani ambayo ina barabara chache sana za lami kwenye nchi hii? Ndugu zangu, Liwale kama siyo ya kwanza basi ni ya pili kwa uchache wa barabara za lami, maana sisi tuna kilometa tatu tu za lami pale mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali ilione hili. Tunaposema walione hili, wawapelekee fedha *TARURA* waweze kutekeleza yale ambayo wameahidi. Niseme tu ukweli, Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Liwale ni mtu msikivu, mwaminifu, na mchapakazi sana. Kila mipango tunayopanga, tunapanga naye, lakini tatizo linakuja kwenye fedha, hana fedha za kutosha. Kwa hiyo, ninaomba Serikali walione hili watuongezee fedha, *TARURA* wapate fedha ili waweze kutukwamua sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa hizo barabara ni mkubwa sana. Hizi barabara ndizo zinazotoa mazao haya ya wakulima kupeleka sokoni. Maana tukizungumzia Barabara za *TARURA* mnaweza mkazipuuza, mkaziona tu ni barabara ambazo zina umuhimu mdogo; hapana. Hizi barabara ndizo zinazotoa mazao ya wakulima kutoka mashambani kupeleka sokoni. Sasa, kama hizi barabara haziko sawa sawa, maana yake mazao ya wakulima yatakuwa hayawezi kufika sokoni na mazao ya

wakulima yasipofika sokoni maana yake uchumi wa wakulima hawa utakwenda kuharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo ninaomba nijihamishe niende kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii. 60% ya ardhi ya Liwale inazungukwa na Hifadhi ya Selous pamoja na Hifadhi ya Mwalimu Nyerere. Suala la wanyamapori limekuwa ni kitendawili kisichopata majibu. Juzi nilizungumza hapa kwamba tumeshapotea zaidi ya watu wanne ndani ya mwezi mmoja. Kuanzia tarehe 20 mwezi uliopita mpaka tarehe 11 mwezi huu tumeshapoteza watu wanne ambao wamepoteza maisha kwa ajili ya kadhia ya wanyama (tembo).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuatilia, nimejaribu kuzungumza na Wahifadhi, wanasema hawa tembo mahali walikozalia wanaona kama ndiyo nyumbani. Sasa, ninaomba nitoe taarifa kwamba tembo sasa wanazalia kwenye mashamba yetu. Sasa, sijui tuseme ndiyo wamehamia! Maana wanasema kwamba hawa wanyama wanapozalia ndiyo wanaona kama nyumbani. Sasa, tembo wa Liwale wanazalia kwenye mashamba yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ninaomba ndugu zangu wa Hifadhi, hebu jaribuni kuongeza juhudi. Mnawahamishaje hawa tembo hapa walikozalia? Kwa sababu mnasema hapa walikozalia hawa tembo wamefanya kama nyumbani kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa ambalo ninaliona pale, pamoja na kwamba juhudi kubwa za Serikali zinafanywa kusogeza tembo hawa Hifadhini, lakini wako watumishi wa *TAWA* na *TANAPA* siyo waaminifu. Wanaruhusu mifugo kupita kwenye hifadhi zetu. Liwale ni miongoni mwa maeneo ambayo tunapokea wafugaji, lakini inawezekanaje leo mifugo itoke Iringa, itoke Mbeya, itoke Morogoro, ifike Liwale kwa njia ya miguu? Maana yake wanapita Hifadhini. Wanawezaje kupita Hifadhini bila kuonekana na hawa askari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini? Kwamba, sasa tembo wanaondoka hifadhini wanakimbia hawa mifugo,

matokeo yake wanakuja kutubughudhi sisi. Ninaoimba Serikali idhibiti sana hawa watumishi ambao siyo waaminifu, ambao wanapitisha ng'ombe kwenye Hifadhi, matokeo yake ng'ombe wanakuja kutudhuru sisi kule kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni vitendeakazi. Vitendeakazi ni vichache mno. Sisi Liwale 60% kama nilivyosema, tunahitaji kuwa na askari wengi. Kwa sababu leo unapata ripoti tembo wametokea Ngongowele, askari wanakwenda, kesho wametokea Ndapata, askari wanatakiwa waende. Hao askari wenyewe ni wachache. Unakwenda pale hifadhini wanakwambia gari imeondoka imekwenda kijiji fulani au hatuna gari au mafuta hatuna. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali kuongeza vifaa vya kutendea kazi kuhakikisha kuwadhibiti hawa wanyama (tembo).

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kwenye hili ni kuhusu kifuta machozi. Wilaya ya Liwale mara ya mwisho kupata kifuta machozi ni mwaka 2022. Kwa hiyo, kuanzia mwaka 2022, mwaka 2023, mwaka 2024 na leo mwaka 2025, wananchi wale waliopata madhara ya tembo bado hawajapata kitu kinachoitwa kifuta machozi. Japokuwa kifuta machozi chenyewe bado nacho ni kidogo, lakini bado tunadai kifuta machozi, bado hakijawafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nishati *(TANESCO)*. Sisi kule kwetu zamani ilikuwa umeme ukiwaka watu wanashangilia au wanashtuka. Sasa hivi kule kwetu sisi umeme ukiwaka ndiyo watu wanashangaa, kwa sababu mara nyingi tunakuwa gizani. Kwa hiyo, ninaendelea kuwaomba na nilishawahi kuongea hapa kwamba, shida kubwa ambayo tunaipata umeme kutoka Mahumbika mpaka Liwale, umbali ule ni mrefu. Tunaomba mtuongezee kituo cha kupoozea umeme pale Liwale au hata Nachingwea, ili tuweze kupata umeme huu kwa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulienda Mtwara wakatuambia kwamba kuna mashine imepelekwa kutoka Ubungo kwenda Mtwara megawati 20 na mahitaji ya Mkoa wa Lindi na Mtwara ni

Megawati 18. Bado mashine ile pamoja na kwamba imefungwa, bado upatikanaji wa umeme kwa Mkoa wa Lindi na Mtwara bado ni kitendawili. Tunaomba sana Serikali muone namna ya kutuwezesha sisi watu wa Mkoa wa Lindi kutuingiza kwenye Gridi ya Taifa, ili sisi wote tufaidi keki ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, ninaunga mkono hoja na ninakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zuberi. Tunaendelea na Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, atafuatiwa na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga ajiandae.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza ninachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri aliyoifanya katika nchi yetu. Ninampongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo imegusa kila eneo, na ninawapongeza pia Mawaziri wake wote na Manaibu wake wote na watendaji katika Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze katika Sekta ya Kilimo. Ninamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Bashe na Naibu wake Mheshimiwa Silinde. Kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Bashe kwa kukubali taarifa ya ukusanyaji upya wa *data* za wakulima katika Mikoa ya Kusini, lakini pia ninampongeza kwa ugawaji wa pembejeo. Kwa sasa hivi zimeanza kuingia katika Wilaya ya Masasi, hivyo zimefika wakati muafaka na tumeenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamkumbusha pia, Mheshimiwa Bashe katika Kilimo cha Korosho, mauzo yanapoanza Jimbo la Lulindi huwa ni la kwanza kupeleka mazao katika ghala, lakini malipo yanachelewa. Inafika mpaka mwezi Januari wengine hawajalipwa, wanashindwa kupeleka watoto shule wakisubiri ada. Ninaomba malipo ya korosho katika Jimbo la Lulindi yalipwe

mapema sambamba na upelekaji wa zao hilo katika ghala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nizungumzie kwenye Sekta ya Maji; ninachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Aweso na Naibu wake Mheshimiwa Kundo, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Sekta nzima ya Maji. Kuna changamoto chache ambazo ninapenda kuzielezea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, katika chanzo cha maji Lupaso; chanzo kile kimekufa katika Kata ya Lupaso ndani ya Jimbo la Lulindi. Maji yanatoka mara moja tu, yalitoka mwaka mmoja tu hayajatoka mpaka sasa hivi. Tunaomba chanzo kile kirekebishwe ili wananchi wa maeneo yale waweze kunywa maji safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia,chanzo cha maji kutoka Mto Ruvuma. Mradi huu unasuasua; maji yanatoka kwa mwezi mara moja na yanatoka kipindi cha kiangazi. Hiyo ni kero kubwa inayowagusa wananchi wa Vijiji vya Mapili, Chikoropora, Mkalivata, Chipingo, na Mnyonyo, ndani ya Jimbo la Lulindi. Ninaomba mradi huo utengenezwe vizuri, wananchi wa maeneo hayo waweze kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maji hayo ninapenda kuzungumzia maji kutoka kwenye chanzo cha Kijiji cha Njechele kinachonufaisha katika Kata ya Namwanga, Vijiji vya Namwanga, Mkoropora, Chipango, Nakalola, Nakachindu, na katika Kata ya Mijelejele ndani ya Kijiji cha Mijelejele, Nambunda, Tupendane, Mpwapwa na Toleani. Maji haya yanatoka mara moja kwa wiki. Tunaishukuru Serikali kwa kutuletea maji yao, lakini tunaomba yawekwe dawa kwa sababu maji yale yanakuja yakiwa na rangi ambayo inakatisha tamaa hata kunywa. Tunaomba maji hayo yawekwe dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie katika Sekta ya Barabara. Ninampongeza Mheshimiwa Ulega na Naibu wake Mheshimiwa *Engineer* Kasekenya kwa kazi nzuri wanayoifanya katika maeneo yote ndani ya barabara. Barabara

za Jimbo la Lulindi zinapitika japo ni za vumbi, lakini kwa mwaka huwa zinakwanguliwa mara mbili au mara tatu, hivyo zinapitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ni vivuko au madaraja. Kuna madaraja mengine yamejengwa pale kimtegomtengo tu, yaani ukifika unasimama unajiuliza nipite au nirudi? Kwa mfano Daraja la Mpindimbi – Kanyimbi – Nakalola; Daraja hilo limekaa kimtego, ukifika pale unajishauri nipite au nisipite? Tunaomba marekebisho yafanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Daraja la Nakachindu kwenda Kata ya Mkululu halipitiki. Kijiji cha Nakalola kwenda Kipango halipitiki, Kijiji cha Nakachindu kwenda Lulindi hakipitiki. Tunaomba maeneo hayo yafanyiwe marekebisho ya haraka. Tunaingia kwenye uchaguzi, tuna nafasi ya kupita kwenda kuomba kura za wananchi kwa ajili ya Mama Samia, nyumba kwa nyumba, mtaa kwa mtaa. Tunaomba watutengenezee barabara tuweze kupita kuomba kura kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie vile vile kwenye suala la Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Hapa ninampongeza Mheshimiwa Jerry na Mheshimiwa Maryprisca kwa kazi nzuri. Vijijini simu tunaziona, tunazitumia, lakini kuna maeneo ambayo yana changamoto. Kwa mfano, kwenye Kata ya Mnavira, Kata ya Lipumburu na Kata ya Sindano, ndani ya Jimbo la Lulindi; kata hizi ziko mpakani na Msumbiji. Kwa hiyo, ukitaka upate mawasiliano vizuri uchukue Mtandao wa *Movitel* kutoka Msumbiji, ambako ndiyo unaweza kupata mawasiliano vizuri, lakini ya kwetu haya hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Jerry shuka, ashuke aje Lulindi; ashuke aje aone watu wanavyoongea juu ya mikorosho, aje aone watu wanavyoongea kwenye vichuguu. Kwa hiyo, tunaomba sana yeye na Naibu wake waje Jimbo la Lulindi waangalie mawasiliano jinsi yanavyokwenda. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie Sekta ya Michezo. Kwenye Sekta ya Michezo ninampongeza Mheshimiwa Waziri Profesa Palamagamba na Naibu wake Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, alimaarufu Mwana FA. Sekta hii ninaipongeza sana. Nimeshuhudia wakienda mpaka kwenye mechi za mpira chandimu; wanaenda kuongea wakiwa wageni rasmi. Tunaomba nguvu hiyo isiishie hapa, waendelee kushuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi hiyo pia, ninaipeleka kwa Wabunge na Madiwani wote ambao wanafanya michezo katika maeneo yao. Ninafikiri Chama cha Mpira wa Michezo wa Miguu kinaona jinsi Madiwani na Wabunge wanavyofanya mashindano mbalimbali kwa gharama zao kwenye maeneo yao ili kuboresha mchezo huo. Sisi bado tuko tayari kuendelea na michezo hiyo mahali popote ilimradi tuibue na kukuza vipaji vya Mpira wa Miguu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ,ninaunga mkono hoja na ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Angelina Malembeka. Tunaendelea na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, atafuatiwa na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga na Mheshimiwa Maimuna Pathan ajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi. Ninaomba na mimi nianze kwa kuanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kupata nafasi ya kuchangia, lakini ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya na nguvu. Kipekee ninakupongeza Mheshimiwa Mwenyekiti kwa namna ambavyo unaendesha kikao chako leo. Ninaona tunakwenda kwa *speed* kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imeonyesha mafanikio makubwa ya Serikali na kimsingi ninaomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Serikali nzima kwa kazi nzuri ambayo Serikai inafanya, hasa katika maeneo mahususi ambayo nitakwenda kuyazungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imeeleza namna ambavyo kazi mbalimbali zilivyoanza wakati Mheshimiwa Rais anachukua nafasi na namna ambavyo nyingine zimekamilika na nyingine zinaendelea. Kwa kifupi kabisa nizungumzie maeneo mawili ambayo mimi mwenyewe binafsi kama Mjumbe nimeshiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kwenye eneo la bwawa la umeme; mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini. Kazi kubwa sana imefanyika. Tulikwenda kule ikiwa 27%, tumekwenda ikiwa 98%, sasa hivi ukifika eneo lile unaweza ukafikiri umefika nje ya nchi. Tunaipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo imefanyika kwenye bwawa lenyewe, lakini kwenye maeneo ya miundombinu ambayo yanasafirisha umeme. Tumekwenda kwenye Kituo cha Chalinze na maeneo mengine ambapo *line* kubwa ya umeme inajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni eneo la Daraja la Kigongo – Busisi. Mimi ni sehemu ya Wabunge tulioomba sana Daraja lile lijengwe, kwa sababu wananchi wanaotoka Mikoa ya Kigoma, Geita na Kagera walikuwa wakifika pale wakakuta magugu maji yamejaa, wakakuta boti haipo, hata kama una mgonjwa anaweza akafia mikononi mwako unamwangalia ukiwa unampeleka Bugando. Kukamilika kwa Daraja hilo nii faraja kubwa kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa, lakini kutarahisisha biashara katika maeneo mbalimbali. Tunaipongeza sana Serikali kwa miradi hii pamoja na miradi mingine mingi ikiwemo ya reli, ikiwemo ya elimu na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ninataka kumshukuru sana Mheshimiwa Rais. Katika kipindi cha takribani miaka 10 ambayo nimekaa Bungeni, nilikuwa nikiomba sana Geita Mji iweze kupata manispaa. Nilikuwa ninaomba siyo kwa upendeleo, ni kwa sababu ya takwimu za mafanikio yaliyoko pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Geita kwa maana ya Geita Manispaa, tunakusanya takribani shilingi bilioni 20 kwa mwaka na ni moja ya halmashauri ambazo sehemu kubwa ya miradi ya maendeleo tunafadhili wenyewe. Pia, ni mji ambao

tumeutengenezea *Masterplan,* tumeupanga na ni mji ambao unakua kwa kasi. Kwa hiyo, hoja yangu ya kuomba manispaa nilikuwa ninaomba nikiwa na takwimu, lakini na vigezo. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, kwa kulisimamia jambo hili na kuitangaza Geita kuwa Manispaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo dogo tu ambalo ninataka kuomba sehemu hii ni kwamba, baada ya Geita kuwa manispaa sasa tunaiomba Serikali ituongezee bajeti ya miundombinu. Kwa sababu, huwezi kuwa na manispaa ambayo ina barabara za lami chache na sehemu kubwa ni barabara za matope. Tunaomba sana Serikali kwenye eneo hilo iweze kutuangalia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo ninataka kuzungumza ni eneo la madini. Ninataka kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Madini na Serikali kwa ujumla. Kwenye takwimu inaonekana kwamba sasa madini yanachangia sehemu kubwa sana ya fedha za kigeni. Mchango huu haujaja wenyewe, umekuja kwa kazi kubwa iliyofanywa na Mawaziri na Serikali pamoja na Mawaziri waliotangulia. Kwa kweli sisi wananchi tuliotoka kwenye machimbo tunaona kabisa mchango wa Serikali kwenye kufanikisha mafanikio ya wachimbaji wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wachimbaji wadogo wadogo wanachangia zaidi ya 40% ya mauzo ya madini ambayo yanauzwa nje ya nchi. Siyo jambo dogo! Ninaipongeza Serikali kwa sababu imechukua hatua mahususi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya eneo kubwa ambalo limefanya kazi kubwa ni kununua mitambo ya kuchoronga ili kurahisishia wachimbaji wadogo kuacha kuchimba kwa kubunibuni. Miaka ya nyuma huko tulikuwa tunasema ili mchimbaji mdogo aweze kujua hapa kuna dhahabu ama kuna kiasi gani, utamwona anakwenda kwa mganga wa kienyeji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ilipelekea mauaji mengi sana ya watu kwa sababu waganga wengi wa kienyeji walikuwa wanadanganya. Sasa tuna vifaa vya kuchoronga na tuna maabara nyingi nchini, kiasi kwamba wachimbaji wadogo wadogo wengi wanaweza kupata huduma hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee pia ninaipongeza Wizara hii kwa namna ambavyo miezi ya hivi karibuni baada ya mabadiliko ya maeneo mbalimbali, leseni nyingi ambazo zilikuwa hazifanyi kazi zilirudishwa na wamepewa wachimbaji wadogo wadogo. Katika Pori kubwa la Kigosi wachimbaji wadogo wadogo wamepata takribani leseni zaidi ya 2,000 na kuna nyingine zaidi ya 2,000 zinakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba, miaka michache ijayo uchumi wa madini Tanzania utakuwa ni uchumi mkubwa kuliko uchumi wa kitu kingine chochote kile. Sasa, hapa nina jambo ambalo ninataka Serikali inisaidie na inisikilize kwa makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Tanzania takribani katika *kilometre square* 945,000, tumefanya utafiti kwenye 16% tu. Kwenye lugha ya utafiti tunasema *QDS (Quater Degree System)* 16, lakini eneo ambalo lina madini inasadikika ni kubwa kuliko eneo hilo. Maana yake ni nini? Leo pale Nyarugusu ambapo inaaminika kuna *millions of ounces* za dhahabu kule chini, pale Rwamgasa kuna *millions of ounces* pale chini, pamegeuka kuwa miji. Sehemu zote hizi zinakuwa *urbanized* kwa sababu tumeshindwa kuzilinda, tumeshidwa kutengeneza mpango mahususi wa kulinda maeneo haya ili yaje kuwa na faida baadaye kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ombi langu ni kwamba, kwanza tuiwezeshe hii Wizara ikamilishe mpango wake wa kufanya utafiti kwa nchi nzima, utafiti ambao tayari mwaka jana tulipitisha pesa.  Ninaamini kwamba, wakifanya utafiti nchi nzima tutasaidia kuyalinda maeneo ambayo kesho kutwa yatageuka kuwa makazi ya watu *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la pili, tulete mfumo wa kuwa na *Mineral Land Bank*. Maeneo ambayo tunagundua kwamba yana madini tusiruhusu yakageuka kuwa makazi. Kwa sababu, mwisho wa siku hatutaweza kuwaondoa wale watu na tukiweza kuwaondoa, tutawaondoa kwa gharama kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo mifano mahususi. Pale Geita kuna eneo la Nyamarembo, eneo la Magema, eneo la Nyakabale; kuna madini mengi nchini, lakini mgodi umeshindwa kufanya maamuzi, *either* kuwalipa fidia au kuwaacha pale kwa muda mrefu kwa sababu tayari yamegeuka kuwa makazi. Kwa nini? Tulizembea kuyatenga maeneo haya na kuyalinda. Sasa, nchi yetu ni kubwa, maeneo ya madini ni mengi, lakini keshokutwa tutakuwa ni miji kila kona, tutashindwa kuchimba madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaaminika pale Nzuguni kuna dhahabu; inaaminika maeneo mengi ya Dodoma kuna dhahabu, lakini tayari ni miji, hatutaweza kuwaondoa. Jambo kubwa hapa Wizara hii iwezeshwe, kiwe ni kipaumbele maeneo haya yapimwe, maeneo haya yatunzwe, itungwe sheria yasimamiwe. Sheria hii ni muhimu kwa sababu kesho kutwa hayatakuwepo maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine; wakati tunafanya *High Resolution Geophysical Survey*, ni vizuri tukafanya mambo mawili. Tufanye maji, tuangalie maji pamoja na madini. Tulipata bahati ya kwenda Zambia; Zambia wana takribani *square kilometre* 740,000. Wako 95% ya kufanya *survey* ya nchi nzima na wanafanya mambo mawili. Wanaangalia wapi kuna maji mengi na wapi kuna madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu madini ni sehemu kubwa inayoleta *forex* kwenye Nchi ya Zambia, sasa tuna nchi kubwa uchumi wetu ni mkubwa ni vizuri tukawekeza kwenye eneo hili kwa bidii kubwa kwa sababu baada ya siku chache zijazo maeneo yote haya yatakuwa miji, yatakuwa vijiji na hatutaweza kuwaondoa na tutakuwa tumekula hasara kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tumeona juzi mafanikio makubwa sana kwenye uvuvi kwa maana ya *cage*, uvuvi wa vizimba, nami nilikuwa muumini sana wa kuhubiri uvuvi wa vizimba. Sasa hivi samaki wa Tanzania ni gharama kubwa, ni *expensive* kumla kuliko samaki anayetoka nje. Kwa nini, ni kwa sababu Ziwa Victoria namna linavyokwenda litakwenda kuwa *redundant* kwa sababu, maeneo yote ya mazalia ya samaki yamejaa magugu maji na magugu maji yanamaliza oksijeni chini, yanatengeneza *siltation,* kwa hiyo samaki kwenye *griding area* zote zitageuka kuwa matope na maeneo yote samaki watashindwa kuzaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna uhaba mkubwa wa samaki, hata wanaokaa pembeni ya Ziwa Victoria hawana samaki lakini wanaokaa pembeni ya ziwa Victoria hawawezi kula samaki kwa sababu ni bei ghali ni bora ule samaki wa kutoka nje ya nchi kuliko wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu hapa ni tuweke nguvu kubwa kwenye kudhibiti magugu maji Ziwa Victoria, ukifika leo Busisi kuna kisiwa cha magugu maji na hapo ni Busisi, kule Nkome kuna kisiwa cha magugu maji lakini kule Igombe kuna kisiwa cha magugu maji. Inawezekana tunaliona tatizo hili ni dogo, lakini baada ya muda mfupi tutakuwa na Ziwa ambalo halitakuwa na maana tena, samaki wamepungua na samaki hawazaliwi katikati ya ziwa, wanazaliwa *off shores*. Huku *off shores* hawawezi kuzaa sehemu ambapo hakuna oksijeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti ninakushukuru sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kanyasu. Tunaendelea na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, atafuatiwa na Mheshimiwa Maimuna Pathan, upande wa Serikali mjiandae.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nichangie hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mungu Muumba wa Mbingu na Nchi kwa kuniwezesha na kupata hii nafasi adimu kabisa ya kuweza kuzungumza na Watanzania wote kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi ambazo amezifanya ndani ya mwaka huu wa tano na sisi kama Wabunge wake washauri wake tunaenda vizuri kabisa, lakini pia hata hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, inatoa taswira kwamba tunapokwenda na tunapotoka ni jambo la kumshukuru Mungu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hakika tulipotoka ni mbali, nchi yetu imepita kwenye bonde la umauti, kupotelewa na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano kila mmoja tulikuwa tunatazamana kwamba tutamalizaje safari, lakini sasa hivi tunashukuru miradi inazidi kukamilika, bwawa la Mwalimu Nyerere limekamilika, lakini pia feri ya Busisi imekamilika na mambo mengine mengi lukuki siwezi kuyataja yote yamekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze sasa kwa kusema, ninatokea Mbogwe na Mbogwe tumepata neema mwaka huu Wizara ya Madini tumepata leseni nyingi, tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Madini kwa leseni alizozitoa, japokuwa kila kitu kizuri huwa kinakuwa na changamoto, taarifa ambayo hapa sasa hivi inasumbua kwenye mkoa huu wa kimadini, watu wanahitaji zile Sheria za Misitu na Sheria za Madini ziweze kulegezwa kidogo ili kusudi watu waende wakachimbe kwenye leseni zao. Kwa hiyo, kupitia hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, niiombe sana Serikali na wahusika wote kwamba waone sasa kila sababu hawa watu waliyolipia leseni huko waende wakaanze uzalishaji ili kusudi nchi yetu tuweze kupata mapato mengi na kuweza kukamilisha hii miradi mingine ambayo bado tunaihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu bado ina uhitaji mwingi, Majimbo yetu kila Mbunge hapa ukiongea naye ukimuuliza bado mahitaji yapo ni mengi pamoja na kwamba yaliyofanywa ni mengi, lakini shida na zenyewe bado zipo nyingi majimboni. Kupitia mkoa wa kimadini wa Mbogwe nina imani tuna trilioni nyingi tunaenda kuzipata, nikiangalia upande wa barabara kila Mbunge hapa ukimuuliza barabara zake hazipo sawa, lakini pia upande wa maboma wananchi walijenga miaka mingi huko maboma bado yana uhitaji wa pesa. Kwa hiyo, niiombe sasa Wizara ya Madini kwa vile tunaona kabisa kwamba dhahabu zipo nje nje hapo Mbogwe kwetu waweze kuwasiliana na watu wa *TFS* ili kusudi walegeze masharti hayo yaliyopo ili dhahabu ziweze kuchimbwa na kazi ziweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine hapa napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu. Waziri Mkuu umekuwa msaada wetu mkubwa sana Wabunge wako, tulikuwa tukipata na matatizo mbalimbali tunakufuata unatuelekeza kwamba nini cha kufanya, Mungu akubariki sana. Mwaka huu ni mwaka wa 10 Mheshimiwa Waziri Mkuu na amefanya kazi na hayati John Pombe Joseph Magufuli pia alikuwa akitusikiliza, lakini vilevile hajaonesha ubaguzi wala kinyongo chochote kwa Mama ametusikiliza, hajabadilika kwa kweli abarikiwe sana Baba Mungu ambariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza pia wasaidizi wake kwa maana ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Doto Mashaka Biteko pamoja na wengine ndani ya ofisi yake, Mungu awasimamie na hii hotuba yenu inatupa dira kwamba kama Wabunge nini cha kuwashauri na nini cha kufanya ili kusudi watu wetu waweze kuneemeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie masuala ya mikopo hii ya 10%, eneo hili halijakaa vizuri, naiomba ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu waweze kufanya maboresho vizuri na kwenye suala la ajira hasa walemavu wanapohitimu elimu ya juu, wapewe kipaumbele ili kusudi kuweza kuingia kwenye mifumo kuweza kulitumikia Taifa hili, kwa sababu unakutana na mwenye ulemavu amesoma vizuri, ana kila kitu na kipo safi, lakini changamoto ni

ajira. Kwa hiyo niiombe Serikali hii ya Awamu ya Sita watu wenye ulemavu iwape kipaumbele ikiwemo hiyo mikopo ya 10% pale inapotoka kwenye halmashauri zetu, lakini na wao kama wao kwa vile wamesoma, ni wasomi wazuri, waweze kuajiriwa na Serikali hii ili tubaki sisi wazima sasa tupambane, wale wengine kama ajira zitakuwa bado, lakini hawa wenye ulemavu waajiriwe kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine napenda kushauri hapa kwamba mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi, ninapenda kuwashauri viongozi wenzangu wa vyama vyote na wachungaji wote pamoja na mashehe, huu mwaka ni mwaka wa kuomba sana, tunahitaji tupate viongozi waaminifu kwenye Taifa letu, kitakachotutoa kwenye umaskini ni uaminifu tu, lakini ni mbaya sana pale mnapompata kiongozi asiye mwaminifu, matokeo yake tena kuja kuanza kutukanana pale tunapoanza kuzijadili ripoti za *CAG*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wananchi tunaowaongoza kwenye maeneo yetu kila mmoja wetu wanatujua kwamba huyu ana tabia gani na huyu ana tabia gani, kama kuna mtu ana tabia siyo nzuri siyo mwaminifu sana katika Serikali hii ya Awamu ya Sita na tunaenda kupigiwa kura wamalizane naye huko huko wananchi ili huku tunataka warudi wale wenye nguvu ya Mungu, wenye upendo na Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu tumelia na umaskini muda mrefu, tunahitaji sasa yatosha Waislamu na Wakristo waseme kwa Jina la Yesu tunatuma viongozi ambao ni waaminifu ili kusudi tupige hatua kwenye Taifa letu. Inauma sana wapo watu wanaolipa ushuru, wanalipa kodi wakitegemea maendeleo waone kwenye maeneo yao, inaumiza pale ripoti inapokuja kutoka *CAG* tena kuna baadhi ya watu wenzetu wamelihujumu Taifa, ukiangalia Mheshimiwa Rais, anavyopambana kutafuta miradi anajibana usiku na mchana anasafiri kuhakikisha kwamba Taifa lake lisikwame, miradi hii inatumwa kijijini, huko kijijini wanaenda kupokea watu wetu ambao ni wataalam wetu, kweli wapo wazuri, lakini wapo na wabaya. Wengi ni wazuri wabaya ni

wachache, kwa hiyo wachache watolewe kwenye mfumo wabaki waaminifu ili Taifa letu liweze kupiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu zipo changamoto katika miradi hii mingi tunajisifia, kwa mfano mimi zaidi ya shilingi bilioni 74 nimepokea kwenye Jimbo langu la Mbogwe, lakini ipo miradi mingine wananchi walikuwa wakishirikishwa, mradi unakuja unakamilika kabisa, unajitosheleza mwananchi kwa vile hajui huko, Mbunge na wewe upo bize huku na vikao vya bajeti wanaambiwa wananchi tena kuchangishwa, kitu ambapo Serikali hii imeshatoa hela ya jengo zima bila mwananchi kugusa kitu chochote, lakini kwa kutokutambua wananchi wetu wanaambiwa tena walete matofali, walete nondo, walete kokoto, unajikuta pesa zilizotolewa kwa mradi mzima zinaishia kwenye mifuko ya watu wengine, sasa hao ndiyo nawaombea washindwe kwa Jina la Yesu na waweze kupotea kabisa kwenye Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mama tena kwa kufungua demokrasia na juzi nimeona vyama 18 vimesaini, kwa hiyo niwaombe vijana wenzangu wote tukachukue fomu kuanzia tarehe moja ili tuweze kupimwa na wananchi na tuweze kuingia kwenye michakato na wananchi waweze kuhakikisha kwamba wanabadilisha uongozi mbovu wanaweka mtu yule wanayemwamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala lingine la rushwa, niwaombe wananchi kupitia mkutano huu ama jukwaa hili la Bunge, mtoa rushwa ni *cancer* moja kubwa sana. Kwenye maandiko matakatifu rushwa imekataliwa mara tatu, lakini pia hata sheria zetu rushwa hazitakiwi, sasa wananchi unapopewa rushwa na mtu isiwe ndoa ya kufunga naye, wewe chukua rushwa kaa kimya halafu za kwako kwenye akili sasa kufikiria kwamba hii rushwa niliyopewa huyu hana mapenzi mazuri na mimi, mwisho wa siku usimpe kura kabisa ili kusudi ajue kabisa kwamba unajua na tunajielewa vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kukushukuru wewe, ninajua na wewe unaingia kwenye michakato hii ambayo

tunategemea kuingia wote, Mungu akubariki, Mungu akusimamie sana na wewe ukavuke salama ni imani yangu tutarudi pamoja lakini cha msingi tumtangulize Mungu, hata faulo tutakazoanza kuzicheza huko baada ya Bunge letu Tukufu kuvunjwa tarehe 27 najua kila mtu atatoka na sura yake hapa. Kwa hiyo, tumwombe Mungu, pia vile vyombo ambavyo vimepewa kutusimamia kama marefarii wetu haki ndiyo kitu pekee ambacho kitatuvusha salama, kwa sababu hata vurugu huwa zinaanzia pale haki inapokuwa haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hata jinsi vita zinavyotokea nchi zingine chanzo kabisa ukikuta haki imepindishwa lazima vurugu itakuja tu. Ndiyo maana mimi nasema kipaumbele changu mimi ni haki amani baadaye, mtu akivunja haki yangu lazima tuvurugane, mambo ya amani yatakuja baadaye. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa wito kwa wale wote viongozi waliyochaguliwa kutusimamia kwenye uchaguzi huu watende haki ile ya Mungu, mimi Maganga kama kura zangu hazitoshi ziache hivyo hivyo zikae hivyo, usiniongezee wala kuniibia kura. Nikiwa nimeshinda ziache hivyo tu hivyo kura zangu zikae hivyo kwa sababu mimi siamini katika haramu kwenye maisha yangu. Haramu mimi ni mtu wa halali, kwa maana hiyo na Wabunge wenzangu niwaombe tusiwe na ubaridi wala unyonge twendeni tukapambane na tuhakikishe tunatafuta haki ya Mungu na tukipata haki ina maana Taifa letu litazidi kuwa la haki, tukipata haramu ina maana na Taifa letu litakuwa haramu kwa sababu tulipatikana kiharamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nimshukuru Mungu, nikushukuru sana, niwashukuru watu wote walionisikiliza, ahsanteni sana na Bwana awabariki sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nicodemas. Tunaendelea na Mheshimiwa Maimuna Pathan, upande wa Serikali wajiandae.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi siku ya leo kuchangia hoja ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai siku ya leo, pumzi yake kwa bei ya bure kabisa pia ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambazo anazifanya, akishirikiana na Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, kazi zao wanazozifanya hakika zinaonekana. Tunashukuru sana viongozi wetu chini ya Chama cha Mapinduzi kwa kuwa wameitekeleza sana vizuri Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja iliyopo mbele yetu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nichangie machache kwenye hoja hii. *(Mkaofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuna reli yetu ya *SGR*, kuna treni ambayo tunaitumia sasa hivi, ndugu zangu hii reli ni ya kizalendo. Niwaombe Watanzania tuitunze, tuithamini na tuendeleze hii reli yetu ya *SGR*, hii ni reli ya kwanza Tanzania ya kizalendo ambayo imejengwa na Watanzania wenyewe. Kuna reli ile ya *TAZARA* ile ilijengwa na Wachina, kuna reli nyingine hii ya kati na yenyewe imejengwa na Wajerumani, kwa hiyo ni uthubutu mkubwa sana sisi Watanzania wenyewe *whether* kwa pesa zetu wenyewe au kwa kukopa, lakini ni uthubutu ambao tumeuanzisha Watanzania wenyewe, hakika ni tunu kubwa sana kuwa na *SGR*. Tunaona jinsi inavyopunguza muda wa kusafiri kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam, badala ya masaa tisa au 10 tunatumia masaa matatu na nusu hakika kweli tuwapongeze viongozi wetu kwa kazi kubwa waliyoifanya na maono makubwa waliyoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo mwanzo kwamba reli hii ni ya kizalendo, hii tumetengeneza sisi wenyewe, tuitunze, tuithamini ili iende vizuri, tusiharibu cha kwetu. Najisikia fahari sana ninaposafiri nikitumia chombo hiki cha *SGR*, ninakuwa na amani kwa muda mfupi ninafika ninapokwenda bila wasiwasi

wowote. Mungu awaongoze viongozi wetu waweze kuiendeleza mpaka pale walivyopanga ifike Nchi ya Congo, ifike Rwanda na kwingineko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana tuangalie mpango mbadala kwa wananchi wa Mkoa wa Lindi, mpango mkakati wa kimaendeleo. Kama tunavyojua Serikali inafanya juhudi kubwa sana kuondoa wanyama wale tembo, inajitahidi kwa kweli na kazi zao zinaonekana, lakini pamoja na hayo tujue sasa hivi kwa Mkoa wa Lindi kutakuwa na njaa kubwa sana, kwa hiyo niombe sana Serikali kwa sababu mazao hayakai kule. Hivi juzi eneo la Kilimarondo kuna mtu alilima heka 30 zote zimevamiwa na wanyama, vyakula vyote vimeliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu na ninajua juhudi kubwa wanazozifanya Serikali, bado tuwaombe waendelee, lakini pia lile wazo langu ambalo nilishatoa mara nyingi la kuweka *solar electric fence* kwenye maeneo ambayo yamezungukwa na mbuga za Wanyama. Naomba Serikali bado iendelee kulitilia mkazo najua ni suala la muda mrefu siyo la haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kuliongelea ni Mradi mkubwa wa Maji wa kutoka Mwalimu Nyerere kuelekea Mkoa wa Lindi na Mtwara. Mkoa wa Lindi hatuna mradi mkubwa wa maji, tuna miradi midogo midogo ya maji, ombi langu kwa Serikali kuna maji ambayo yanaweza kutusaidia watu wa Mkoa wa Lindi na Mtwara yanayotokea kwenye bwawa la Mwalimu Nyerere. Huu mradi tukiunganishwa na sisi wananchi wa Mkoa wa Lindi na Mtwara utatunufaisha sana, niiombe Serikali iweze kufikiria chanzo hicho cha maji, huo ni mradi mkubwa ili na sisi wananchi wa Mkoa wa Lindi na Mtwara tuweze kufaidika na mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala la umeme kama alivyoongelea Mbunge mwenzangu pale Mheshimiwa Kuchauka, tunaomba wananchi wa Mkoa wa Lindi na Mtwara tuungwe kwenye gridi ya Taifa. Tatizo tulilonalo la umeme ni kubwa sana lakini tatizo hili litakaa vizuri au litapungua pale tutakapoungwa

na sisi kwenye gridi ya Taifa, niiombe sana Serikali ijitahidi kufanya hivyo ili nasi tufaidi matunda ya Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Serikali kwa matengenezo ya haraka ya madaraja kwa barabara ya Kusini ya kwenda Lindi na Mtwara ilipokatika kutokana na mvua, lakini wamejitahidi wamefanya kazi usiku na mchana, Mheshimiwa Waziri alikuwa pale, amerejesha barabara, usafiri tunasafiri vizuri tunaelekea Kusini, lakini bado niwaombe Serikali tuwe na barabara mbadala kumtoa mwananchi anayetoka Liwale apite Nachingwea aende Masasi, aende Tunduru apite Ruvuma aende Mbeya apite kule Njombe, Iringa aje Dar es Salaam, *route* ni ndefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali yetu sikivu itutengenezee barabara ile ya kufungua mkoa ya kutoka Lindi kwenda Morogoro. Barabara hii ya kupitia Liwale ikitengenezwa itasaidia sana inapotokea janga kama hilo, siyo tu inapotokea janga kama hilo itapunguza foleni na matatizo mengine kwenye kutumia barabara moja kwa sababu barabara hii itakuwa ni fupi sana itasaidia sana wananchi hasa kusafirisha mazao ya wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe pia, Serikali kuna wananchi ambao walipisha upanuzi wa viwanja vya ndege Wilaya ya Kilwa na Wilaya ya Nachingwea muda mrefu sana, ni zaidi ya miaka kumi tumekuwa tukilizungumzia hili. Niiombe Serikali yangu sikivu kwa kuwa, malipo hayo walisema yapo kwenye bajeti ya mwaka huu unaoisha mwezi wa Juni, niombe iweze kuwalipa wale wananchi kwa sababu, hawajui wafanye nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine maeneo yao yalikuwa ni yaleyale, hawana maeneo mengine ya kulima, hawana maeneo mengine ya kuishi, wamekaa hawaelewi wafanye nini. Niiombe Serikali yetu sikivu iweze kuwalipa wananchi wa Kilwa na Nachingwea, kwa ajili ya ku-*compensate* maeneo yao ili maisha yao yaweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ajira kwa walemavu. Ajira kwa walemavu kiukweli, kidogo wamesahaulika. Kuna kijana nilikuwa ninahangaika naye muda mrefu kweli, ni wa kule kwetu Mkoa wa Lindi; amesoma vizuri, ana *degree* yake, lakini ni mlemavu. Amekuja Dodoma mara nyingi sana, kuja kufanya *interview,* lakini inaonekana hawa walemavu nafasi zao zile bado hawazipati vizuri. Ninajua Serikali yetu ina nia nzuri sana, Serikali yetu ni sikivu, niiombe iendelee kusimamia ajira za walemavu, ili waweze kupata haki yao ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe pia Barabara ya kutoka Masasi kuelekea Nachingwea kwenda Liwale. Nimeona kuna mradi mpya ambao utatengeneza barabara kipande kidogo, lakini bado niendelee kuiomba Serikali, barabara hii ni ya msingi sana na ni ya kimkakati, iweze kutenga bajeti ili barabara hii iweze kutengenezwa kwa kuwa, barabara hii ni muhimu na ni ya mkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi mikubwa imefanywa na Serikali kwa kweli, tumeiona. Miradi ya maji imemwagwa mingi sana, shule za sekondari, shule za msingi, zahanati, vituo vya afya na pale Kilwa sisi tumepata bandari ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Mama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa, ametoa miradi mingi kwa nchi nzima, amejitahidi, mama amefanya; sisi wananchi wa Lindi, Bandari ile ya Kilwa na miradi ambayo ameileta tunamshukuru sana. Niwaombe ndugu zangu Watanzania wote ambao mnanisikiliza sasa hivi, kazi alizozifanya mama zinaonekana, ni nyingi mno na kila sehemu kwenye Majimbo yote, si ndio ndugu zangu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana, mama huyu kwa kazi alizozifanya tunatakiwa tumwongezee miaka mingine mitano, ili aweze kumaliza miradi yake ambayo ameianzisha na miradi ambayo inaendelea, kama neno lake linavyosema, kazi inaendelea na yeye ataendeleza miradi yake. Ahsanteni sana ndugu zangu. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea na uchangiaji, ninaomba niwatambue wageni ambao wamekuja muda huu. Wageni wa Waheshimiwa Wabunge:-

Wageni 97 wa Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, ambao ni Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Bagamoyo, Viongozi wa Kata za Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze, Waheshimiwa Madiwani wa Viti Maalum na Wawakilishi wa Wazee wa Chalinze, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Bagamoyo, Ndugu Abubakar Kalama Bulawa. Karibuni sana viongozi wetu. Karibuni Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 100 wa Mheshimiwa Paschal Patrobass Katambi, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, ambao ni Halmashauri Kuu ya CCM, Wilaya ya Shinyanga Mjini wakiongozwa na Ndugu Arnold Makombe, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Shinyanga Mjini. Pia, wapo, wageni wengine 52 wa Mheshimiwa Katambi, ambao ni Watumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga Mjini. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Patrobass Katambi, ambao ni watoto wake watatu na mdogo wake kutoka Jijini Dar es Salaam, ambao ninaomba niwatambue kwa majina; tunaye Ndugu Ernestina Patrobass Katambi, Ndugu Praise Patrobass Katambi, Ndugu Michelle Patrobass Katambi na Daktari Adolf Katambi. Hii ni familia ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Karibuni sana kwenye Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji na sasa Serikali inafafanua na kujibu hoja za Wizara zao. Kwa kuanzia tutakuwa na Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi au Naibu Waziri, sina uhakika.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. AMINA DAUD HASSAN:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutuletea hotuba ya mwaka wa fedha 2025/2026 ambayo imesheheni mambo ya maendeleo katika nchi. Pia niwapongeze watendaji wako wote kwa utendaji wao wa ufanisi na waliokupa ushirikiano mema pia Naibu Waziri Mkuu Dkt. Doto Biteko pamoja na viongozi wote wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri tangu alipoanza kuiongoza nchi hii tarehe 19 Machi, 2021. Nimpongeze pia kwa sababu kumekuwa na mafanikio makubwa aliyoyapata katika kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020. Kwa kweli ametekeleza kwa vitendo na matokeo yanaonekana na vilevile katika kipindi cha uongozi wake tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kila kona ikiwemo kuimarisha miundombinu, kuboresha utoaji wa huduma za kiuchumi na jamii, kusimamia utawala bora, kuongoza mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi na kuhamasisha uwekezaji, diplomasia ya kiuchumi na ushirikiano wa kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Muungano wetu, Serikali inaendelea kuratibu vikao vya Kamati ya Pamoja kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi kwa ajili ya kushughulikia masuala ya Muungano. Katika mwaka 2024/2025 vikao viwili vya kujadili masuala ya Muungano vilifanyika na kupitia vikao hivyo ilifanyika tathmini ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Pamoja ya kushughulikia masuala ya Muungano. Kutokana na vikao hivi wananchi wa pande zote mbili wamenufaika kwa makubaliano yaliyowekwa kwa maslahi ya pande zote za Muungano.

Mheshimiwa Spika, mirada mbalimbali ya kimaendeleo inatokana na maendeleo ya Muungano wetu. Tukiangalia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF III);* miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kutokana na kuongezeka kwa kina cha

maji ya Bahari ya Hindi, Sipwese Pemba na mradi wa kurejesha ardhi iliyoharibika pamoja na kuongeza usalama wa chakula katika maeneo kama ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mirada ya programu za kukuza uchumi, kupunguza umaskini na kuboresha maisha; miradi hii imeleta mafanikio makubwa kwa wananchi kwa kutatua changamoto mbalimbali hasa katika kaya maskini kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, pia nizungumzie ushuru wa forodha kati ya pande mbili ya Muungano; naishukuru sana Serikali yangu ya Jamhuri ya Muungano kwa kuweka bayana ushuru wa bidhaa zote ambazo zimeainishwa katika bango maalumu katika pande zote mbili za Muungano kwenye maeneo ya Bandari ya Zanzibar pamoja na Bandari ya Der es Salaam, lakini bado kuna ukosefu wa viashiria vya uadilifu kwa wananchi hasa kwa wanaohama katika pande za Muungano.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali yetu izidishe nguvu katika suala hili kwani inaharibu taswira ya Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, hivyo namba kuunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kutoa mchango wangu kwenye hotuba hii ya Waziri Mkuu ya mwaka huu wa 2025. Nampongeza sana Waziri Mkuu kwa usimamizi wake katika majukumu ya kazi zake. Kwa umuhimu mkubwa nasema kwa sauti kumpongeza sana Rais Dkt. Samia kwa juhudi zake na usimamizi mahiri wa kuiongoza nchi yetu na hivyo kuhakikisha kwamba Ilani yetu ya Uchaguzi inaendelea kutekelezwa kwa ufanisi wa hali juu.

Mheshimiwa Spika, napongeza sana Makamu wa Rais kwa jinsi anavyomsaidia Rais katika majukumu ya shughuli za uendeshaji nchi yetu. Pongezi pia kwa Naibu Waziri Mkuu kwa jinsi anavyowajibika kwa kiwango cha juu kabisa.

Mheshimiwa Spika, tunathamini dhana nzima ya Rais wetu falsafa za *R4* zinavyoweza kuchangia ustahimilivu, maridhiano na mabadiliko ya pamoja na kuijenga nchi ikiwa imara na tulivu. Kwa dhana hii Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia anatuweka kwenye njia sahihi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya juhudi sana kuzalisha fursa za kuongeza ajira kutokana na kuanzishwa miradi mikubwa ya maendeleo, mfano ujenzi wa bomba la mafuta, bwawa la kufua umeme pia ujenzi wa uwanja wa ndege wa Msalato ambao unakwenda kuwa lango muhimu la kuinua uchumi wa Tanzania. Usafiri na kuunganisha ulimwengu itakuwa jambo lenye tija sana.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa *SGR;* reli muhimu sana ambayo imewaondelea wananchi wa Tanzania wakijikomboa na dhiki ya usafiri, kupata usafiri wa hakika na wa haraka, haya ni mafanikio makubwa. Kwa sasa reli imekamilika Dar es Salaam-Dodoma na mradi unasonga mbele kuelekea kukamilisha kipande cha kufikia Mwanza na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, kwenye sekta ya kilimo juhudi kubwa zimeelekezwa kwenye miradi ya umwagiliaji. Tunatambua kwamba sekta hii ya umwagiliaji ndio uti wa mgongo wa kilimo na Serikali imetenga bajeti kubwa kwa eneo hili. Wakulima wameendelea kuandaliwa kulima kwa tija, napongeza sana kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo la faida na maana sana kwa Serikali kutia nguvu ya ziada kuanzisha shule za sayansi za wasichana katika mikoa 26 ujenzi ambao umeigharimu Serikali shilingi bilioni 121.55 na wanafunzi 10,274 wanakwenda kupata elimu ambayo inahitajika kwa ustawi wa nchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wa vyuo vya kati na elimu ya juu wamefaidika sana na fursa ya *Samia Scholarship Program* kuwanufaisha wasomi kwenye nyanja za sayansi, teknolojia, ubunifu, uhandisi na tiba. Jambo la kutia moyo ni kwamba shilingi bilioni 6.63 zimeelekezwa na tayari wanufaika 1,313 wamehusika.

Pia wanafunzi wa vyuo wa stashhada wamenufaika kwenye fani za ufundi, kuwahusisha wanafunzi 7,732 kwa mafanikio hayo inaashiria tunakwenda kupata ufanisi mkubwa kuelekea kuinua viwanda vyetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee ninaomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza vyema miaka minne kwa kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususani barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa uzoefu na weledi wake, kama ilivyo kwa Watanzania walio wengi, nina imani kubwa kwa Mheshimiwa Nchimbi na kumtakia afya njema na kila la heri kwenye mchakato ujao.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kutekeleza majukumu ya kumsaidia Waziri Mkuu, ikiwa na pamoja na jukumu la kuendelea kuisimamia ipasavyo sekta ya nishati.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika na pia uongozi wote

wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika ya Ushindani wa Kimataifa *(National Competitiveness)*. Bajeti hii ambayo ni ya mwisho, inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi chake akiwa Waziri Mkuu, tathmini zinathibitisha mafanikio makubwa ya utekelezaji na usimazi wa Mpango wa Kwanza na wa Pili na kupelekea Taifa letu la Tanzania kufanya vizuri mno kuinua uchumi katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2023, pato halisi la Taifa kwa bei za mwaka 2015 lilifikia shilingi billioni 148,399.76 kutoka shilingi billioni 141,247.19 mwaka 2022, sawa na ukuaji wa 5.1% ikilinganishwa na 4.7% mwaka 2022. Ukuaji huu ni wa kiwango kizuri sana ukilinganisha kikanda na hata kidunia. Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)* ya mwezi Julai, 2024, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia imeendelea kupungua hadi kufikia 3.3% mwaka 2023 ikilinganishwa na 3.5% mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha ukuaji wa pato la Taifa kwa nchi za ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC)* ulikuwa kwa wastani wa 4.6% na 3.9% mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa 4.2% na 5.0% mwaka 2022 mtawalia. Vilevile ukuaji wa uchumi wa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ulipungua hadi kufikia wastani wa 3.4% mwaka 2023 ikilinganishwa na 4.0% mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mwendelezo huo mzuri wa kiuchumi, Kampuni ya Moody’s imechapisha matokeo Machi, 2024 ambapo Tanzania imepanda kutoka daraja la chini la *B2*

*(with Positive Outlook)* na kwenda ngazi ya juu ya *B1 (with STABLE Outlook)*. Matokeo hayo ni ya juu kabisa katika ukanda wetu wa Afrika Mashariki na hivyo hatuna budi kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake mahiri uliowezesha Taifa kupata mafanikio hayo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukua hadhi kimataifa, bado kuna kigugumizi kwa baadhi ya Taasisi za Kifedha nchini kuelekeza mikopo kwenye sekta muhimu za kiuchumi ikiwemo kilimo. Serikali kupitia Benki Kuu *(BoT),* ilitenga shilingi trilioni moja kuwezesha mabenki kutumia dirisha hili kukopesha sekta ya kilimo kwa riba isiozidi 10%. Kwa muda mrefu sasa hilo dirisha halijaonesha mafanikio ya kuchochea mabenki kupunguza riba kwenye mikopo ya kilimo na hata Taasisi za Serikali zinazonunua mazao ya kilimo bado zinahangaikia kupata hiyo fursa na badala yake kulazimika kukopa kwa riba za juu.

Mheshimiwa Spika, kilimo kama ilivyo kwa madini na utalii, zinaliingizia Taifa asilimia kubwa ya fedha za kigeni, Serikali iweke mkakati wa kuvutia uwekezaji ikiwemo mikopo ya mabenki ili kuongeza tija na ushindani katika masoko ya kimataifa. Kutokana na kilimo kuajiri asilimia kubwa ya Watanzania, Serikali itenge bajeti ya kuongeza mtaji wa angalau shilingi bilioni 150 kwa Benki ya Kilimo *(TADB)*.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 mpaka Machi, 2025 Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya kimkakati kwa mafanikio makubwa sana na utekelezaji huu unaonekana mpaka kwenye ngazi ya halmashauri zetu. Mafanikio makubwa yamejikita kwenye uboreshaji wa miundombinu ya barabara, reli, bandari, mtandao wa mawasiliano na uboreshaji wa usafiri wa anga. Naipongeza Serikali kwa hatua nzuri za utekelezaji wa mradi wa kihistoria wa ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR* na ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (megawati 2,115). Miradi hii miwili ya *SGR* na umeme ni nguzo imara ya kiushindani katika uchumi wetu na nchi za Maziwa Makuu na hata za Kusini mwa Afrika na Kati.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatakiwa kuendelea kuchukua hatua za kibajeti kukabiliana hasa na mfuko wa bei na kuporomoka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani na sarafu kuu zingine. Kwa kuzingatia kuyumba kwa uchumi wa dunia, bajeti hii ijielekeze kuchukua hatua za kuchochea uzalishaji wa ndani ili kupunguza nakisi ya urari wa biashara *(balance of payment – BOP),* kuimarisha pato la Taifa kupitia sekta za kilimo, madini, utalii na uchukuzi. Hatua hizi ziende sambamba na kuimarisha mazingira ya uwekezaji hasa kwenye sekta ya kilimo na madini. Pia Serikali iendelee kusimamia sera ya fedha na bajeti ikiwemo ukimarisha mifumo na kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Kutokana na utekelezaji wa miradi ya kimkakati, kunapelekea mahitaji makubwa ya fedha za kigeni na hivyo msukumo uwepo kwenye kuongeza uzalishaji wa madini na mazao ya kilimo. Hatua hizi ni muhimu kuhakikisha utulivu wa thamani ya shilingi na pia kuimarisha uhimilivu wa deni la Taifa hasa kwenye kigezo za ulipaji wa deni la nje kwa kulinganisha na uuzaji wa bidhaa nje (mapato ya fedha za kigeni).

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto za tabianchi, bado kuna fursa kubwa kwa Tanzania kwenye uzalishaji wa ziada wa nafaka ukilinaganisha na nchi za ukanda huu. Serikali iimarishe upatikanaji wa pembejeo bora kwa bei nafuu na kuimarisha upatikanaji wa masoko ya uhakika kupitia *NFRA* and Soko la Bidhaa *(TMX)*. Kutokana na ruzuku kwenye mbolea na jitihada walizofanya Wizara ya Kilimo kuwapatia vitendea kazi Maafisa Ugani, ichochee kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo kutoka uzalishaji wa sasa wa kilo 1,000 za mahindi kwa eka mpaka kilo 4,000 kwa eka ya mahindi. Tanzania ina fursa kubwa ya biashara ya hewa ukaa *(carbon credit)* ikiwa ni pamoja na kuwa chanzo cha uhakika wa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na msukumo kwenye kilimo, madini na utalii, Serikali inatakiwa kuwekeza hasa kwenye miundombinu ya usafirishaji ikiwemo barabara, reli, bandari na usafiri wa anga hasa kwa mizigo. Kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha, zimesababisha uharibifu mkubwa kwenye miundombinu ya barabara na hata reli. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, barabara zinazohudumiwa na

*TARURA* kwa zaidi ya 80% zipo kwenye hali mbaya sana kutokana na mvua kubwa na pia kwa kukosa matengenezo ya mara kwa mara. Maeneo mengi ya vijijini barabara hazipitiki kutokana na ufinyu wa bajeti ukilinganisha na mtandao wa barabara zinazohudumiwa na *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ichukue hatua za haraka kunusuru hali hii ili wananchi waweze angalau kusafirisha mazao yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuidhisha ujenzi wa barabara ya njia nne kuanzia Nsalaga (Uyole) mpaka Ifisi jirani na uwanja wa ndege wa Songwe. Kipande hiki cha barabara ambacho ni sehemu ya barabara kuu ya *TANZAM*, ni muhimu sana kwa kuinua uchumi wa Tanzania na hata kupunguza ajali za mara kwa mara zinazotokea katika mteremko wa Mlima Iwambi kuelekea Mji wa Mbalizi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa usafirishaji wa mazao yetu kwa soko la ndani na nje ikiwemo fursa za biashara ukanda wa *SADC* na uzalishaji mkubwa kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, napendekeza mwendelezo wa uboreshaji wa barabara za *TANZAM* kipande cha Igawa - Tunduma; barabara ya *bypass* ya Uyole - Songwe; barabara ya Mbalizi – Shigamba – Isongole kutokana na uzalishaji wa mazao ya kilimo; barabara ya Mbalizi – Galula – Makongorosi kutokana na uzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo na madini; na pia barabara ya Isyonje – Kikondo – Makete.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya kazi kubwa kuhakikisha ujenzi wa *SGR* unaendelea kwa kasi ile ile na pia napongeza jitihada za kuendelea kutafuta vyanzo vya fedha vya masharti nafuu kugharamia ujenzi huo. Pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa, Serikali imefanya maboresho makubwa ya miundombinu na huduma katika bandari zetu hususana Bandari ya Dar es Salaam ili kukabiliana na ushindani mkubwa wa bandari zingine za ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika. Bandari ya Dar es Salaam inakumbana na ushindani mkubwa toka Bandari

za Mombasa (Kenya), Beira (Msumbiji), Nacala (Msumbiji), Durban (Afrika Kusini), Lobito (Angola) na Walvis Bay (Namibia).

Mheshimiwa Spika, maboresho ya bandari zetu iendane na kuondoa changamoto zingine ambazo zinasabisha gharama kubwa za usafirishaji kwa bandari zetu na kusababisha kupoteza biashara ya usafirishaji kwa bandari shindani. Ufanisi wa bandari unategemea pia maboresho ya barabara, reli ya kati *(TRL)*, reli ya *TAZARA*, utendaji wenye tija wa wadau wote wa bandari na hata watumishi ili kupunguza gharama za usafirishaji kwa wateja wa bandari zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa zilizopo, zaidi ya 70% ya mzigo wote wa nchi za nje unasafirishwa kwa kupitia *Dar es Salaam Corridor* inayohudumia cchi za DR Congo, Zambia na Malawi. Pamoja na fursa za kijiografia ya bandari zetu, mzigo unaopita sasa kwenye Bandari ya Dar es Salaam, ni 50% tu ya biashara yote ambayo kwa sasa inashikiliwa na bandari shindani. Kwa ajili ya kunusuru biashara hii inayopotea kwa bandari shindani, Serikali ichukue hatua za haraka kuboresha huduma za *TAZARA* ikiwa ni pamoja ya maboresho ya miundombinu ya reli, ununuzi wa vichwa vya reli, mabehewa na vitendea kazi vingine.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali kwa haraka ishughulikie maboresho ya mkataba wa *TAZARA* na kisha kutafuta mbia mwenye uwezo wa kifedha na uendeshaji. Katika kipindi hiki cha ushindani mkubwa usafirishaji wa reli ni mojawapo ya suluhisho kubwa la kupunguzo mzigo wa bei kubwa kwa wateja wa bandari zetu na hata wananchi. Pamoja na maboresha ya reli ya *TAZARA*, napendekeza kuendelea na ujenzi wa Bandari Kavu Mbeya ambayo ina fursa kubwa katika kipindi hiki katika kuwezesha kupunguza gharama za kusafirisha kwa wateja wa bandari na hata kupunguza bei za mafuta ya petroli, pembejeo na mazao ya kilimo. Bandari Kavu ya Mbeya ni njia panda kwa wateja wa nchi za Malawi, Zambia, DRC, Lubumbashi na hata kwa Zimbabwe na Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kuvutia wawekezaji na kuongeza pato la fedha za kigeni, napendekeza Serikali

kuchukua hatua kuharakisha uwekezaji kwenye mradi wa madini ya kimkakati kidunia, ikiwemo na gesi ya Helium na madini ya Niobium. Serikali iweke msukumo kuanza kwa uzalishaji wa gesi ya Helium na uzalishaji wa madini ya Niobium ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Kiwanda cha Ferroniobium *(FeNb)* ambacho kitakuwa cha kwanza Afrika na cha nne duniani. Kutokana na mahitaji makubwa ya ujenzi wa reli, madaraja na reli ya *SGR,* kuna mahitaji makubwa ya vifaa vya chuma ambavyo ni imara, lakini vyepesi na vyenye ubora wa kimataifa. Kwa kutumia sheria zetu za uwekezaji, Serikali itumie fursa za kipindi hiki ili kuvutia wawekezaji kwenye madini ya viwandani ili yaongezwe thamani hapa kwetu na pia kuvutia malighafi ya madini toka nchi zingine ili yachakatwe hapo kwetu. Tanzania imebahatika kuwepo kwa madini ya Niobium ambayo inapatikana milima ya *Pandahill* Songwe, Wilaya ya Mbeya na mahitaji ya Ferroniobium *(FeNb end product)* ni makubwa duniani na hapa kwetu pia.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia rasilimali zetu za madini, Serikali inaweza kutengeneza fursa nyingi na kupitia Mradi wa Niobium na Kiwanda cha Ferroniobium, ajira 2,000 zitakazozalishwa wakati wa ujenzi na pia kutakuwepo ajira za kudumu zaidi ya 600 na *indirect jobs 7,000.* Mradi utazalisha mapato kila mwaka shilingi bilioni 500 *(US$ 220 million)* ambapo mapato kwa serikali kila mwaka shilingi bilioni 50 *(US$ 22 million)* uhai wa mgodi ni zaidi ya miaka 30. Hiki kitakuwa kiwanda cha kisasa cha kwanza Afrika *(modern manufacturing plant and smelter)*. Pamoja na kuingiza teknolojia hii adimu na ujuzi *(skills transfer)* pia itakuwa itachangia huduma za kijamii *(corporate social investment in community)* na chanzo cha fedha ya kigeni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu kwa kutujaalia uhai na wasaa wa kuchangia hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Pili, nikushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania pamoja na Dkt. Emmanuel Nchimbi, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kuchaguliwa kuwa wagombea wa Urais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Pia nikupongeze Mheshmiwa Waziri Mkuu kwa kuendelea kuwa kiongozi mahiri na kuisimamia Serikali kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika Ofisi ya Waziri Mkuu pia nawapongeza Mawaziri wote, Naibu Mawaziri na watendaji wote wa Wizara zilizopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Ofisi ya Waziri Mkuu imeendelea kusimamia masuala mazima ya utumishi kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusimamia na kuhakikisha mazingira ya kufanyia kazi yanakuwa bora na watumishi wanakuwa salama katika utekelezaji wa majukumu yao. Naishauri Serikali iongeze kasi katika suala zima la kaguzi mahala pa kazi kupitia OSHA.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusimamia masuala mazima ya utatu yaani usimamizi wa uhusiano mzuri kati ya wafanyakazi, waajiri na Serikali kwa kuwa na mahusiano mazuri na pia imeendelea kusimamia vyema vyama vya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara inayosimamia Sera, Bunge na Uratibu chini ya Waziri Mkuu, imeendelea kuratibu masuala mazima ya kuzuia na kupambana na dawa za kulevya kupitia Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Mamlaka hii ilikuwa ikifanya kazi katika mazingira magumu kwa kuwa na bajeti ndogo ya matumizi ya kawaida, pili haikuwa na fungu la maendeleo katika Bunge hili Tukufu tumeishauri Serikali sikivu ilikubali na kuipatia mamlaka hii fungu la bajeti ya maendeleo. Kwa sababu hiyo tumeona sasa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya inafanya kazi kwa weledi na ufanisi mkubwa kwani iliweza angalau kwa kiasi kidogo kuongeza vitendea kazi mfano walinunua boti na wameongeza vituo vya matibabu *(MAT- Clinic)*.

Mheshimiwa Spika, ni jambo lisilopingika kuwa watumishi hawa wanafanya kazi nyeti sana na kwa muda mrefu wamekuwa na bajeti ndogo sana ya Matumizi ya Kawaida *(OC),* watumishi wamekuwa hawalipwi maslahi yao mfano posho mbalimbali katika kazi hizo ngumu wanazofanya, lakini wameendelea kufanya kazi kwa uadilifu na uzalendo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha 2025/2026 tumeishauri Serikali iongezee bajeti mamlaka hii na Serikali sikivu inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imekubali kuongeza bajeti ya shilingi 5,000,000,000 kwa ajili ya maslahi mbalimbali ya watumishi na kwa ajili ya ofisi za kanda, kwa hakika hii itaongeza sana tija.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali tuliishauri tuwe na Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, kwa kuwa suala la dawa za kulevya ni suala mtambuka kuna haja ya mapambano haya kuhusisha wadau mbalimbali, tunaipongeza Serikali kwamba imekamilisha sera hiyo ambayo inaitwa Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya mwaka 2024.

Naipongeza Serikali kwa kuwa mamlaka hii sasa imeweza kwanza kuanzisha Kituo cha Habari na Mawasiliano *(call center)* kupitia namba 119 ambapo Watanzania watapata elimu na maelekezo ya matibabu bure. Pili Serikali imeanzisha maabara ya uchunguzi wa awali wa sampuli za dawa za kulevya, tatu mamlaka na sasa imejidhatiti na imethubutu kufanya tafiti na kubaini matumizi ya dawa za kulevya kupitia shisha, mimea mbalimbali, hii inafanywa na watumishi na wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kazi kubwa imefanyika, kwa muktadha huo nimpongeze sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu na Kamishna Aretas Lyimo wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya pamoja na watumishi wa mamlaka kwa kufanya kazi kwa uzalendo mkubwa kwa muda mrefu pamoja na maslahi kuwa madogo bila ya kukata tamaa na ufanisi wa juu katika kazi hii njema ya kupambana na dawa za kulevya mpaka sasa Serikali

imekubali ushauri wa Kamati na kuwaongezea bajeti ya Matumizi ya Kawaida *(OC)* kuboresha maslahi ya watumishi hao, hii ndiyo Serikali sikivu inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan na wafanyakazi tunasema Dkt. Samia mitano tena, na maslahi bora kwa wafanyakazi na huo ndiyo moyo wa Rais kwa watumishi.

Mheshimiwa Spika, pia ninaipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kukamilisha ujenzi wa kiwanda kipya cha Uchapaji wa Nyaraka za Serikali na kufungwa kwa mitambo ya kisasa hakika kazi kubwa imefanyika, sasa nyaraka zote za Serikali za siri na za wazi zitachapishwa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa ubora na usalama na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya na wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kusimamia vyema shughuli za Serikali kwa umakini, kwa kujitolea na kizalendo. Kwa ufuatiliaji na utendaji wako imesaidia kuwabaini watendaji wasiosimamia vyema miradi ya Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu nitajikita katika maeneo matatu ya kilimo, maji na miundombinu ya nishati na maji.

Moja ni kuhusu kilimo, ninaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa pembejeo za zao la korosho bure kwa wakulima. Hii imesaidia kuongezeka kwa mikorosho inayohudumiwa na hiyo kuongeza uzalishaji wa zao la korosho kutoka tani 244,000 hadi tani 500,000 kwa msimu uliopita. Ushauri wangu ni kuiomba Serikali kuendelea kutoa pembejeo ya ruzuku na kutatua changamoto zilizopo kwenye tasnia ya korosho baadhi yake ni tozo nyingi, upungufu wa maghala na kadhalika.

Pili, naishukuru Serikali kwa maboresho na upanuzi wa mradi mkubwa wa maji wa Makonde, kwa sasa mradi huu unasuasua kwa sababu mkandarasi anadai fedha. Naomba mkandarasi alipwe ili aweze kuendelea na utekelezaji wa mradi.

Tatu, Barabara ya Kibiti - Lindi imeharibika na inahitaji ujenzi upya na si ukarabati. Naomba ujenzi wake uzingatie mahitaji halisi ya barabara hiyo. Aidha, miundombinu ya nishati kwa Mikoa ya Kusini iimarishwe ili ipunguze kukatikakatika kwa maji.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuungana na Watanzania wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake katika nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuungana na wananchi wa jimbo langu la Mbulu Mjini kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali nzima ya Awamu ya Sita kwa jinsi wanavyoiongoza Taifa letu na kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2020-2025 Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa - Waziri Mkuu, Mawaziri, Naibu Mawaziri wote walio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi kubwa wanayoifanya toka mwaka 2020 hadi 2025, hakika mambo mengi yaliyoshindikana muda mrefu yamefanyika.

Mheshimiwa Spika, nazipongeza sana Kamati zetu zote za Kudumu zinazosimamia bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara zilizoko chini ya ofisi yake.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kupitia mapendekezo ya bajeti ya Wizara hii muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwanza tunaomba Serikali itoe fedha zote zinazoombwa katika kifungu hiki kwa 100% ili tuweze kutekeleza mambo yote yaliyokusudiwa.

Pili, Serikali ijitahidi kupeleka walimu wa elimu maalumu kwenye shule zote nchini ambazo tayari tumejenga miundombinu ya huduma kama madarasa, mabweni na kadhalika, lakini

hakuna walimu na watumishi wasio walimu, mfano huu uko Shule ya Msingi Endagikort katika Halmashauri ya Mbulu Mjini.

Tatu, Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza pensheni ya wastaafu wa zamani wanaolipwa shilingi 100,000 hadi shilingi 150,000 kwa kuwa kundi hili lina changamoto kubwa sana ya kugharamia huduma za afya na mahitaji mengine ya maisha.

Nne, Serikali ijitahidi kuongeza bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kitengo cha Maafa kwa kuwa hali ya mabadiliko ya tabianchi yanazidi kuleta majanga mengi sana bila kutarajiwa na kusababisha madhara makubwa ya maisha ya Watanzania na rasilimali zingine.

Tano, Serikali iangalie utaratibu wa kuweka mkakati wa kuzuia utengenezaji na uingizaji wa bidhaa zilizo chini ya kiwango kwani tunapata athari za kiafya na kiuchumi kwa kuwa ukaguzi unafanyika wakati wauzaji, wasambazaji na watumiaji tayari wameshaathirika.

Sita, Serikali iangalie upya kupitia *blueprint* tumefanikiwa kiasi gani na upande wa wadau wake wanasemaje kama upande wa pili ili kufanya tathmini na kuleta mafanikio na maaboresho zaidi.

Saba, tayari tumepata mafanikio makubwa sana katika dhana ya uwekezaji, Serikali ijikite kuwahamasisha na wawekezaji wenye fursa ya kuajirika kwa kundi kubwa la vijana nchini.

Mheshimiwa Spika, nane, kwa kuwa Serikali ilikuwa na nia njema ya kujenga barabara kilometa 2035 za *EPC+F* nchini na kwa kuwa sasa huenda mpango ule hatutaweza kutekeleza na wananchi wa maeneo hayo wanasubiri kwa hamu kubwa sana ujenzi wa miradi hiyo Serikali iangalie namna ya kujenga hizo barabara ili kujibu kiu ya wanufaika wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, sasa naunga mkono hoja 100% na naomba kuwasilisha.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa hotuba yake nzuri ya bajeti. Pia niwapongeze Mawaziri Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu na Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa utendaji wao mzuri.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita kwenye kundi la vijana na maendeleo yao kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Taifa kuwekeza kwenye maendeleo ya vijana ni muhimu sana. Uwekezaji huu unatakiwa upanuke zaidi ya kuwapatia vijana huduma za elimu ya kawaida kwa ngazi ya elimu ya sekondari na vyuo na kuwasaidia vijana wavinjari na kutambua vipaji vyao na kuvijengea mikakati ya kuvitekeleza kwa vitendo na hatimaye kufikia ndoto zao za maisha.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inakabiliwa na tatizo kubwa la ukosefu wa ajira kwa vijana. Hivyo basi, ni muhimu sana Serikali ichukue hatua za kimkakati ili kuondokana na tatizo hili kwani lina hatarisha kesho yetu kama Taifa. Katika kipindi hiki, kumekuwa na ongezeko la vijana wengi wanaomaliza elimu katika ngazi mbalimbali (sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu) kila mwaka na kuishia majumbani na mitaani kwani katika soko hakuna ajira za kuwachukua.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hii ya ukosefu wa ajira kwa vijana wetu, Serikali inapaswa kuanzisha programu zenye uhalisia kutatua changamoto za ajira kwa vijana. Ni muhimu sana Serikali ikaanzisha mpango maalumu wa kuwapa vijana ujuzi ili uweze kusaidia kwenye kuzalisha ajira za haraka katika kundi hili. Programu hizi zinatakiwa zilenge idadi kubwa ya vijana walioko mitaani bila ajira, wale walioko mashuleni na vyuoni na wale wanaotarajia kujiunga na masomo ya sekondari na vyuo vya kada zote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Serikali imeanza kuweka mazingira rafiki ya kuwawezesha vijana kushiriki kikamilifu

katika shughuli za maendeleo, kujipatia ajira na kujikwamua kiuchumi, lakini juhudi hizo ni ndogo mno ukilinganisha na ukubwa wa hii changamoto.

Mheshimiwa Spika, niipongeze sana Serikali kwani kutokana na ukubwa wa tatizo hili, wameanzisha mitaala mipya ya elimu inayolenga kuwaandaa vijana kujitegemea na kupunguza tatizo la ajira. Katika hili, Serikali imeweka kipaumbele katika utoaji elimu ya kukuza ujuzi wa ujasiriamali kuanzia shule za msingi, sekondari hadi vyuoni. Kwa mfano, wameanzisha masomo ya stadi za kazi kwa shule za msingi na taasusi ya ujasiriamali ambayo ni hiyari katika vyuo mbalimbali. Mabadilko haya yanategemewa kuleta ukombozi wa kiuchumi na maendeleo katika Taifa letu. Hivyo basi, ni muhimu Serikali ikawekeza rasilimali fedha ya kutosha katika mipango hii.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huu, ni vyema Serikali ikahusisha na kuwashirikisha vijana kwenye mambo mbalimbali ya msingi ambayo yakizingatiwa yataleta mabadiliko makubwa. Ili kufanikisha hili, napendekeza Serikali ifanye yafuatayo kwani yanaweza kuwa muarobaini wa kuwakomboa vijana wa nchi hii dhidi ya janga la ukosefu wa ajira.

Kwanza, Serikali iwe na programu maalumu ya kuhamasisha ujasiriamali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali zikiwemo *NGO'S* zinazoshughulika na masuala ya vijana.

Mheshimiwa Spika, kuanzisha uhamasishaji wa ujasiriamali kwa vijana kutachochea ushiriki wa vijana kuanzisha shughuli za kuwapatia ajira na kipato. Serikali inaweza kutoa mafunzo ya ujasiriamali kupitia semina na mikutano mbalimbali kwa kushirikiana na *NGO's* zote zinazosaidia maendeleo ya vijana hapa nchini. Hii itachochea ushiriki wa vijana kutoka maeneo yote na kuwasaidia kujiajiri na kukuza uchumi wao na wa Taifa.

Pili, Serikali iwekeze kuwezesha vijana kujiajiri kwenye sekta isiyo rasmi. Ni vyema Serikali ikaboresha mazingira ya sekta hii kwa kutoa ruzuku na mafunzo ya kibiashara kwa vijana. Kufanya hivi kutasaidia sekta isiyo rasmi kuwa rasmi na kutoa fursa nyingi

zaidi za ajira kwa vijana. Hili likifanyika, vijana wengi wasio na ajira wataingia kwenye sekta isiyo rasmi na kuboresha maisha yao.

Tatu, kuhamasisha makundi ya vijana kuwekeza kwenye kilimo, mifugo na uvuvi; kilimo, mifugo na uvuvi ni sekta zenye fursa nyingi na uwekezaji wa kimkakati kwenye maeneo haya kunaweza kuwakomboa vijana wengi. Kwa kuwa nchi yetu ina ardhi ya kutosha ya kilimo na mifugo na maji ya kufugia samaki, sekta hizi zina uwezo wa kutoa ajira nyingi mno iwapo vijana watafundishwa kilimo na ufugaji wa kibiashara. Programu za Jenga Kesho Bora *(Build Better Tomorrow - BBT)* zilizoanzishwa na Serikali ni mifano yenye nia nzuri ya kuwapatia vijana ajira katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi. Naishauri Serikali iendelee kuwekeza kwenye miradi hii muhimu na ipanue wigo kwa kuwashirikisha wadau wengine wa kutoka ndani na nje ya nchi.

Nne, uwezeshaji vijana kupata mitaji; ni vyema Serikali ikaja na mikatati kabambe ya kuwasaidia na kuwezesha vijana kupata mikopo kwa masharti nafuu. Mkakati huu ni vyema uambatanishwe na mafunzo na ushauri wa kibiashara na ujasiriamali kwa vijana wanaoanza miradi katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Serikali ina programu ya kuwapatia vijana mikopo isiyo na riba kupitia halmashauri za wilaya, ni kwamba hadi sasa haijakidhi mahitaji ya vijana wote wanaotaka kusaidiwa hapa nchini. Hivyo basi, ni vyema Serikali ikashirikiana na taasisi za fedha na kuja na mifumo rafiki ya mikopo isiyo na riba kubwa na inayojali changamoto za riba kubwa kwenye mabenki yetu. Mikopo nafuu itawezesha vijana kuwa na uwezo wa kuanzisha miradi na biashara mpya zitakazolipa kwa pande zote mbili.

Tano, kuwezesha vijana kwenye uwekezaji katika viwanda vidogo vidogo; vijana wa Kitanzania wanaweza kupata maendeleo ya haraka kwa kujiajiri wao binafsi au katika vikundi na kuanzisha viwanda vidogo na kuwatafutia soko lenye tija kwa bidhaa watakazozalisha. Kushirikisha vijana kwenye hili suala la

ujenzi wa viwanda, kutasaidia Taifa kujenga uchumi imara na endelevu.

Sita, ushirikiano na Taasisi za Kimataifa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; kwa kuleta mashirika mbalimbali, hasa yenye programu za maendeleo ya vijana, Tanzania inaweza kujifunza kutoka kwa nchi zingine jinsi ya kutatua changamoto za ajira. Mashirika haya yanaweza pia kusaidia kutoa mafunzo na mitaji kwa biashara changa zinazomilikiwa na vijana. Wizara inatakiwa ichukue mifano ya nchi zilizofanikiwa kama China na kuwapekeka vijana kwenda kuiga miradi mbalimbali ya maendeleo.

Saba, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (*Youth Development Fund –YDF)* uongezewe fedha; katika mipango mipya ya maendeleo, Serikali itoe fedha ya kutosha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kwa lengo kuu la kuwawezesha vijana kupata mitaji ya kutosha ili wajitengenezee fursa nyingi za ajira. Kwa maoni yangu, pesa inayotolewa na Serikali kuendesha mfuko huu ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, nimalizie mchango wangu kwa kushauri kwamba katika hili suala la vijana, ni muhimu kuwepo na ushirikiano kati ya sekta zote na Serikali, kwa kuhakikisha kuwa uwekezaji, elimu na sera zinazoimarisha ujasiriamali na kubuni mazingira rafiki ya ukuaji wa ajira yanapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. BAHATI KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ametufanyia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kwa ufupi kama ifuatavyo nikianza na mafanikio makubwa ambayo tumeyapata katika sekta zote, nani kama Samia? Niwaombe Watanzania wote wasisikilize matapeli wa kisiasa, tulikuwa na shida ya usafiri kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma, leo tunatumia saa chache tu tumefika Dodoma.

Mheshimiwa Spika, lililobaki kwa sasa tuangalie usafiri wa majini kwa zile sehemu ambazo hawajapata usafiri wa *marine*.

Mheshimiwa Spika, tuipongeze Serikali kwa kupata umeme na pia tubadilishe miundombinu ili wananchi waweze kufanya biashara zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri karibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, ningependa kutoa ufafanuzi kwenye sekta yetu. Kimsingi nianze kumshukuru kwanza yeye kwa uongozi thabiti wa sekta hii, kwa kuniamini mimi msaidizi wake niweze kutoa ufafanuzi wa hoja chache kwa niaba yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na nitafafanua maeneo machache ambayo kimsingi yameonekana kwetu. Maelezo yangu yataanza kwanza kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu, ukisikiliza Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu unaona mambo mengi na makubwa yaliyofanyika kwenye Sekta ya Uchukuzi, ambayo pengine huko nyuma ilikuwa ni kama historia. Nitajikita kwenye maeneo machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na bandari. *Performance* ya bandari yetu imeongezeka mara dufu, Watanzania wanakumbuka miaka minne nyuma mzigo uliokuwa unasafirishwa kwenda nje ya nchi ulikuwa ni tani 5,600,000, lakini ndani ya miaka michache hii umefika takribani tani 9,100,000. Hata mzigo kwa ujumla, wa nchi nzima, ulikuwa ni tani takribani 16,000,000, lakini leo umefika tani 27,000,000 unaweza ukaona ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatokana na kazi kubwa ya maboresho ya bandari iliyofanyika katika nchi yetu, ukianza na

Bandari yenyewe ya Dar es Salaam, uchimbaji wa kina na mradi wetu mkubwa zaidi ya dola milioni 421 na Bandari yetu ya Mtwara, ambapo takribani shilingi bilioni 429 zimeelekezwa, ambayo imesababisha hata *performance* ya bandari sasa kuongezeka kutoka mzigo uliokuwepo wa tani karibu 600,000/700,000 mpaka 1,600,000. Hivyo hivyo kwa Tanga, fedha takribani shilingi bilioni 157 zilielekezwa pale na *performance* imefikia karibu tani 1,000,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamezungumza juu ya maboresho ya bandari mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Ziwa Victoria. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, mpaka 2021 Serikali ilikuwa imerasimisha bandari karibu 86, sasa zimefika bandari 135 na zote hizo sasa zipo kuanzia Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika pamoja na Ziwa Nyasa. Kwa upande wa Ziwa Victoria tumeshaanza maboresho makubwa kwenye Bandari ya *North* Mwanza, Kemondo na Bukoba, hivyo niwaombe Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa *Engineer* Ezra na wengine, hatua kwa hatua tutakwenda kufikia bandari zao pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi mnafahamu, kwenye Ziwa Nyasa tunajenga bandari kubwa kuliko bandari nyingine yoyote iliyowahi kujengwa hapo nyuma, Bandari ya *Mbamba-Bay* kule Nyasa, lakini pia, upande wa Ziwa Tanganyika tumeshafanya ujenzi mkubwa kuanzia Kalema – Kabwe mpaka na Kigoma kwenyewe. Hivyo, hata maeneo mengine niwape uhakika Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba ya Serikali kwamba, tutakwenda kuzifikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa *SGR*. Kwanza, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, nishukuru Wabunge wote kwa kutambua na kuthamini kazi kubwa ambayo Serikali, chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeifanya ya uwekezaji mkubwa kwenye *SGR*. Hili ni jambo ambalo halijawahi kutokea kwenye historia yetu, leo Watanzania wanasafiri kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma na kurudi kwa muda mfupi, kwa raha mustarehe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya tulizoea kuyaona kwa watu wengine, Ulaya, leo yapo hapa Tanzania na hivyo kuifanya nchi yetu kuwa ndio nchi inayojenga reli ndefu kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza mpaka Kigoma na sasa tunaelekea mpaka Burundi, takribani zaidi ya kilometa 2,400. reli ndefu kuliko zote za kisasa Barani Afrika ipo Tanzania inajengwa. Tunaipongeza Serikali, kama ambavyo imezungumzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kwenye upande wa miundombinu ya viwanja vya ndege. Hivi ninavyozungumza karibu kila kona ya nchi tunafanya maendelezo ya viwanja vya ndege. Ukianza na kule Iringa uwanja upo karibu 98%, ukienda Shinyanga, ukienda Mwanza, ukienda Musoma, ukienda Arusha, ukienda Moshi, Lindi, Mtwara, Tabora na Rukwa, karibu kila sehemu. Zaidi ya shilingi trilioni moja zimeelekezwa katika kuboresha miundombinu hii ya viwanja vya ndege na hili linakwenda sambamba na kuongeza ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wanafahamu, takribani miaka 10 nyuma tulikuwa na ndege moja tu, mwaka 2016, leo tuna ndege 16 ikiwa ni pamoja na ndege ya mizigo. Haya ni mambo ambayo kimsingi hayakuwepo huko nyuma, tumeyafanya. Hivyo basi, hata maeneo ambayo viwanja vya ndege pengine hatujaanza, ikiwa ni pamoja na Njombe, Simiyu na maeneo mengine, Serikali inaendelea na mchakato, itayafikia na itajenga viwanja vya ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge kwa hisia kubwa ni kwenye meli. Kama ambavyo nimezungumza, unapozungumzia uchukuzi unaanzia baharini ambako mzigo ndiko unafika, unakuja usafirishaji ambako ndiyo reli, *SGR,* pamoja na *meter gauge* na pili, unakwenda kwenye upande wa pili kwenye maziwa makuu. Serikali imefanya kazi kubwa sana katika miaka hii minne na hasa katika mwaka huu wa fedha ambao tunauzungumzia, ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu ameuzungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kuainisha kwa ufupi; kwenye Ziwa Victoria tayari meli yetu ya *MV Mwanza Hapa Kazi Tu*, ambayo ilianza kujengwa miaka michache iliyopita ipo 98%. Ninataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, ndani ya miezi hii michache itakuwa imekamilika na itaanza kutumika. Kama hiyo haitoshi, Serikali imefanya maamuzi ya kujenga meli nyingine mpya ya tani 3,000 katika Ziwa Victoria, meli hii haijawahi kujengwa, lakini pamoja na hiyo tunaendelea na ukarabati, tumesaini mikataba ya *Mt Ukerewe*, Nyangumi, Clarias na Butiama na wiki ijayo meli yetu ya Butiama itaanza kufanya kazi tena baada ya kusimama hapo katikati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, Ziwa Tanganyika ambalo limekuwa likizungumzwa na wenzetu, Wabunge wa Mikoa hii ya Kigoma, Rukwa na Katavi kwa muda mrefu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameelewa umuhimu na ameamua kufanya mambo mengi na makubwa katika ziwa hilo. Jambo la kwanza ni, ukarabati wa meli yetu ya *MV Liemba* iliyojengwa Mwaka 1913 ikasimama mwaka 2019, tumeenza ukarabati rasmi mwaka jana, fedha tumeshalipa na hivi ninavyozungumza tupo 19%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni meli yetu ya Mwongozo iliyojengwa mwaka 1982 ikasimama mwaka 2006 kufanya kazi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameamua kuanza kuikarabati. Tumesaini mkataba tarehe 8 mwezi uliopita, wa miezi kama tisa hivi ili ikarabatiwe irudi kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, meli yetu ya *Mt. Sangara* ambayo na yenyewe ilijengwa mwaka 1981 ikasimama kufanya kazi mwaka 2018 na yenyewe ipo 98% ya ukarabati. Tunachosubiri kwa sasa hivi ni ifanyiwe majaribio, siyo muda mrefu itaanza kufanya kazi. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameelewa kwamba, Ziwa Tanganyika ni uchumi, hivyo anajenga meli nyingine kubwa ya mizigo ya tani 3,500; meli hii haijawahi kuwepo katika mwambao wetu wa maziwa makuu. Meli hii, itakuwa na uwezo kama nilivyozungumza, itakuwa ina

urefu wa mita 124, yaani kiwanja cha mpira uongeze na mita nyingine 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, meli hii itakuwa na uwezo wa kubeba mzigo sawa na malori marefu 25 au mabehewa 25 ya *SGR,* behewa moja likiwa na uzito wa tani 140 kwenye sakafu moja. Sakafu ya chini itakuwa na uwezo wa kubeba magari madogo 65, haijawahi kutokea katika historia ya nchi yetu. Watanzania tuungane kumshukuru kiongozi wetu kwa maono, uthubutu na utayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza, kutoa mzigo Dar es Salaam mpaka ufike Kalemie unahitaji kutumia siku saba, meli hii ikamilika pamoja na *SGR,* ndani ya saa 24 utakuwa umeutoa mzigo Dar es Salaam na kuufikisha Kalemie, Kongo. Tuna kila sababu ya kuendelea kushukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili tunakwenda kujenga kiwanda kikubwa cha kujenga meli ambacho kitakuwa na uwezo wa kuweka meli mbili za tani 5,000 kwa wakati mmoja, nacho hakijawahi kiwepo katika historia yetu. Kiwanda hiki ambacho nakizungumza kinajengwa Katabe, Kigoma, kitasaidia nchi jirani zote za Zambia, Kongo na Burundi kujenga meli mpya na kukarabati zilizokuwepo. Hivi ninavyozungumza tayari mkandarasi ameshalipwa pesa za awali, *advance payment,* ili aanze maboresha na pia, tumeshalipa shilingi 1,000,000,000, kwa ajili ya ujenzi wa barabara pale Katabe na wenzetu wa *TANESCO* wanaanza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea miundombinu hii ya ujenzi wa meli ikiungana na *SGR* na maboresho ya baharini, vyote kwa pamoja vinakwenda kufanya mapinduzi makubwa ya sekta ya uchukuzi katika nchi yetu ya Tanzania. Baada ya maelezo hayo, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Kuhusu Utaratibu; hoja iliyopo mezani ni hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sasa tutampa nafasi

Mheshimiwa Waziri Mkuu kuendelea kuwasikiliza Wabunge katika ujumla wake wakiwa wanachangia Bungeni. Hoja binafsi ambazo zinaenda kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu zitatafutiwa nafasi nyingine. Kwa hiyo, kuna nafasi ile ambayo imewekwa, kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge kuongea na Mheshimiwa Waziri Mkuu itabaki wazi kwa kipindi hiki chote mpaka tutakapohitimisha hoja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa fursa hii. Ninaomba nianze kwanza kwa kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Hoja ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Waheshimiwa Wabunge walio wengi wamepongeza kazi kubwa na nzuri ambayo imefanywa na Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi na ni kweli kwamba, Serikali hii ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya kazi kubwa sana ya kimapinduzi, kazi kubwa ya kutukuka na ya kihistoria katika kuleta miradi ya maendeleo kwa wananchi. Sote tumekuwa ni mashahidi kwa hakika, tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais, lakini pia, tunamshukuru kwa kazi kubwa aliyofanya na tunamwombea afya njema, ili aendelee kulihudumia na kulitumikia Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya kazi kubwa na nzuri ya kupigiwa mfano ya kumsaidia Mheshimiwa Rais, ya kuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni na pia, kama msimamizi wa shughuli za kila siku za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hakika ni kiongozi wa mfano; ni kiongozi rahimu, ni kiongozi mwema, ni mchapakazi, lakini pia, ni kiongozi mwema. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana kwa uongozi wako na tunakuombea sana afya njema ili uendelee kulitumikia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, wametoa michango mingi, lakini kwa maana ya muda nitaongea katika maeneo makubwa matatu; nikianza na eneo la Barabara za Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini *(TARURA)*. Serikali inatambua umuhimu wa barabara; barabara ni uchumi, barabara inadumisha na kuboresha huduma za kijamii na ndio maana mwaka 2017 ilianzisha Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini ikiwa na lengo, kwanza kuhakikisha barabara zetu zote za vijijini na mijini zinaboreshwa kwa wakati, lakini pia, kuongeza mtandao wa barabara za vijijini na mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka minne ya Serikali hii ya Awamu ya Sita barabara za vijijini na mijini bajeti yake imeongezeka sana kwa zaidi ya mara tatu ya bajeti ya mwaka 2020/2021. Kwa mfano, mwaka 2020 na 2021 Bajeti ya *TARURA* ilikuwa ni shilingi bilioni 250 tu, leo mwaka 2024/2025 Bajeti ya *TARURA* imeongezeka mpaka kufikia shilingi bilioni 870.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imeendelea kuongeza mtandao wa barabara, mwaka 2020/2021 mtandao wa barabara za *TARURA* ilikuwa ni kilometa 108,946, lakini leo tunaongea mtandao umeongezeka mpaka kilometa 144,430. Hii ni kazi kubwa sana iliyofanywa na Serikali katika kuongeza mtandao wa barabara vijijini na mijini, kwa leo kusogeza huduma za usafiri bora kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TARURA* imeendelea kujenga barabara za lami, na barabara hizi za lami zimeendelea kuongezeka. Kwa mfano, katika kipindi cha miaka minne iliyopita kilomita za barabara za lami zilikuwa 1,449, leo tunaongea, Serikali imeweka fedha za kutosha katika ujenzi wa barabara za lami na

kiwango cha barabara kimeongezeka mpaka kilomita 3,467. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunaendelea kuzi-*upgrade* barabara za udongo kwenda kuwa barabara za changarawe kwa sababu barabara hizi zinadumu zaidi lakini pia zinarahisisha zaidi usafiri. Mpaka sasa tumeongeza sana ujenzi wa barabara za changarawe kutoka kilometa 27,309 mpaka kilometa 44,372. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamechangia kwa kina eneo la *TARURA;* na moja ya eneo ambalo wamechangia ni namna ambavyo Serikali ina wajibu wa kuongeza upatikanaji wa fedha kwa wakati ili kuwalipa makandarasi. Kufuatia muktadha huo Serikali ilifanya ubunifu na kuanzisha Mfuko wa Hati Fungani za Samia *(Samia Infrastructure Bond)* ambapo, mwezi *October* mwaka 2024, mwaka jana Mfuko huo ulifunguliwa ukiwa na lengo la kukusanya shilingi bilioni 150.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari njema ni kwamba mwitikio ulikuwa mkubwa na mzuri na mpaka sasa Serikali imekusanya zaidi ya shilingi bilioni 320 kwa ajili ya *Samia Infrastructure Bond.* Mfuko huu utawawezesha sana makandarasi wazawa, kwanza kuhakikisha kwamba wanapata mkopo wa masharti nafuu ambao hauhitaji dhamana ili waweze kukamilisha miradi yetu ambayo inaendelea katika maeneo yetu ya miji na vijijini. Kwa hiyo nitumie nafasi hii kuwatia shime makandarasi wazawa wote wanaofanya kazi kupitia *TARURA* wahakikishe wanatumia fursa hii nzuri ya *Samia Infrastructure Bond* kwa ajili ya kukwamua ile miradi inayokwama ili miradi yetu ya barabara vijijini na mijini isikwame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekta ya Elimu ya Msingi; tunafahamu kuwa elimu ndiyo nyenzo muhimu katika maendeleo ya Taifa lolote. Serikali hii ya Awamu ya Sita imeendelea kuwekeza kwa kiwango kikubwa katika Sekta ya Elimu ya Msingi na Sekondari. Katika kipindi cha miaka minne Serikali hii imefanya kazi kubwa ya kihistoria ya kujenga miundombinu ya huduma za elimu, kwa maana ya shule mpya za msingi, shule mpya za

sekondari, pia ujenzi wa madarasa na miundombinu mingine muhimu ya elimu. Katika kipindi cha miaka hii minne, jumla ya shule mpya za msingi ambazo zimejengwa ni 1,580 na shule mpya za sekondari zilizojengwa ni 1,031. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haijawahi kutokea katika kipindi cha miaka minne Serikali ikajenga shule kwa wingi kwa kiasi ambacho kimefanyika katika kipindi cha miaka hii minne. Waheshimiwa Wabunge ni mashuhuda, katika maeneo yetu tumeona kazi kubwa ambayo imefanyika. Lengo la Serikali ni kuendelea kusogeza huduma za elimu karibu na watoto wetu, karibu na wananchi na pia kupunguza mdondoko wa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha na kuondoa changamoto ya mdondoko, Serikali imeendelea kujenga mabweni kwa ajili ya watoto wa shule za sekondari na hususani watoto wa kike. Jumla ya mabweni 1,000 yamejengwa katika kipindi cha miaka minne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kuboresha sana huduma za chakula katika shule zetu za msingi na sekondari. Katika eneo la sekondari tumeendelea kujenga pia mabwalo. Waheshimiwa Wabunge katika michango wamesisitiza umuhimu wa kuboresha miundombinu hiyo na mabwalo yameendelea kujengwa. Jumla ya mabwalo 133 yamejengwa na yanatumika katika shule zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii iliweka mpango kabambe wa kukarabati na kujenga madarasa kwenye shule zilizopo, ambazo zina upungufu mkubwa wa madarasa. Katika kipindi hiki cha miaka minne Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amejenga jumla ya madarasa 62,685 katika shule za msingi na sekondari kote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii inatekeleza mpango wa elimu bila malipo ambapo Serikali inatoa zaidi ya shilingi bilioni 484 kila mwaka kwa ajili ya sekta ya elimu bila malipo. Ili elimu hii iwe bora, lazima tupate walimu. Serikali imeendelea kuajiri walimu kila

mwaka wa fedha; na mpaka sasa tangu mwaka 2020/2021 jumla ya walimu 45,809 wameajiriwa na kati yao msisitizo mkubwa, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge mmekuwa mkichangia, walimu wa sekondari wa masomo ya sayansi wameajiriwa 29,399. Wakati huo huo ufaulu wa elimu ya msingi na sekondari umeendelea kuongezeka kati ya 85% na 99.9%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Sekta ya Afya, Serikali hii ya Awamu ya Sita imevunja rekodi kwa kuwekeza kwa kiwango kikubwa sana katika Sekta ya Afya ya Msingi. Katika kipindi hiki cha miaka minne Serikali imewekeza zaidi ya shilingi trilioni moja na bilioni mia mbili tisini na saba katika Sekta ya Afya ya Msingi kwa kujenga hospitali za halmashauri 129, kwa kujenga vituo vya afya vipya 367 na kwa kujenga zahanati 980; kwa maana ya kuchangia nguvu za wananchi. Serikali itaendelea kuboresha sana miundombinu hii ya huduma za afya kwa kuhakikisha kwamba maboma yote yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi yanaendelea kukamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kupeleka magari ya wagonjwa. Jumla ya magari 316 yamepelekwa, yakiwemo magari ya wagonjwa 382 na magari ya kusimamia huduma za afya msingi 210. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile eneo la muhimu sana ambalo Waheshimiwa Wabunge wamechangia ni eneo la vifaa tiba. Mheshimiwa Rais kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI ameanzisha utaratibu wa kununua vifaatiba bora na vya kisasa katika kila mwaka wa fedha; na katika kipindi hiki cha miaka minne Serikali imenunua vifaa vya kisasa zikiwemo *digital x-rays,* mashine za *ultrasound,* vifaa vya maabara na vimepelekwa kwenye zahanati zetu, kwenye vituo vya afya pia kwenye hospitali za halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma zetu za afya zimeendelea kuboreka sana ndiyo maana katika historia ya nchi yetu, mwaka huu Mheshimiwa Rais amepewa zawadi au tuzo ya *The Global Goalkeeper Award,* ambayo imetokana na mafanikio makubwa ya kihistoria ya kupunguza vifo vya akina mama wajawazito

kutoka 500,056 kati ya vizazi hai 100,000 mwaka 2016/2017 mpaka vifo 104 tu kati ya vizazi hai 100,000 mwaka 2023. Niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba mafanikio haya makubwa yataendelea kufanyiwa kazi, ikiwemo eneo la ajira kwa walimu 25,936. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwneyekiti, ninahitimisha kwanza kwa kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge; na kwamba mafanikio haya makubwa ya sekta hizi nilizozisema kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni mafanikio yetu sote; na mimi ninawaombea katika mchakato unaofuata kwa kazi hii kubwa ya kutukuka na ya kihistoria; wote Mwenyezi Mungu akatujalie tuweze kurejea kwa sababu, kwa hakika tumeweka alama kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI. Tutaendelea na Mheshimiwa Waziri wa Maji, wajiandae Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niungane na Waheshimiwa Mawaziri wenzangu kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameifanya na kwa wasilisho zuri la bajeti yake. Moja, ni bajeti ambayo imesheheni mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na vilevile imebeba matumaini ya kweli ya Watanzania katika kuhakikisha kuwa wanapata maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati ya moyo nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu. Moja ya jukumu kubwa ni kumsaidia Mheshimiwa Rais; amemsaidia kwa vitendo. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa tumemwona maeneo mbalimbali akifanya kazi. Miongoni mwa maeneo ambayo aliona kuwa yanahitajika kuchukuliwa hatua ni hasa kwa watumishi wazembe. Huko amechukua hatua bila kuangalia pasi na shaka kabisa. Kwa dhati na kwa moyo tunajifunza mengi lakini kwa dhati

kabisa nimpongeze kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine, nipongeze Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Waheshimiwa Wabunge, wamepata michango mbalimbali kupitia bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini eneo la maji wamethamini kazi kubwa ambayo imefanyika katika kipindi hiki cha miaka mitano. Tunashukuru kwa jitihada na pongezi ambazo Wabunge wametupa, lakini yapo maeneo ambayo wameweza kuyachangia na nitaweza kuyatolea ufafanuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji tulipewa maelekezo mahususi na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan; alisema kwamba yeye ni mama na asilimia kubwa ya wanaoteseka juu ya adha ya maji ni akinamama, kwa sababu hiyo hataki kusikia na wala hataki kuona kuwa akina mama wa nchi hii wanateseka kutokana na adha ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa imefanyika katika eneo la maji. Miaka ya nyuma moja ya changamoto kubwa sana katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ikija bajeti ya Wizara ya Maji ilikuwa hapatoshi, lakini leo tunaona katika kipindi hiki cha miaka mitano, bajeti ya maji tumepata ushirikiano mkubwa hasa kwa Waheshimiwa Wabunge, hasa chini ya michango yao, lakini juu ya usimamizi mzuri wa Kamati yetu ya Maji na Mazingira na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yangu ninataka kusema kwamba; moja ya changamoto ilikuwa ni ufinyu wa bajeti. Miradi mingi imejengwa ilikuwa haikamiliki kwa sababu ya bajeti, lakini Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameongeza fedha katika eneo hili la maji. Leo tunaona na tunashuhudia kuwa miradi ambayo imejegwa tangu mwaka 1974 ambayo ilikuwa haikamiliki imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda zako kule Serengeti Mugumu ilikuwa ni mifano ya miradi dhahiri ambayo imejengwa kwa muda mrefu bila haikamiliki lakini leo imekamilika. Tulikuwa

tunafahamu kabisa kuwa tulikuwa na miradi chechefu zaidi ya 177 ambayo imejengwa lakini ilikuwa haitoi maji. Chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan miradi yote 177 imekamilika na inatoa huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo tumeona uthubutu wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kwenye miradi mingi mikubwa ya kimkakati iliyokuwa ikijengwa kwa fedha za wafadhili. Kwa sasa, kupitia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tunaona uthubutu wake kwamba fedha za ndani ndizo zilizowezesha kujenga miradi mikubwa ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Longido utakuta tumejenga miradi mikubwa. Leo tunajenga Bwawa la Farqwa, vilevile tunajenga Bwawa la Kidunda kwa ajili ya kupeleka maji Dar es Salaam, bwawa ambalo limezungumzwa kwa muda mrefu sana, lakini chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametupatia zaidi ya bilioni 335. Hivi ninavyozungumza mkandarasi yupo *site* na Mheshimiwa Waziri Mkuu amefika na ameweka jiwe la msingi. Hii ni miradi ambayo imezungumzwa na Bunge hili, yalikuwa ni maazimio ya Bunge kwa muda mrefu na chini ya Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tumeweza kujenga huu mradi. Ninaamini katika kipindi hiki kifupi tutaweza kukamilisha ili kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri zaidi na zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhamira yake ya dhati, ametupa malengo kuwa itakapofika mwaka 2025 kuwe na 85% ya upatikanaji wa maji vijijini na 95% ya upatikanaji wa maji mjini. Hivi ninavyozungumza mpaka hivi sasa leo vijijini tuna takribani 83% na mijini zaidi ya 91%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miradi ya kimkakati ambayo tunaendelea nayo zaidi ya 1,000. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, moja ya maelekezo yao na hoja ambazo wamezijenga ni kuhakikisha kwamba miradi ambayo tumeianza tunakwenda kuikamilisha. Ninataka niwahakikishie, jitihada ambazo tunazipata kupitia Wizara ya Fedha na *supportive* kubwa ya fedha, miradi yote ambayo tumeianza tutaikamilisha na

Watanzania waishio vijijini watapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ya Tanzania ina takribani vijiji 12,318. Mpaka sasa kupitia wakala wa maji vijijini *RUWASA* tumekwishafika kwenye vijiji zaidi ya 10,000 na zaidi, tumebakisha vijiji 2,000 tu. Mkakati wa Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha kuwa vijiji vyote vya Tanzania vinapata huduma ya maji safi na salama. Hii ni katika kutimiza dhamira yake ya kumtua mwanamama ndoo kichwani. Mheshimiwa Rais ametununulia mitambo ya uchimbaji wa visima, ametununulia mitambo ya uchimbaji wa mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa vijiji vyote vya Tanzania vinapata huduma ya maji safi na salama tumeanzisha *program* ya visima 900. Tumeanza *phase one* ambapo tutahakikisha kwamba katika kila jimbo tunachimba visima vitano na tutahakikisha kwamba hivi vijiji 2,000 tunavikamilisha. Tumeanza *phase one,* tunakuja *phase two;* mkakati wetu ni kuhakikisha kwamba vijiji vyote vinapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamejenga hoja ya kuwatetea wananchi wao. Kwa dhamira na *support* hii kubwa ambayo tunaipata kutoka kwa Mheshimiwa Rais sina mashaka, ninaamini kwamba vijiji vyote vitapata huduma ya maji safi na salama. Tunajua, si maeneo yote ukichimba maji utapata maji, yapo baadhi ya maeneo ni lazima uchimbe mabwawa. Tumepewa seti za mitambo ya uchimbaji wa mabwawa na kwa hiyo Wizara ya Maji haina kisingizio. Tumejielekeza huko na tumeanza kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda Handeni kwenkambala tumejenga bwawa kubwa la kimkakati kupitia mitambo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan; ukienda Kizengi kule Tabora tumejenga bwawa la kimkakati na sasa leo wanapata huduma ya maji safi na salama. Ukienda zako Monduli, tumejenga Bwawa la Lepurko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wetu ni kwamba mvua isiwe maafa, iwe fursa, hasa juu ya uchimbaji wa mabwawa kwa kuhakikisha kwamba tunavuna maji kwa ajili ya kunywa, kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na maji kwa ajili ya kutumika kunyweshea pia mifugo yetu iliyokuwepo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba, kumpata Rais aina ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hapatikani kila mahali na hapatikani kila wakati. Tumempata na hivyo ni lazima tumtumie kwa maslahi ya Watanzania. Hapa ninachotaka kusema ni kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni suluhu ya matatizo ya Watanzania. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jumaa Aweso, Waziri wa Maji, tunakushukuru sana kwa ufafanuzi wa hoja. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Abdallah Ulega.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na mwingi wa ukarimu. Pili, nitumie fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika mjadala huu wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu nzima ya ofisi yake kwa namna ya uwasilishaji mahiri na mzuri sana wa bajeti hii iliyoleta mwelekeo wa utendaji kazi wa Serikali uliokwisha kufanyika na ule ambao tunauelekea. Ninaomba pia nimpongeze yeye binafsi kwa namna ambavyo amemsaidia sana kazi Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mheshimiwa Waziri Mkuu hongera sana kwa kazi kubwa na nzuri uliyoifanya wakati wote katika kumsaidia kazi Mheshimiwa Rais, kinara wetu na jemedari wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wametoa michango inayohusu ujenzi wa barabara katika maeneo mbalimbali nchini.

Barabara na madaraja yanayoendelea kujengwa, lakini na yale maombi mapya vilevile ambayo tumekwishakuanza kuyapokea wakati huu ambapo tumekuwa tukijadili bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata zaidi ya Wabunge 20 waliochangia kwa namna ya kuzungumza hapa Bungeni, lakini vilevile kwa namna ya kuandika. Tunawashukuru sana kwa michango hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba uniruhusu nieleze machache sana juu ya mafanikio ambayo tayari pia yalikwishaanza kuelezwa katika risala na hotuba iliyosomwa hapa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Miongoni mwa mambo makubwa yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na kinara na jemedari wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni pamoja na miradi ya kielelezo ya kimkakati, kama vile Daraja la Kigongo-Busisi, Daraja la Pangani, Daraja la *Tanzanite* pale Dar es Salaam na miradi mingine mikubwa inayoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka minne ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yetu ya Awamu ya Sita ya Chama Cha Mapinduzi, jumla ya kilomita za lami 1,365 zimekamilika nchini kote. Hili Daraja la Kigongo-Busisi sasa limekwishakufika mwisho. Tunafahamu ya kwamba ni kiu ya Watanzania kuona kwamba jambo hili sasa linafunguliwa na linaanza kutoa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Naibu wangu, amekuwa akijibu maswali hapa na kueleza; na hata jambo la Kigongo – Busisi amelieleza. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu amelieleza pia. Ni matumaini yetu kuwa mwezi Mei, 2025, Daraja la Kigongo-Busisi panapo majaliwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan atakwenda kulifungua; na huo ndio utakaokuwa mwanzo na mwisho wa kuandikwa na kuelezwa kwa historia ya matumizi ya vivuko na habari ya vivuko katika eneo hili. Tunavichukua vivuko vile tunavitafutia maeneo mengine ya kwenda kuvipeleka. Hayo ni mafanikio makubwa ya Mheshimiwa

Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na ni mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia alilikuta daraja hili likiwa limefikia 20% tu ya utengenezwaji wake. Kazi kubwa ameisimamia, ameifanya na sasa kazi ile imekwenda kukamilika. Siku ya kulizindua daraja lile, tutawaalika Waheshimiwa Wabunge wote na wananchi wote wa Taifa hili kwa kuwa jambo hili ni kielelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja lile lina urefu wa kilometa tatu. Katika Eneo la Afrika ya Mashariki na Kati, hakuna daraja lingine refu linalozidi Daraja la Kigongo Busisi la John Pombe Magufuli (JPM). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, pia tunayo mafanikio ya *ring road* ya hapa Dodoma ambayo ina zaidi ya kilometa 104. Hii ni katika kuonesha namna tulivyojiandaa kama Serikali kuufanya Mji wa Dodoma kuwa ni Makao Makuu ya Taifa letu na namna ambavyo hatutaki kurejea makosa ya kuwa na misongamano tena hapa katika Jiji la Dodoma. Ndiyo maana tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuturidhia tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha huu mradi wa *ring road* ya Dodoma, tuna mradi mwingine mkubwa wa kutoka Chamwino kuingiza barabara sita mpaka Dodoma Mjini na nyingine zitatoka zitaelekea usawa wa Arusha na nyingine zitaelekea usawa wa Iringa. Hii ni programu ambayo sasa hivi tupo katika hatua za kimanunuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, naomba nieleze juu ya mambo mbalimbali yaliyoelezwa na Waheshimiwa Wabunge, ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa ya Kusini walivyoeleza namna ambavyo barabara hii imechakaa sana na namna ambavyo wanatamani kuona barabara hiyo inafumuliwa na kujengwa upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaeleze kuwa Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo. Tuna hatua kubwa mbili; kwanza, ni hatua ambayo haijaiva ambayo tunaendelea nayo, tunaitafutia fedha barabara hii ili tuifumue yote na tuanze upya ukiacha haya madaraja ambayo yanaendelea kujengwa sasa hivi. Wakati tunasubiri hilo, tayari tunayo maelekezo ya kuanza kutengeneza vipande kwa vipande hasa katika yale maeneo yaliyoharibika sana. Kwa mfano, eneo la kutoka Ikwiriri – Chumbi – Marendego mpaka Somanga, hili ni eneo ambalo limeharibika sana. Kwa hiyo, tayari hilo tumeliweka katika mipango ya bajeti ya 2025/2026 ili kuhakikisha kwamba tunalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, mvua zimekuwa zikituathiri sana. Sisi Serikalini tumejipanga vyema na tunashukuru sana kwamba wakati wote zinapotokea dharura hizi, huwa tunachukua hatua ya haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuru Mameneja wetu wa Mikoa na viongozi wa mikoa na wilaya; Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama wamekuwa wakitusaidia sana juu ya kuhakikisha kuwa mambo yanakaa sawasawa. Hata hili la Somanga, tunaushukuru sana Uongozi wa Mkoa wa Lindi na Wilaya ya Kilwa kwa namna ambavyo tumesaidiana kwenye kuli-*handle* jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge, ipo taarifa ambayo imesambaa jana usiku mpaka leo asubuhi ya kuwa daraja la muda la Somanga limekatika. Ninalihakikishia Bunge, daraja halijakatika, daraja la muda bado liko sawasawa. Mvua zinazonyesha nchini kote hususan katika maeneo ya Morogoro na mengineyo ambayo haya maji yote yanakwenda katika Bahari ya Hindi, yamefanya maji yapite juu ya daraja lile la muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa msingi huo, kwa ajili ya usalama wa watu, tukasema, tusubiri kwanza na hiki ni kitu ambacho tunakifanya sehemu nyingi ikiwa ni pamoja na kwenye

Daraja la Jangwani na kwingineko ili kuangalia usalama wa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, nasema tu, kazi inaendelea na kazi ni nzuri. Tunayo matarajio, tutakaposoma bajeti yetu tutaeleza kwa kina sana juu ya mipango kadha wa kadha tuliyonayo ya kuhakikisha barabara mbalimbali katika Taifa zinaendelea kujengwa, zinakamilika na zile mpya zinaenda kuanza pia vilevile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa hatua hii, na ninasema kwamba, Mheshimiwa Rais Samia aliidhinisha jumla ya fedha shilingi bilioni 840 kwa ajili ya kushughulika na mambo ya dharura peke yake nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdallah Ulega, Waziri wa Ujenzi kwa ufafanuzi. Namkaribisha Mheshimiwa Hussein Bashe, Waziri wa Kilimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na tutakuwa na Naibu Mawaziri wawili; Naibu Waziri - Sera, Bunge na Uratibu pamoja na Naibu Waziri - Kazi, Vijana na Ajira.

Karibu Mheshimiwa Bashe.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naanza na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai wa kufika siku ya leo na kuweza kushiriki shughuli hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, natumia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri, pia kwa *coordination* ya shughuli za Serikali na kwa namna anavyoweza kutuongoza kwa ajili ya kufikia malengo tuliyopewa na Ilani ya

Uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi pamoja na malengo na matamanio ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Waziri wa Kilimo, kwa kipindi chote nikiwa Naibu Waziri ninayeshuhulikia masuala ya ushirika wakati huo na nikiwa Waziri mwenye dhamana ya kilimo, namshukuru kwa dhati Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa *support* ambayo amekuwa akinipa mimi na kusaidia sekta ya ushirika kuweza kusimama na kufikia hapa ilipofika. Namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo ya Mheshimiwa Rais ilikuwa ni kwamba, lazima Tanzania tuwe na benki ya ushirika. Tarehe 28 mwezi huu Mheshimiwa Rais atazindua Benki ya Ushirika Tanzania, ambayo inaanza na mtaji wa shilingi bilioni 55 na itakuwa na matawi manne ambayo yatakuwa Mkoa wa Kilimanjaro, Mtwara, Tabora na Makao Makuu Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari benki hiyo imeshaanza pale ambapo lilikuwa jengo la ushirika. Mpaka kufika mwisho wa mwaka huu, tunaamini kwamba benki hii itakuwa na matawi nane na mawakala 36. Vilevile, vyama vyote vikuu vya ushirika vitakuwa ni mawakala wa Benki ya Ushirika ambao watafanya kazi ya kufungua akaunti za wakulima, *deposit* na *withdraw*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, benki hii kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais itakuwa ina dirisha maalumu la *guarantee scheme* na *equity fund* kwa ajili ya kuwasaidia wakulima ili waweze kuwekeza kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka niseme, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa dhati kwa sababu, unaweza ukawa na ilani na mipango, lakini pale ambapo kunakuwa hakuna *political will* kwenye ofisi kuu ya nchi, mambo mengi yanakuwa hayawezi kutokea. Namshukuru Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2021 wakati Mheshimiwa Rais anahutubia ndani ya Bunge hili, ukuaji wa sekta yetu ya kilimo ulikuwa ni 2.7% na bajeti ya kilimo ilikuwa shilingi bilioni 290. Mwaka 2024/2025 ukuaji wa sekta umefika 4.2% na bajeti imefika shilingi trilioni 1.2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyoongea, mauzo ya nje ya sekta ya kilimo; na ninapozungumzia kilimo sizungumzii kilimo kwa mapana, ninazungumzia kilimo mazao. Mwaka 2021 mauzo ya nje ya sekta ya kilimo yalikuwa ni wastani wa dola bilioni 1.2. mwaka 2024 tumefika dola bilioni 3.5, mauzo ya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Rais anahutubia Bunge hili, eneo la umwagiliaji ambalo limekuwa ni jambo kubwa sana leo, nami ninawaelewa sana matarajio mliyonayo Waheshimiwa Wabunge. Hatuwezi kukaa tunalalamikia mabadiliko ya tabianchi wakati Mwenyezi Mungu anatupatia maji, lakini tunashindwa kuyavuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ilikuwa ni shilingi bilioni 55, lakini leo bajeti yetu ni shilingi bilioni 400 lakini tunatekeleza miradi 780 ndani ya kipindi cha miaka mitatu. Leo hii mtandao wetu umetoka hekta 560,000 umefika hekta 970,000. Lengo la ilani ni hekta milioni 1.2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya upembuzi yakinifu wa mabwawa 100. Kati ya haya 100, mabwawa 27 tayari yana wakandarasi na kati ya haya 27, mabwawa 10 yako zaidi ya 80%. Hizi ni hatua ambazo Serikali hii imechukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki ndiyo inaongoza kuendesha skimu ya ruzuku kwa wakulima kuliko Serikali yoyote. Tunatumia karibu shilingi bilioni 300 kwa ajili ya wakulima wa mazao ya kawaida, kwa maana ya mazao 13 ya chakula ambayo yanatupatia *food security*. Nini matokeo yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2021/2022 uzalishaji wetu wa mahindi ulikuwa tani milioni sita. Msimu uliopita tumefika tani

milioni 12, tumekuwa ni nchi ya pili Afrika kwa uzalishaji wa mahindi. Tulikuwa tunazalisha wastani wa tani 1,200,000 mpaka 1,600,000 za mchele. Sasa tuko tani 3,500,000 za mchele. Sisi ndio *exporter* tunaoongoza katika Ukanda huu wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii imelia sana kuhusu mazao yanayoitwa ya biashara kwa maana ya korosho, pamba, tumbaku na kahawa. Leo tunavyoongea, sisi kama nchi mwaka 2024 kwenye zao la korosho kwa wastani kwa kipindi cha miaka mitatu, Serikali hii imetoa ruzuku ya zaidi ya shilingi bilioni 400 kwenye zao la korosho peke yake. Kwa kipindi cha miaka mitatu! Tumetoka wastani wa tani 180,000, leo tumefika tani 520,000 kwa msimu uliopita wa zao la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wastani wa bei ya mkulima kwa mara ya kwanza tumefikia kuuza zaidi ya shilingi 4,200/= wastani wa bei ya mkulima katika mfumo wa *TMX*. Vyama vyetu vya ushirika vimekusanya mazao na kuyauza kupitia Mfumo wa Stakabadhi ya Ghala na Ushirika kwa zaidi ya shilingi trilioni nne. Hili jambo halijawahi kufanyika katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulikuwa kwenye kundi linaloitwa *others* kwenye uzalishaji wa tumbaku. Yaani wanatajwa wa kwanza, wa pili, wa kumi, halafu sisi tumewekwa kwenye kundi la wengineo; lakini leo hii Tanzania ni nchi ya pili Afrika kwa uzalishaji wa zao la tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauzo yetu ya tumbaku yamefika zaidi ya dola milioni 400. Serikali hii inagawa ruzuku ya mbolea kwa wakulima wa kahawa pamoja na miche bure. Pia, kwa mwaka tunagawa zaidi ya miche milioni 22 kwa wakulima wa kahawa bure. Humu ndani ya Bunge wapo Waheshimiwa Wabunge ambao ni wakulima wa kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bei ya kahawa, kwa upande wa Kagera ilikuwa inanunuliwa kwa shilingi 700 mpaka shilingi 1,100. Msimu uliopita kahawa imefika zaidi ya shilingi 5,000 kwa wakulima katika Mkoa ya Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye tumbaku kulikuwa kuna madaraja 65, na kuna daraja linaitwa *reject* kwenye nchi hii. Yaani mkulima atalima, atavuna halafu inaitwa *reject*, inatupwa. Leo hakuna *reject* kwenye tumbaku. Leo mkulima aliyekuwa anapata Dola 0.5 kwa kilo, msimu umelioisha juzi Serengeti bei ya wastani ni Dola 2.5 kwa wakulima wa tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo moja ambalo nataka nilisemee kidogo. Kwa nini tunatoa ruzuku? Huu umekuwa mjadala na taasisi nyingine za Kimataifa zinatuonesha sisi kwetu ruzuku kwa wakulima ni *wastage of resources*, siyo sahihi. Ruzuku kwa wakulima ni njia mojawapo ya *stabilization* na kupunguza gharama ya uzalishaji. La pili, kama ambavyo Serikali inatoa ruzuku kujenga daraja au kutoa fedha kwenye kodi kujenga Barabara, ni sawasawa na kumsaidia mkulima, na ni sehemu ya *facilitation* kwenye shughuli za uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Rehema amesema hapa, kwa nini tunasainisha fomu? Nawaomba wakulima wa tumbaku, najua kilio cha ruzuku yenu. Serikali imeshatoa shilingi bilioni 13. Tunachokifanya ni kwenda kujiridhisha, huyu Hussein Mohamed Bashe wa Ulyankulu, hii akaunti ni ya kwake? Asaini mwenyewe kwamba hii akaunti ni ya kwake. Sasa mnataka tuzipeleke hizi fedha za wananchi mitaani bure?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho, niongelee wakulima wa miwa. Kumekuwa na kilio kwa wakulima na nimeshongea na ndugu yangu Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Bunge hili halijapitisha sheria ya kuwataka wakulima wa nchi hii wawe na *EFD receipts* na *EFD machine*. Hatukupitisha humu na haya siyo maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi, wala siyo maelekezo ya chama kilichoko madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotakiwa, vyombo vyetu vya ukusanyaji wa kodi viende vikakusanye kodi kwenye eneo la *formalization* ambako tumewataka *traders* wawe na *business license*. Anayenunua mazao, lazima awe na *TIN* na atatoa risiti ya

*EFD* na siyo mkulima wa kijijini kufuatwa na kuambiwa leta risiti ya *EFD*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitumie Bunge hili kuwatangazia wakulima, hamwajibiki kwenda kutafuta *EFD machine* kwa ajili ya ku-*produce* risiti za *EFD*. Hiyo siyo shughuli ya wakulima wala vyama vya ushirika. Hii siyo *genesis* ya sheria iliyopitishwa na Bunge hili. Tunamfahamu ambaye anatakiwa ku-*produce* risiti za *EFD*. Tushirikiane ku-*formalize* kwenye sekta ya kilimo kwa kuwarasimisha wafanyabiashara wawe na leseni, wawe na *TIN,* na waingie kwenye *tax base*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niingie *on record* ndani ya Bunge hili, kwamba tukifanya hivi, vyama vyote vya ushirika vitaacha ku-*formalize* na kuwa *aggregated,* na tutaua *aggregation system* tunayoijenga kwa jasho katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba *TRA* huko waliko wawaache wakulima wafanye kazi ya uzalishaji. Nendeni mkachukue kodi kwa *traders* ambao wanafanya biashara. Kipato cha mkulima ni kimoja tu kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Hussein Bashe, Waziri wa Kilimo kwa ufafanuzi. Tunaendelea na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia hoja iliyoko Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya, na kwa kweli Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweza kuivusha nchi katika kipindi ambacho dunia nzima ilikuwa inapita kwenye misukosuko. Ni kipindi ambacho

kimeambatana na misukosuko mingi kutokea katika *records* za masuala ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi matukio haya ya kimisukosuko huwa linatokea moja, linahangaikiwa hilo hilo, linapita, watu wanarejea, lakini kwa kipindi hiki cha miaka minne kumekuwa na misukosuko mfululizo ambayo ilikuwa ikitokea katika masuala ya kiuchumi, lakini jemedari wetu amesimama imara na nchi imevuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na *Covid* ambayo ilipiga nchi zote za dunia hii, tukavuka. Likaja suala la mzozo Mashariki mwa Ulaya ambao ulichangia gharama za maisha kupanda, tukavuka. Yakaja masuala ya uhaba wa fedha za kigeni na kwenyewe tumevuka, tumerudi katika hali ya kawaida. Hata sasa limekuja suala la sera za nje za baadhi ya Mataifa na lenyewe kama ambavyo Mheshimiwa Rais wetu ameweza kusimama kwenye masuala mengine na Taifa letu, likavuka na hili tayari Serikali imeshaanza kuchukua hatua, na ninawahakikishia Waheshimiwa Wabunge hata hilo tutavuka na tayari kazi imeshaanza kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilijitokeza hoja, na nianzie hapo hapo kwamba kuna baadhi ya Mataifa yamebadilisha sera zao ambazo zinahusisha kupunguza fedha katika mataifa yanayoendelea ikiwemo Tanzania. Sitataja kwa ajili ya mahusiano ya Kimataifa, lakini nadhani mmeshapata hayo Mataifa ambayo yamefanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawahakikishia, Serikali yetu tayari ilishafanya tathmini na tayari kazi hiyo ya tathmini imeshafanyika na ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Timu hiyo iliyosimamia kazi hiyo ilikuwa chini yake na tathmini ya sekta zote imeshafanyika na tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyoongea, tayari Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeshaanza kuchukua hatua. Kwa mfano, tulikuwa na mahitaji ya takribani shilingi bilioni 220 kwenye sekta ya afya kuweza kuziba

pengo ambalo limetokana na fedha zile ambazo tulitarajia kutoka kwa wenzetu ambao wamebadilisha sera yao na kupunguza fedha zinazokuja kwenye Mataifa haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyoongea, tayari Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeshatoa shilingi bilioni 98 kwenda kwenye afya, kuweza kufidia zile fedha ambazo zingepatikana kutoka kwa wadau, wenzetu wale ambao walikuwa wanachangia katika hiyo sekta. Tathmini hiyo inaendelea katika maeneo mengine, lakini pia na utoaji wa fedha utaendelea katika maeneo mengine yale ambayo yalikuwa yanahitaji fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Afya ndiyo iliyoguswa zaidi. Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa usimamizi wa shughuli za Serikali wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, imeendelea kutekeleza na tutaenda hatua zaidi ikiwemo kuwekeza fedha kwenye uzalishaji wa dawa zile ambazo tulikuwa tunapata kupitia wale wabia wetu, ziweze kuzalishwa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye mpango wa maendeleo utakaosomwa katika hili Bunge; na bajeti itakayosomwa katika Bunge hili, sehemu hiyo ya fedha itaelekezwa kwenye viwanda vinavyozalisha dawa ndani ya nchi ili tuweze kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu, umri wake, uwezo wake na uwekezaji uliofanyika kwenye afya tunaweza tukajitegemea kumaliza Malaria, tunaweza kujitegemea kwenye *TB*, tunaweza tukajitegemea kwenye vitendanishi, na tunaweza tukajitegemea katika madawa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari shilingi bilioni 98 zimeshakwenda na nyingine zitakwenda kwenye *MSD* ili kuweza kuhakikisha kwamba *MSD* inajitegemea, na hili jambo linaendelea. Fedha nyingine tutakaposoma Mpango na Bajeti, zitakwenda kwenye Bima ya Afya kwa Wote ili tuweze

kujitegemea katika Sekta ya Afya kama ambavyo Mheshimiwa Rais ametoa kwenye maelekezo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sekta nyingine ambazo zimeguswa, niwahakikishie Watanzania, hapatakuwa na sekta ambayo itakosa fedha eti kwa sababu kuna Taifa mojawapo limebadilisha sera ambalo lilitakiwa lisaidie Mataifa yanayoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumeshaingia uchumi wa kipato cha kati, na tunaendelea kusonga mbele tutoke uchumi wa kati wa chini, twende uchumi wa kati wa juu. Kwa hiyo, hakuna sekta itakosa fedha kwa sababu kuna Taifa limebadilisha sera yake ya kusaidia Mataifa yanayoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutatengeneza mkakati wa kubana matumizi, tuondoe matumizi kwenye maeneo ambayo yana uhitaji usio mkubwa sana, tupeleke fedha kwenye maeneo ambayo yana matumizi yenye ulazima ikiwemo miundombinu, afya, elimu, maji, umeme pamoja na sekta nyingine zote kwa ujumla ikiwemo sekta za uzalishaji. Tutafanya hivyo na kazi hiyo tayari imefanyika, timu ya wataalamu imeendelea kuyafanya hayo. Tutayafanya hayo na Taifa ni lazima lisonge mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imeshaingia kwenye kumbukumbu za kupanga jambo kubwa na kutekeleza. Moja, tulipanga kuhusu kutekeleza Mradi wa Umeme wa Mwalimu Nyerere. Tuliupanga ulikuwa mkubwa, ulikuwa unatisha, ulikuwa ndani ya misukosuko, lakini tumetekeleza na umekamilika na sasa unafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tulipanga kutekeleza Mradi wa Reli ya Kisasa kweli kweli ambayo hata Mataifa makubwa mengine hayana mradi kama huo, tumeutekeleza. Sasa hivi zaidi ya kilometa 722 kazi yake inaonekana, na sehemu kubwa imeshaanza kufanya kazi, Dar es Salaam mpaka hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi pande zote zilizosalia, zina wakandarasi, na makabidhiano ya fedha na utiaji saini tunamalizia hatua za mwisho, na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya vipande vyote vinavyosalia, ziko hatua ya mwisho. Kwa hiyo, kuanzia huu mwaka wa fedha, fedha zitaanza kumiminika katika hivyo vipande kwa uhakika ili kuweza kuhakikisha kwamba miradi hiyo inakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu lile daraja kubwa la kuunganisha sehemu moja ya nchi yetu na sehemu nyingine, Daraja la Kigongo – Busisi (Daraja la Magufuli). Tumepanga na tumetekeleza, limeshakamilika na leo hii Waziri akipita pale hahitaji Mabuti, anapita na suti yake, pameshakuwa tayari kwa ajili ya matumizi. Hii ni miradi mikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunatekeleza Bomba la Mafuta ambalo Tanzania imetekeleza wajibu wake, upande wake ambao unatakiwa utekelezwe kwenye hilo Bomba la Mafuta. Kwa hiyo, hii ni mifano kwamba hili ni Taifa linalojitegemea, lenye kiongozi makini na wasaidizi wake makini kama Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa na shughuli anazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa maeneo mawili yaliyotajwa, maji na barabara tumeongea na Mawaziri wa Kisekta. *TARURA* tumeongea na Mawaziri wa Kisekta. TAMISEMI, Kilimo, pamoja na sekta nyingine zote tumeshaongea na Mawaziri wa Kisekta. Tayari tumeshatoa fedha za *TARURA*, tumeshatoa fedha za maboma, tumeshatoa fedha za vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedgha zote tumeshazitoa na tutaendelea kutoa nyingine zinazotakiwa ili hiyo kazi yote ambayo Waheshimiwa Wabunge makini kabisa, Wawakilishi wa wananchi wa uhakika, wasio na mbambamba, mmesema humu ndani ya Bunge ili hizo fedha ziweze kufika na hiyo miradi iweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji huu unahitaji mapato, kwa hiyo, tutaongeza mapato. Tumekubaliana na Mamlaka ya Mapato kuongeza elimu kwa mlipakodi ili kuongeza *compliance*,

kulipakodi kwa hiari kama Mheshimiwa Rais alivyokuwa ameelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi juzi tulisaini Mkataba na Shirikisho la Mpira wa Miguu ili tutumie michezo kutangaza elimu ya mlipakodi. Tuna fungu letu ambalo huwa tunalitumia kwa elimu ya mlipakodi, tutalisambaza kuanzia michezo ya mashuleni, ili wanafunzi wale kuanzia wako shuleni; shule za msingi na sekondari waanze kujifunza uzalendo wa kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnakumbuka wakati tuko shule tulikuwa tunaimbishwa Kaburu Matata na tukamchukia kweli Kaburu. Hivyo hivyo, na uvamizi ule tuliuimba tukauchukia sana. Hata mlipakodi akiandaliwa hivyo kwamba kukwepa kodi ni jambo baya, watakapofika kuwa walipakodi, itakuwa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisaini mkataba na *Federation*, tutatumia ile. Tutavitumia vilabu vya Simba na Yanga, vina walipakodi wengi na wafuasi wengi. Sisi tunahitaji kodi, wao wana walipakodi, ili viweze kutusaidia katika kutoa elimu pamoja na michezo yote itumike katika kutoa masuala ya kuelimisha watu kulipa kodi kwa hiari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hata hivi sasa nawapongeza sana Simba, bado wana michezo ya Kimataifa, nawapongeze sana. Mimi siyo shabiki wa Simba, lakini ni kiongozi wa Simba. Nawapongeza sana Simba na ... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, muda wako umeisha. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana Simba kwa kuwa bado wana michezo, wao pamoja na Yanga waende Mamlaka ya Mapato Tanzania ili waendeleze ule mkataba tuliokubaliana wa kutumia mpira wa miguu kutangaza elimu ya mlipakodi, na hivi Simba wataenda kucheza *South Africa,* waweze kupata na fungu la kuweza kuhakikisha

wanaenda kuwatoa wale wenzetu kule, liwasaidie kuwatoa wale wenzetu kule ili waweze kuendelea kutangaza vizuri Taifa letu pamoja na hii kazi ambayo tunataka tutumie pia michezo kuweza kuelimisha walipakodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata taasisi nyingine zenye matangazo, mpeleke pale Simba, halafu wasaidiwe mafuta, waende kule, watatangaza hizo shughuli zenu ili waweze kuhakikisha wanapeperusha vyema bendera yetu. Tukirudi humu ndani nami nakuwa na sehemu ninazoshabikia, basi huko tutaongea tukiwa humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi/ Vicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, walikuwa wanaomba uwazungumzie na wale wengine, lakini muda hauruhusu. Utapata fursa wakati mwingine. *(Makofi)*

Tunaye Mheshimiwa Ummy Nderiananga, Naibu Waziri, Sera, Bunge na Uratibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Naomba nimshukuru Waziri wangu wa Nchi, Sera, Bunge na Uratibu kwa kunipa fursa ili nami niweze kuchangia bajeti yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nianze kwa kuungana na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kumpongeza Mheshimiwa Spika wa Bunge letu kwa umahiri wake na uchapakazi wake mkubwa ambao umeliwezesha Bunge letu kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mweyekiti, pia, tumemwona Mheshimiwa Spika duniani akiwakilisha nchi yetu na kutuletea heshima, pongezi sana kwake. Pia, nampongeza na Mheshimiwa Naibu Spika na ninyi Waheshimiwa Wenyeviti mnaomsaidia Mheshimiwa Spika kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati ya moyo wangu naomba sasa nimpongeze na kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake mahiri wenye kujali utu na pia kwa kuniamini mimi Ummy Nderiananga kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais na hii heshima kwangu ni jambo kubwa sana kwenye historia ya maisha yangu. Mheshimiwa Rais, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kukipongeza Chama chetu cha Mapinduzi kwa kumpa ridhaa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini na mgombea wake mwenza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi; na kwa upande wa Zanzibar, Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kazi za viongozi wetu. Nchi yetu imepata mafanikio makubwa chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kipindi cha miaka minne tu, Mheshimiwa Rais ameonyesha kazi kubwa sana na tumeona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuru Waheshimiwa Mawaziri mliochangia sekta mbalimbali, mmeonyesha namna Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa. Kwa hiyo, nawaomba Watanzania wote wanaotufuatilia, waendelee kumuunga mkono Mheshimiwa Rais, tumpe nafasi akafanye kazi nyingine kubwa zaidi kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunawaahidi viongozi wetu, tutaendelea kuwapa ushirikiano, na tutaendelea pia kuwaombea kura maeneo mbalimbali na Mwenyezi Mungu atawajaalia *Insha'Allah,* watashinda kwa kishindo mwezi wa Kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe pongezi kwa wasaidizi wanaomsaidia hii kazi nzuri Mheshimiwa Rais. Kwanza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango kwa uchapakazi wake imara na maelekezo yake ambayo yameendelea kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nampongeza pia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa uongozi imara na utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, naye tunampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naungana na Waheshimiwa Wabunge kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uchapakazi wake, umahiri wake, unyenyekevu na upole. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ofisini kwake Mheshimiwa Waziri Mkuu ameendelea kutupatia maelekezo na miongozo mbalimbali. Tunampongeza na sisi tunaofanya naye kazi, tunashuhudia kwamba yote Waheshimiwa Wabunge waliyokuwa wanayasema, ni kweli, nami binafsi nimeingia Ofisi ya Waziri Mkuu mwaka 2020. Mheshimiwa Waziri Mkuu amenilea vizuri, nimeweza kufanya kazi chini yake, nimejengeka kiuongozi na niko tayari na ninaendelea kulitumikia Taifa letu. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nampongeza Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Mashaka Doto Biteko kwa uongozi wake mahiri na kutuongoza vyema. Sambamba na utendaji kazi wake mzuri kwenye Wizara ya Nishati, tumemwona anavyochapa kazi, pamoja na maelekezo yake ambayo yamesaidia Ofisi yetu. Hata leo mnavyotuona, mkisemea vizuri Ofisi ya Waziri Mkuu, ni kwa sababu viongozi wetu hawa wapo na wanatuongoza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uniruhusu kwa dhati ya moyo wangu nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Sera, Bunge na Uratibu, Mheshimiwa William Lukuvi. Huyu ni *mentor* wetu, ni *senior*, ni mwalimu wetu, amekuwa kiongozi mahiri, mwenye upendo na mlezi. Binafsi nimepata bahati ya kufanya naye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lukuvi ni moja ya hazina pia ya uongozi kwa nchi yetu. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, ninakuombea afya njema, Mwenyezi Mungu aendelee kukubariki. Muda ukifika Mheshimiwa Waziri, basi Wanaismani waendelee kutupatia burudani kwa kukupa ushindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru Watendaji wetu. Katibu Mkuu Dkt. Jim James Yonazi; Naibu Katibu Mkuu, James Henry Kilabuko; Wakurugenzi wote na Wakuu wa Idara na Vitengo kwa kumsaidia kazi Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Sera, Bunge na Uratibu, Mheshimiwa William Lukuvi na kufanikisha utekelezaji mzuri wa majukumu ya ofisi yetu na bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na usimamizi na uratibu mzuri wa shughuli zote za Serikali. Tunawashukuru sana Watendaji wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uniruhusu niseme kwamba, mimi natokana na Jumuiya ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT). Naomba nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza viongozi wetu UWT kuanzia ngazi ya Taifa, Tanzania Bara na Zanzibar chini ya Mwenyekiti wetu mahiri, Mama Mary Chatanda na Makamu wake Mama Shomari; Katibu Mkuu, Dada Suzan Kunambi na Manaibu wao, wanawake wote wa UWT Mikoa, Wilaya, ngazi zote mpaka ngazi ya Mashina kwa kazi nzuri ambazo tumeendelea kushirikiana pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia kwa heshima mliyonipa binti yenu, na kwa kazi nzuri nyingi ambazo tumefanya pamoja katika maeneo mbalimbali kwa kipindi cha miaka mitano. Nawaomba kwa unyenyekevu mwendelee kuniunga mkono binti yenu muda utakapofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wetu wa Nchi, Sera, Bunge na Uratibu, naomba niwashukuru pia na ninyi Kamati. Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge, Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na wewe Mwenyekiti, Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano, ushauri na namna ambavyo mmeisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naishukuru Kamati yetu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI chini ya Mheshimiwa Mwenyekiti Elibariki Kingu na Wajumbe wote, tunawashukuru sana. Tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote, uchangiaji wao umetupatia faraja na msukumo wa kuendelea kumsaidia kazi Mheshimiwa Rais, ahsanteni sana, Mungu awabariki. Pia, nawashukuru Waheshimiwa Naibu Mawaziri na Mawaziri wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu hoja chache, nyingine Mheshimiwa Waziri wangu atakuja kuzimalizia. Kwanza ni kufikia malengo ya kidunia kupambana na UKIMWI hadi mwaka 2030, Serikali tunajipangaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ya utangulizi ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ambayo yametuwekea msingi wa kuonyesha kwamba nchi yetu hakuna litakaloshindikana, tutaenda vizuri. Kulikuwa kuna maneno hapa katikati kwamba sasa UKIMWI watu hivi na vile, lakini tunaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia tuliandaa mpango wa uendelevu na uhimilivu wa kupambana na UKIMWI. Mpango huu tuliuzindua mwaka 2024 kwenye Siku ya UKIMWI kule Ruvuma na Mheshimiwa Makamu wa Rais ndiye aliyetuzindulia mpango ambao kidunia wanaita, *sustainability roadmap* ambayo lazima kila nchi itengeneze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi Tanzania tumefanya vizuri, tumeshauandaa, lakini tumeona mwelekeo mzuri. Wadau sasa wanaendelea kujitokeza kutuunga mkono kwenye hili eneo. Mheshimiwa Waziri wetu ameendelea kuturatibu na kutuambia hata kwenye mapambano dhidi ya Virusi vya UKIMWI, mambo mengine ambayo siyo ya lazima tuyaahirishe, tufanye yale ambayo ni ya ulazima zaidi ili tuendelee kuhakikisha kwamba tunabana matumizi, lakini tunaenda vizuri. Kwa hiyo, nawahakikishia kwamba, kufikia 2030 nchi yetu tutakuwa tuko vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko hoja ya kuendelea kuwapatia dawa wafungwa walioko Magerezani. Tunaendelea vizuri na nakushukuru wewe na Kamati yako, tumeendelea kutembelea maeneo mbalimbali kuona afua za UKIMWI zinavyotekelezwa Magerezani. Hakuna mfungwa atakayekosa dawa chini ya Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, tutaendelea kuwapa dawa, kuwapa huduma za kinga, kuwapa lishe na kadhalika ili waendelee vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la ufuatiliaji wa miradi mikubwa ya kimkakati, tumeambiwa kufanya mambo ya *monitoring and evaluation*. Ofisi yetu chini ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi tumeendelea kufanya vizuri na ndiyo maana leo tunaripoti. Mheshimiwa Waziri Mkuu anasema, miradi imekamilika, reli ya *SGR* (Dar es Salaam – Dodoma) wote tumepanda tumeona. Pia, Mji wa Serikali tumefika 89%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tunaendelea kumalizia mfumo wetu wa ufuatiliaji na tathmini chini ya Mheshimiwa Waziri wa Sera, Bunge na Uratibu pamoja na *e-GA* ili kuwa na kitu kikubwa zaidi kitakachotuongoza kama nchi kwenye mambo ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, hapa hapa kwenye *monitoring and evaluation,* tunakuja na *application* maalum. Tunatengeneza mfumo ambao utaitwa *Kiongozi App*, ambao utawafanya Waheshimiwa Mawaziri, Makatibu Wakuu, viongozi wote ndani ya Serikali kuweza kusomana na kuwa na *information* kiganjani wawe na taarifa. Unapoongelea mradi fulani, umefikia asilimia ngapi, tutakuja na hiyo na tunamshukuru Mheshimiwa Waziri wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, nawashukuru sana, Mwenyezi Mungu atubariki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ummy Nderiananga ahsante sana kwa mchango na kujibu hoja za Waheshimiwa

Wabunge. Sasa ni zamu ya Naibu Waziri, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Mheshimiwa Patrobass Katambi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa fursa ambayo umenipatia. Niungane na wenzangu kumpongeza sana, sana, sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi yake nzuri ambayo ameifanya ya mapinduzi makubwa na maendeleo makubwa ambayo ameipatia nchi yetu katika sekta zote. Tunashuhudia, vitu hivi vimefanyika kwa kipindi cha muda mfupi sana wa kipindi cha miaka minne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza kwangu, namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kuturuzuku uhai, lakini pia kutuwezesha kufanya kazi kwa umahiri katika kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa imani yake kubwa ambayo ameiweka kwangu katika kipindi hiki ambacho ameniteua kuweza kumsaidia kuhudumu katika Ofisi ya Waziri Mkuu katika eneo la Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazidi kumshukuru Mheshimiwa Rais, lakini pia tunampongeza, kwani amekuwa ni kiongozi shupavu, mahiri, na ni Rais ambaye ameonyesha busara kubwa sana katika kuamua na kufanya maamuzi yake. Pia, ni Rais ambaye ameonyesha uwezo mkubwa wa uvumilivu na weledi. Vivyo hivyo ni Rais ambaye amekuwa na mapenzi makubwa sana kwa Watanzania bila kuwabagua na amepeleka maendeleo katika kila kona ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hatuna budi, na hatuna cha kumpa zaidi ya kumwombea sana kwa Mwenyezi Mungu ampe afya njema, umri, riziki na uwezo wa kuendelea kulihudumia Taifa letu, nasi tuzidi kumwombea na kumpigia kura nyingi sana katika uchaguzi ujao kwa ajili ya mafanikio ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili naomba nichukue fursa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango ambaye ni Makamu wa Rais wetu kwa huduma nzuri anayoifanya kwa ajili ya Taifa hili na kumsaidia Mheshimiwa Rais. Sambamba naye yupo Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye sisi ndio Kiongozi wetu katika Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kweli ni kiongozi wa mfano wa aina yake. Ni mpole, mpenda watu, sijawahi kumwona amekasirika katika kipindi changu chote cha miaka minne ya kufanya kazi ofisini, lakini zaidi hata pale ilipotokea hali ambayo ina tafrani, amekuwa na utulivu lakini alilenga zaidi katika kutafuta suluhu kuliko kuongeza tatizo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kustahimili maelekezo yake na uongozi wake bora katika ofisi hiyo Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kweli huna baya mbinguni na duniani tunayaona. Mungu akubariki sana, na sisi tutaendelea kuwa nawe katika kuhakikisha tunakusaidia katika majukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameambukiza pia wema na upendo, lakini pia uchapakazi umemwambukiza msaidizi wake Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati ambaye naye pia kwa wema wake na maelekezo yao kwa pamoja wametusaidia sana katika kufanya kazi hizi kwa ubora na viwango ambavyo vinatakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wapo viongozi wetu Mheshimiwa Waziri Mzee Lukuvi, lakini pia yupo Mheshimiwa Ridhiwani. Hawa viongozi nao wanaambukizana wema, Mheshimiwa Lukuvi kwa kweli tangu nimfahamu amekuwa msaada mkubwa sana kwetu sisi vijana na kuiga aina ya uongozi kwake, vivyo hivyo katika maelekezo ambayo amekuwa akiyatoa amefanya kazi kubwa na nzuri nasi kwa kweli tunakushukuru Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yupo Mheshimiwa Waziri wangu Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, wananchi wa Chalinze tunawashukuru sana kwa kweli, sisi tunasema tumelamba dume, kwani wametuletea kiongozi huyu kijana shupavu ambaye sisi tunamwita kaka mkubwa ofisini, amekuwa mchapakazi, amekuwa kiongozi bora, mzuri lakini ni muungwana sana. Huyu mzee naye pia ni kama vile anaambukizwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kila wakati ana-*smile,* sijawahi kuona amechukia na anarahisisha sana kazi kwa kweli. Katika ofisi yetu ameweza kufanya kazi vizuri na amekuwa pia akitoa miongozo na maelekezo inayopelekea kupata mafanikio katika ofisi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri weledi wake, maarifa, ujuzi na ubobevu wake kwenye maeneo mbalimbali. Mimi hapa mdogo wake huwa nateleza tu kwenye majukumu, kwa sababu njia anazonionyesha ni sahihi na tunafanya kazi kwa ukamilifu zaidi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia ofisi yetu, Makatibu Wakuu, Ndugu Jim Yonazi lakini Mama yetu Mary Maganga pamoja na Naibu Katibu Mkuu Zuhura Yunus na viongozi wengine ambao wapo kwenye hii ofisi. Mama huyu ni shupavu, mwenye weledi mkubwa, ameongoza vizuri ofisi hii na ametusaidia sana katika kufikia mafanikio haya na ni mtu wa *facts and figures* na wakati wote ameongoza Ofisi ya Waziri Mkuu katika mafanikio kwa kutekeleza maelekezo na maagizo mahususi ambayo yanatolewa na viongozi wetu hawa wa juu ambao nimewataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia viongozi katika Mifuko yetu ya Hifadhi ya jamii ambayo wamekuwa wakisimamia vizuri sana Wakurugenzi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii *NSSSF, PSSSF, WCF, OSHA, CMA* na taasisi nyingine zote zilizo chini ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa kweli uwezo wao ni mkubwa, wamekuwa mahiri na hii inathibitisha uteuzi wa Mheshimiwa Rais, ni wa jicho la mwewe lisilokosea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwapongeze sana kwa kweli viongozi hawa, wamekuwa wakifanya kazi kubwa. Pia, Wakuu wa

Idara na Taasisi na Vitengo chini ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Spika wetu Dkt. Tulia Ackson. Daktari huyu mahiri, mmbobevu wa Sheria na Mzamivu kwenye maeneo mengi ya kiutawala na uongozi, amekuwa kiongozi wa mfano siyo tu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, bali pia ndiye Rais wa Mabunge yote Duniani ambayo kazi yake ameifanya kwa umahiri mkubwa. Sisi tunaiga wema wake, lakini pia umahiri wake katika kufanya kazi hii. Vivyo hivyo Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii Mheshimiwa Mama Fatma Toufiq pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote kwa miongozo yao na shughuli kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya. Kwa sababu ya muda natambua, lakini pia nashukuru upande wa Chama cha Mapinduzi, hapa tunao Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya ya Shinyanga Mjini. Hawa ndio zao, mimi ni mtoto wao na tunda, nimetokana nao, nawashukuru sana kwa kunifikisha hapa. Nashukuru familia yangu kama ilivyotajwa, lakini kwa sababu ya muda, naona nina hoja ambazo napaswa kuzijibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye hoja kwa haraka na kwa sababu ya muda, naomba hotuba yangu au maelezo yangu ya kujibu hoja kama jinsi ambavyo tumewasilisha yote yaingie katika Kumbukumbu za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja ya kwanza ilihusu zaidi kuhusu Serikali itoe vitendea kazi kwa vijana wanaomaliza mafunzo ya uanagenzi. Serikali imekwishafanya hivyo na tutaendelea kufanya hivyo. Tumeshatoa tayari vifaa vyenye thamani ya shilingi 1,000,900,000 ambavyo vimeenda kununua vifaa hivi vilivyonufaisha vikundi zaidi ya 2,700, ambapo vijana 1,977 wamekuwa wanufaika. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/2026 tunatarajia kupata fedha tena shilingi milioni 637

ambazo zitaenda kuwasaidia vijana ambao wanafuzu mafunzo haya ya uanagenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilihusiana na programu ya ukuzaji ujuzi katika programu hii. Hoja ilikuwa inasema, tutoe elimu. Tunayo furaha Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na maelekezo ya utekelezaji wa Mheshimiwa Waziri Mkuu tumeendelea kutoa elimu katika vyombo vya habari kupitia *platform* zote za *media* na *social media* na matangazo yamekuwa yakifanyika na tumekuwa tukitenga fedha zaidi shilingi 138.1 kwa ajili ya utoaji wa elimu kwa umma na pia zaidi kutoa taarifa ya mafunzo haya yanayofanyika chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa kuna hoja ya Serikali iongeze vyuo vya mafunzo ya uanagenzi. Moja ya hatua ambazo Serikali imefanya ni pamoja na kuongeza Vyuo vya *VETA* ambavyo vinatumika nchini kote, vinajengwa katika Halmashauri zetu za Wilaya, lakini hivyo hivyo vyuo vya maendeleo ya jamii tayari vimeshajengwa na vinafanyiwa maboresho hata pale kwangu Shinyanga tulipata shilingi milioni 650 kwa ajili ya maboresho ya chuo chetu cha maendeleo ya jamii. Vyuo binafsi navyo pia vimekuwa ni sehemu ya kuhakikisha kwamba mpango huu wa Serikali unatimizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika upande wa pili wa mafunzo mwaka wa fedha 2025/2026 tutaenda kuwafikia zaidi ya wanafunzi 8,000 ambao wataenda kwenye vyuo 52 hapa nchini kwa ajili ya kupata mafunzo katika Wilaya 48. Hii ni hatua kubwa ambayo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kuonyesha. Pia katika maeneo mengine kwa haraka nikienda hata masuala ya ajira kwa ujumla, kwenye masuala ya ajira ni mjumuiko, ni pamoja na mpango wa utoaji wa mikopo, ajira za vijana zimeendelea kutolewa katika sekta ya umma hata katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya upanuzi wa maeneo mengi ya ajira, kwa mfano, uwekezaji umeongezwa nchini na kufanya maboresho ya sheria ili kuvutia uwekezaji; na kufanya

maboresho ya sheria ya kuratibu ajira za wageni. Pia katika hatua nyingine katika eneo hilo kwenye suala la ajira tumeendelea kufanya na kukuza maeneo mbalimbali, kutenga maeneo ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetenga maeneo ya kuzalisha na kuuza bidhaa ndani na nje ya nchi, lakini pia punguzo la tozo kwenye maeneo ya baishara yanayoweza kutoa ajira zaidi, tumefanya kwenye maeneo ya mikopo ukiacha 4:4:2 zinazotolewa na Halmashauri zote nchini, tumeenda kwenye hatua nyingine ya kila Wizara ya Kisekta kwa maagizo ya Mheshimiwa Rais na maelekezo ya utekelezaji ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhakikisha kila Wizara inazalisha ajira nchini, kuweza kuhakikisha kwamba katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Wizara ya Miundombinu kwenye ujenzi kote unapofanyika hata maeneo yale ya miradi ya mkakati; Bwawa la Mwalimu Nyerere, *SGR* huko tulipata ajira na mafanikio, tulipata ajira zaidi ya milioni 8,084,000 zaidi hata ya lile takwa la ilani ambalo lilikuwa linahitajika kwamba tupate ajira milioni nane. Haya ni mapinduzi makubwa ambayo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya kilimo, tunao mpango wa *Building a Better Tomorrow* ambapo vijana wanapata mafunzo na tunawapa maeneo maalumu kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu inaratibu. Wizara ya Bashe inafanya kazi hiyo, Wizara ya Madini napo pia tunatoa mafunzo kwa wachimbaji na pia tunawakopesha vifaa ambavyo vinawasaidia kwenye mpango wa *Mining for Brighter Tomorrow* kupitia Mheshimiwa Antony Mavunde Waziri mwenye dhamana husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, zaidi ya shilingi bilioni 10 zilitolewa kwa ajili ya kuwasaidia vijana hao, na pia boti zilitolewa na Mheshimiwa Rais zaidi ya 100, ufugaji wa samaki kupitia vizimba, lakini pia unenepeshaji mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara nyingine ambayo inafanya kazi hiyo, hata Wizara ya Michezo, ili kuongeza wigo wa ajira. Tunatambua michezo inaajiri zaidi, Mheshimiwa Rais anajenga viwanja karibia nchi nzima kwenye maeneo yale ambayo ni ya kimkakati. Arusha unajengwa uwanja utakaobeba zaidi ya watu 22,000. Pia ameanza kutoa fedha, ukiacha zile za Kapu la Mama, kuna fedha zaidi ya shilingi bilioni tano zinatolewa kwa ajili ya ukopeshaji wasanii na watu wengine ili kutoa fursa za vijana hao kwenye hayo maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna thamani ya fedha zaidi ya shilingi trilioni 2.7 zilitolewa kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ulionufaisha wananchi zaidi ya milioni 24 ikiwa ni kuwawezesha walio kwenye biashara na kwenye maeneo ya kukuza mitaji, na pia kuongeza fursa mbalimbali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kwenye masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo napo pia huko ni uwezeshaji wa vijana. Zaidi ya shilingi bilioni 788 zinatolewa Wizara ya Elimu kwa ajili ya kuwasaidia vijana ambao wapo kwenye mfuko wa mpango wa elimu. Pia kuna Samia *Scholarship* zinatolewa yoyote ambaye atafanya vizuri kwenye masomo ya sayansi. Mheshimiwa Rais ameweka mpango wa kuwafadhili bure ili vijana wetu waweze kusoma na kujipatia ajira ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kwenye ajira, tumefanya. Mheshimiwa Waziri wangu, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete ana mpango wa kuingia mikataba na nchi zaidi ya nane ya kupata ajira katika maeneo na Mataifa mbalimbali na tumeanza, mfano na nchi tatu; nchi za Uarabuni na Qatar na maeneo mengine ambapo zaidi ya vijana 500 wameshakwenda kwenye hatua ya kwanza ikiwa ni pamoja na mjumuisho wa mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi, muda ni mchache, lakini tunatambua haya yote yamewezekana kwa sababu wapo watendaji wenye dhamira safi. Mheshimiwa Rais

amekuwa akifanya hivyo na kuhakikisha anatuelekeza katika kuwahudumia Watanzania bila ajizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nizidi kushukuru nafasi yako wewe binafsi, na pia tuzidi kushukuru kwamba Mheshimiwa Rais ajenda za uchaguzi anazo kwa sababu amegusa maisha ya Watanzania, na pia yeye mwenyewe ni mgombea mahiri ambaye hana mshindani hapa nchini, ameji-*organize* vizuri kupitia Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo Mheshimiwa Rais ana-*communication strategy* za maana za kushinda uchaguzi; tatu, ana rasilimali mali za kusaidia kushinda uchaguzi; na nne, ana rasilimali watu ambao wanaweza, sisi tuweze kushinda uchaguzi. Wale majirani zetu kule ni nyumba ya njaa. Ukiona nyumba haina hata paka, ujue kuna njaa. Tuwape pole, na tutawashinda katika uchaguzi ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja na Mheshimiwa Rais tumpe kura za ndiyo, ndiyo. Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

**MAELEZO YA MHESHIMIWA PATROBASS PASCHAL KATAMBI, (MB) NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU - KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU, AKITOA UFAFANUZI WA MICHANGO YA WAHESHIMIWA WABUNGE KATIKA KUHITIMISHA HOJA YA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote ninapenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu siku hii ya leo.

***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa heshima aliyonipa na kuwa na imani kubwa na utendaji wangu katika kuhudumu kwenye nafasi hii ya Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Kazi,

Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Kwa namna ya kipekee ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza miaka minne tangu ashike nafasi ya kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nami niungane na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu kumuombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa nguvu, ulinzi, afya na kila lililo la heri katika kuwatumikia Watanzania.

***Mheshimiwa Spika,*** pia ninamshukuru sana Mhe. Dkt Philip Isdor Mpango - Makamu wa Rais, pamoja na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu kwa miongozo yao, ambayo imetusaidia katika kutimiza majukumu katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Miongozo yao thabiti inayoendana na Dira ya Taifa 2025, Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano (2021/2022 – 2025/2026) pamoja na Mwelekeo wa Serikali kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020 imenijengea uwezo mimi pamoja na watendaji wengine wanaoshughulikia masuala ya Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, kuandaa mipango na mikakati bora.

***Mheshimiwa Spika,*** kipekee, nikupongeze wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge hili Tukufu kwa umahiri na weledi mkubwa. Aidha, niwapongeze Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kukusaidia kikamilifu katika kutekeleza majukumu ya kuliongoza Bunge letu Tukufu. Aidha, ninawapongeza pia, Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

***Mheshimiwa Spika,*** kipekee kabisa, ninaomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete (Mb), kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu). Hakika uongozi na ushirikiano wako kwangu umekuwa msingi mkubwa sana katika kuwahudumia watanzania wote kwenye masuala ya Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu.

***Mheshimiwa Spika*****,** vilevile, ninawashukuru sana Bi. Mary Ngelela Maganga, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu); Bi. Zuhura Yunus, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu); Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na wafanyakazi wote kwa ushirikiano mkubwa wanaoonipatia wakati nikitekeleza majukumu yangu.

***Mheshimiwa Spika*****,** Nimalizie shukurani zangu za mwisho lakini si kwa umuhimu, Kipekee kabisa ninaomba niwashukuru Familia yangu Pamoja na wananchi wangu wa jimbo la Shinyanga Mjini kwa kuniamini na kunipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu.

***Mheshimiwa Spika*****,** ninaomba sasa nijielekeze katika kutoa ufafanuzi wa hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, kwa njia ya maandishi na zile zilizotolewa kwa njia ya mdomo, pamoja na hoja za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya masuala ya ustawi na maendeleo ya jamii.

**A: KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII**

1. **HOJA:** Serikali itoe vitendea kazi kwa vijana wanaonufaika na programu ya uanagenzi mara baada ya kuhitimu.

**MTOA HOJA:** Mhe. Fatma H.Toufiq (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii.

**UFAFANUZI WA HOJA:** Kwa kipindi cha mwaka 2022 hadi mwaka 2024/25 Serikali imetoa vitendea kazi vyenye jumla ya Shilingi 1,091,936,358 kwa vikundi 270 vyenye idadi ya vijana 1,977 waliohitimu mafunzo ya uanagenzi. Vilevile, Serikali katika mwaka 2025/26 itaendelea kutenga Shilingi 637,000,000/= kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mtaji.

2. **HOJA:** Serikali ihakikishe inamrahisishia Mwananchi kupata taarifa kuhusu Programu ya Ukuzaji Ujuzi.

**MTOA HOJA:** Mhe. Fatma H. Toufiq (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii.

**UFAFANUZI WA HOJA:** Serikali inaendelea kutoa taarifa kwa Wananchi kwa lengo la kujenga uelewa kuhusu programu ya kukuza ujuzi kupitia Vyombo vya habari, Mitandao ya kijamii, Maonesho, Matangazo ya redio, Televisheni na Magazeti. Kwa mwaka wa fedha 2025/26 Serikali itaendelea kutenga bajeti kiasi cha shilingi milioni mia moja thelathini na nane, laki moja (138, 100,000/=) kwa ajili ya kutoa taarifa na elimu kwa wananchi.

**3. HOJA:** Serikali iongeze idadi ya vyuo vinavyotoa mafunzo kwa njia ya uanagenzi hadi katika ngazi ya Wilaya.

**MTOA HOJA:** Mhe. Fatma H. Toufiq (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii.

**UFAFANUZI WA HOJA:** Serikali imekuwa ikitoa mafunzo ya uanagenzi kupitia vyuo vya VETA, vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs), vyuo Binafsi na vyuo vya Mashirika ya Dini kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Taifa kwa kuzingatia vigezo na sifa zinazohitajika. Katika Mwaka wa Fedha 2024/25, mafunzo hayo yanatolewa kwa vijana 8,000 katika vyuo 52 kwenye Wilaya 48. Serikali itaendelea kuvikagua vyuo vinavyotaka kutekeleza programu hizi na vikikidhi viwango vitaingizwa katika orodha takiwa.

**B. USIMAMIZI NA VIWANGO VYA KAZI**

**4. HOJA:** Serikali iboreshe maslahi kwa wafanyakazi wa sekta binafsi kwa kuwa maslahi yao ni duni.

**MTOA HOJA:** Mhe. CPA. Japhet Ngailonga Hasunga – (Mb. Vwawa)

**UFAFANUZI WA HOJA:** Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kuboresha maslahi ya Wafanyakazi wa Sekta Binafsi nchini. Mwaka 2023 kupitia Tangazo la Serikali Na. 687 la tarehe 25 Novemba, 2022 Serikali iliboresha Kima cha Chini cha Mshahara katika Sekta 13. Aidha, mwezi Februari, 2025 marekebisho ya Sheria za Kazi yalifanyika na kupitishwa na Bunge.

Vile vile, Serikali inaendelea kufanya utafiti wa Kima kipya cha Chini cha Mshahara katika Sekta Binafsi ambao unatarajiwa kukamilika Mwaka wa Fedha 2025/26. Sambamba na hatua hizo, Serikali inaendelea kuhimiza majadiliano ya pamoja baina ya Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri Mahali pa Kazi ili kufunga Mikataba ya Hali Bora ya Kazi na kuweka Sera ambazo zinaboresha Viwango vya Chini vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria.

5. **HOJA:** Serikali kusimamia na kudhibiti utoaji wa vibali kwa raia wa kigeni ambao hawana vigezo vya kufanya kazi ambazo zingeweza kufanywa na wazawa.

**MTOA HOJA**: Mhe. Sylvia Francis Sigula - (Mb. Viti Maalum).

**UFAFANUZI WA HOJA:** Serikali inaendelea kusimamia na kudhibiti ajira kwa raia wa kigeni na kuwapa fursa wazawa ambapo katika kushughulikia maombi ya vibali hivyo, Serikali huzingatia vigezo vilivyoanishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Ajira za Wageni Sura 436. Kwa mwaka 2024/25 vibali vya kazi 160 vimekataliwa.

6. **HOJA:** Serikali ieleze hatua ilizochukua katika kusimamia ajira za raia wa kigeni wanaofanya kazi nchini.

**MTOA HOJA:** Mhe. Nusrat Shaaban Hanje – (Viti Maalum)

**UFAFANUZI WA HOJA:** Serikali imeendelea kuhakikisha uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Ajira za Wageni Sura 436 kwa kuchukua hatua mbalimbali ambazo ni pamoja na:-

i. Kufanya kaguzi maalum zinazoshirikisha mamlaka nyingine za Serikali ikiwemo Idara ya Uhamiaji, pamoja na kaguzi za kawaida zinaendelea kufanyika ili

kuhakikisha uzingatiaji wa Sheria za Kazi na kuchukua hatua stahiki endapo itabainika kuwepo kwa ukiukwaji wa Sheria; na

ii. Utoaji wa elimu kwa Waajiri, Wafanyakazi na wadau wengine umeendelea kuimarishwa ili kuwawezesha kuzifahamu Sheria hizo na kuzizingatia ipasavyo.

**C. HUDUMA ZA AJIRA NA UKUZAJI UJUZI**

**7. HOJA**: Ni upi mkakati wa Serikali katika kuwezesha fursa za ajira nchini?

**MTOA HOJA:** Mhe. Joseph Michael Mkundi – (Mb. Ukerewe) na Mhe. Michael Mwita Kembaki - (Mb. Tarime Mjini)

**UFAFANUZI WA HOJA:** Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali kuhakikisha mazingira wezeshi kwa sekta binafsi ili kuzalisha ajira zaidi kama ifuatavyo:

i. Kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya uwekezaji katika mikoa yote (SEZ);
ii. Kutenga maeneo kwa ajili ya kuzalisha na kuuza nje (EPZ);
iii. Kuweka vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi kuvutia uwekezaji na mitaji ya moja kwa moja (FDI);
iv. Kupunguza tozo mbalimbali na taratibu zinazochukua muda mrefu;
v. Kuwezesha sekta binafsi kupata mikopo na rasilimali fedha kwa urahisi;
vi. Kuboresha miundombinu kama umeme, maji, barabara, vivuko, bandari, reli na mawasiliano ili kuwezesha biashara kufanya kazi kwa ufanisi;
vii. Kuwekeza katika elimu na mafunzo ya kukuza ujuzi ili kuwa na nguvu kazi inayohitajika katika soko la ajira; na
viii. Kuwezesha sekta binafsi kupata masoko ya ndani na nje.

**D. MAENDELEO YA VIJANA**

8. **HOJA:** Serikali itumie kambi ya Vijana ya Sasanda yenye ukubwa wa ekari 700 kwa ajili ya kuwaandaa vijana ili washiriki katika shughuli za kiuchumi.

**MTOA HOJA:** Mhe. CPA. Japhet Ngailonga Hasunga – (Mb. Vwawa).

**UFAFANUZI WA HOJA:** Serikali itaendelea kutumia kituo cha Vijana cha Sasanda kwa ajili ya kuendeleza programu za mafunzo ya vitendo ya muda mfupi ili kuwawezesha Vijana kushiriki shughuli za kiuchumi. Aidha, kwa sasa eneo la kituo hicho linatumika kama shamba darasa kwa ajili ya mafunzo ya kilimo kwa vijana; utunzaji wa mazingira kwa kupanda miti; na ufugaji wa samaki na nyuki.

9. **HOJA:** Serikali inashauriwa kutoa mafunzo kwa vijana wanaotarajiwa kupewa mikopo ili waweze kunufaika na mikopo hiyo kuwa endelevu kwa kuiga utaratibu wa Mfuko wa Wafanyabiashara Wadogo -NEDF.

**MTOA HOJA**: Mhe. Charles John Mwijage – (Mb. Muleba Kaskazini).

**UFAFANUZI WA HOJA:** Serikali itaendelea kutoa mafunzo kwa vijana wanaotarajiwa kupewa mikopo kuhusu usimamizi wa fedha, huduma za biashara na ujasiriamali ili waweze kutimiza malengo yao.

10. **HOJA:** Serikali itoe elimu katika ngazi mbalimbali kwa wananchi kuhusu mikopo inayotolewa na Serikali pamoja na fursa mbalimbali zinazotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa lengo la kuwaongezea uelewa.

**MTOA HOJA**: Mhe. Zacharia Paul Isaay – (Mb. Mbulu Mjini); Mhe. Sebastian Saimon Kapufi – (Mb. Mpanda Mjini); Mhe. Neema Gerald Mwandabila – (Viti Maalum) na Mhe. Sylvia Francis Sigula - (Mb. Viti Maalum)

**UFAFANUZI WA HOJA:** Serikali itaendelea kutoa elimu kwa vijana kwa lengo la kujenga uelewa kuhusu fursa mbalimbali zinazotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu ikiwemo programu ya kukuza ujuzi na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kupitia Vyombo vya habari, Mitandao ya kijamii, Maonesho, Matangazo ya redio, Televisheni na Magazeti. Kwa mwaka wa fedha 2025/26 Serikali itaendelea kutenga Shilingi 138,100,000/= kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi.

**11.** **HOJA:** Serikali iwezeshe vijana kuunda vikundi na kuwapatia mikopo wahitimu wa Vyuo Vikuu ili waweze kutumia ujuzi walioupata na hivyo kuzalisha fursa za ajira kwa vijana wengi zaidi.

**MTOA HOJA:** Mhe. Janejelly Ntate James– (Mb. Viti Maalum)

**UFAFANUZI WA HOJA:** Serikali imeweka mifumo ya kusajili na kutambua vikundi, makampuni na taasisi za vijana wakiwemo wahitimu wa vyuo vikuu. Baada ya kuunda vikundi na kutambuliwa, vijana hao wanakuwa na sifa ya kuomba mikopo kupitia mifuko mbalimbali ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. Kwa mwaka 2024/25 vikundi vya vijana 2,827 vilianzishwa na mikopo yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 36.64 imetolewa.

**12.** **HOJA:** Serikali itoe fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambazo zilipangwa kutolewa katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**MTOA HOJA:** Mhe. Riziki Said Lulida – (Mb. Viti Maalum)

**UFAFANUZI WA HOJA:** Katika mwaka wa fedha 2024/25 kiasi cha Shilingi 657,252,868 kimetengwa kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya vijana. Aidha, Serikali itahakikisha fedha hizo zinatolewa kabla ya mwaka wa fedha 2024/25 kumalizika.

**13. HOJA:** Serikali iangalie upya na kuongeza fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili kuweza kuwafikia vijana wengi zaidi.

**MTOA HOJA:** Mhe. Fatma Hassan Tofiq – (Mb. Viti Maalum)

**UFAFANUZI WA HOJA:** Katika mwaka wa fedha 2024/25 kiasi cha Shilingi 657,252,868 kimetengwa kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili kuweza kuwafikia vijana wengi zaidi. Aidha, Serikali katika mwaka 2025/26 itaendelea kutenga Shilingi 1,000,000,000 kwa ajili ya mfuko.

**E: HIFADHI YA JAMII**

**14. HOJA:** Serikali ihakikishe Mifumo ya TEHAMA ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii isomane na Mifumo ya Ajira na Utumishi ili kuongeza usahihi wa taarifa za wanachama kwa lengo la kutatua changamoto ya ucheleweshwaji wa michango na ulipaji wa mafao.

**MTOA HOJA:** Mhe. Ally Hassan Omar King – (Mb. Jang'ombe).

**UFAFANUZI WA HOJA:** Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu ya kuwa, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imeshaanza kuoanisha mifumo ya TEHAMA ya ndani na Mifumo ya Ajira na Utumishi na ipo katika hatua mbalimbali za majaribio. Mifumo hiyo ni pamoja na e-watumishi (Human Capital Management Information System-HCMIS) na mfumo wa PSSSF unaoitwa Members Administration system (MAS). Mifumo hiyo inatarajiwa kuanza kutumika ifikapo mwezi Julai, 2025 ili kuongeza ufanisi wa kutoa huduma kwa wanachama.

**15. HOJA:** Serikali kupitia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iendelee kuwekeza sehemu zenye tija zaidi ili kupata faida mtambuka (multiplier effect) na kuendelea kutunza, kuongeza thamani ya michango ya wanachama na kuongeza uwezo wa kuendelea kulipa mafao.

**MTOA HOJA:** Mhe. Ally Hassan Omar King – (Mb. Jang'ombe).

**UFAFANUZI WA HOJA:** Serikali inasimamia uwekezaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kupitia Miongozo ya uwekezaji ili kuhakikisha uwekezaji unaofanywa na mifuko hiyo ni salama na wenye tija kwa wanachama. Aidha, kwa kuzingatia miongozo hiyo, Mifuko itaendelea kubaini maeneo salama na yenye tija kwa Taifa.

**16. HOJA:** Serikali ihakikishe kuwa waliokuwa wafanyakazi wa kiwanda cha MUTEX wanalipwa mafao yao baada ya kiwanda kubinafsishwa.

**MTOA HOJA:** Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi– (Mb. Musoma Mjini).

**UFAFANUZI WA HOJA:** Kiwanda cha MUTEX kilibinafsishwa mwaka 1993. Hata hivyo, baada ya kubinafsishwa Serikali Iliwalipa Mafao waliokuwa wafanyakazi 317 wa kiwanda cha MUTEX kulingana na vipindi vyao vya uchangiaji kupitia uliokuwa Mfuko wa PPF ambao kwa sasa ni sehemu ya Mfuko wa PSSSF. Aidha, Serikali inatoa rai kwa wanachama wenye madai ya mafao ya Hifadhi ya Jamii kuwasilisha maombi yao kwenye ofisi za Mfuko wa PSSSF zilizo karibu.

**17. HOJA:** Serikali ieleze itaanza lini kutoa mikopo kwa wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii baada ya Sheria na Kanuni kupitishwa na Bunge.

**MTOA HOJA:** Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi– (Mb. Musoma Mjini).

**UFAFANUZI WA HOJA:** Sheria ya Hifadhi ya Jamii Sura 135 ya mwaka 2019, Serikali imeandaa Kanuni za kutumia asilimia 50 ya mafao ya wanachama kama dhamana ya mikopo ya kununua na kujenga nyumba kupitia taasisi za fedha. Utekelezaji wa kanuni hizi ambazo zilitangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 141 la mwaka 2024 zitaanza kutumika baada ya kumalizika kwa maandalizi yakiwemo ya kusajili taasisi za fedha zitakazojitokeza kutoa huduma hiyo. Aidha, baada ya kupitishwa kwa kanuni hizo,

Serikali imeandaa mwongozo wa kuratibu na kusimamia suala hili ambao unapatikana kupitia tovuti ya Wizara.

## F. HUDUMA ZA WATU WENYE ULEMAVU

**18. HOJA:** Mfuko wa Taifa wa Watu wenye Ulemavu usiunganishwe na mifuko mingine ya uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa sababu lengo la mfuko huu ni kutoa huduma kwa watu wenye Ulemavu.

**MTOA HOJA:** Mhe. Stella Ikupa Alex – (Mb. Viti Maalum)

**UFAFANUZI WA HOJA:** Serikali itaendelea kuboresha Mfuko wa Taifa wa Watu wenye Ulemavu bila kuathiri madhumuni ya kuanzishwa kwake na kuwa inatambua umuhimu wa mfuko huu katika kuwahudumia Watu wenye Ulemavu nchini.

**19. HOJA:** Serikali itenge na itoe fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kinga dhidi ya miale ya jua kwa Watu wenye Ualbino.

**MTOA HOJA:** Mhe. Stella Ikupa Alex – (Mb. Viti Maalum)

**UFAFANUZI WA HOJA:** Katika mwaka 2024/25 jumla ya kiasi cha Shillingi 1,159,383,821/= kimetengwa kwa ajili ya Mfuko wa Taifa wa Watu wenye Ulemavu pamoja na matumizi mengine, itawezesha ununuzi wa mafuta kinga dhidi ya miale ya jua kwa Watu wenye Ualbino.

Aidha, katika kuboresha huduma hii, mwaka 2024, Serikali ilizindua Mpango Kazi wa Taifa wa Haki na Ustawi kwa Watu wenye Ualbino (2024/25 – 2026/29) ambao umetoa majukumu mbalimbali ya wadau ikiwemo kutenga na kununua mafuta kinga dhidi ya miale ya jua kwa Watu wenye Ualbino.

Serikali pia imeandaa Mpango wa Huduma za Ustawi wa Jamii katika Halmashauri (Comprehensive Council Social Welfare Operational Plan) na kuweka mipango ya vipaumbele na bajeti za ustawi wa jamii ngazi ya Halmashauri ikiwemo kutengwa kwa bajeti ya mafuta kinga kwa Watu wenye Ualbino.

**20. HOJA:** Serikali itoe fedha za Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu ambazo zilipangwa kutolewa katika mwaka wa fedha 2024/2025 ili zitumike katika kutekeleza shughuli za watu wenye ulemavu.

**MTOA HOJA:** Mhe. Riziki Said Lulida – (Mb. Viti Maalum)

**UFAFANUZI WA HOJA:** Katika mwaka 2024/25, Serikali ilitenga fedha kiasi cha Shillingi 1,159,383,821/= kwa ajili ya Mfuko wa Taifa wa Watu wenye Ulemavu. Serikali itahakikisha fedha hizo zinatolewa kabla ya mwaka wa fedha 2024/25 kumalizika.

**21. HOJA:** Serikali iwasaidie watu wenye ulemavu kupata vifaa saidizi ili waweze kushiriki kikamilifu katika masuala mbalimbali.

**MTOA HOJA:** Mhe. Riziki Said Lulida – (Mb. Viti Maalum)

**UFAFANUZI WA HOJA:** Serikali imeweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kuwawezesha Watu wenye Ulemavu kupata vifaa saidizi, ikiwa ni pamoja na kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Teknolojia Saidizi wa mwaka 2024-2027 ili kuhakikisha kunakuwa na mfumo endelevu wa upatikanaji wa vifaa saidizi kwa Watu wenye Ulemavu.

Aidha, katika mwaka 2024/25 jumla ya kiasi cha Shillingi 1,159,383,821/= kimetengwa kwa ajili ya Mfuko wa Taifa wa Watu wenye Ulemavu pamoja na matumizi mengine, utawezesha ununuzi wa vifaa saidizi.

Serikali itaendelea kuwashirikisha wadau mbalimbali ili vifaa saidizi viweze kupatikana kwa ajili ya Watu wenye Ulemavu.

## G. USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI

**22. HOJA:** Serikali itoe elimu kuhusu usalama na afya mahali pa kazi ili kuzuia magonjwa, ajali na vifo vitokavyo na kazi.

**MTOA HOJA:** Mhe. Janejelly Ntate James – (Mb. Viti Maalum)

**UFAFANUZI WA HOJA:** Serikali kupitia Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) imeendelea kutoa elimu kupitia warsha, semina, tovuti, maonesho ya kitaifa, machapisho, vyombo vya habari pamoja na mitandao ya kijamii ili kuongeza wigo wa kuwafikia wafanyakazi wengi zaidi kuhusiana na usalama na afya mahali pa kazi ili kupunguza magonjwa na ajali. Kwa kipindi cha nusu mwaka (2024/25) idadi ya wafanyakazi waliopewa elimu ni 13,702. Aidha, kwa mwaka 2025/26 Serikali inatarajia kutoa elimu kwa wafanyakazi 45,600.

**HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao mizuri na yenye tija waliyoitoa katika Hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu kuhusu bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

***Mheshimiwa Spika*, NINAUNGA MKONO HOJA**

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Patrobass Katambi, Naibu Waziri. Nichukue fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao tumepata nafasi ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tangu asubuhi ya leo, na pia nawashukuru Serikali ambayo imepata nafasi ya kutoa ufafanuzi na kupokea hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge ambazo zimetufikisha muda huu.

Waheshimiwa Wabunge, tunalo tangazo moja muhimu, nalo ni tangazo muhimu sana. Narudia tena, ni tangazo muhimu sana, linatoka kwa Katibu wa Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Rashid Shangazi. Anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi kuhusu Kikao cha *Party Caucus* leo jioni mara baada ya shughuli za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, mara baada ya Shughuli za Bunge, leo jioni kutakuwa na kikao cha Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama Cha Mapinduzi, kikao kitafanyika *White House,* Ofisi za Chama Cha Mapindzui Makao Makuu, maelezo yanasomeka, asikosekane Mbunge hata mmoja.

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.12 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tuketi.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Sasa namwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ajira, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, atafuatiwa na Mheshimiwa Lukuvi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kufika siku ya leo tukihitimisha hoja ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kukushukuru kwa kunipa fursa ya kusimama mbele ya Bunge lako ili kuchangia hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na pia, kutoa maombi ya fedha nikiunga mkono.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja, na pili, kwa kipekee kabisa, naomba uniruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania, kwa kutimiza miaka minne tangu aapishwe kuliongoza Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi chake tumeshuhudia maendeleo makubwa sana ambayo Serikali imetekeleza chini ya uongozi wake. Hakika amethibitisha kuwa, yeye ni kiongozi bora, imara, shupavu na mahiri kuliongoza Taifa letu na kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020. Kwa hakika anafaa kuongezewa muda kuliongoza Taifa letu kwa miaka mingine mitano tena. Namwombea Mwenyezi Mungu amjalie afya na siha njema ili aweze kutekeleza majukumu yake ya kuliongoza Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya kazi, ajira na wenye ulemavu. Kwa kuwa, hii ni mara yangu ya kwanza nasimama nikiwa Waziri wa Wizara hii ya Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, nataka nitoe salamu kubwa za shukrani kwake yeye, lakini pia, na wote wanaomsaidia na kumshauri katika kufanya kazi hizi ambazo zimeendelea kufanyika katika Wizara yetu na miongozo mbalimbali anayotupa.

Mheshimiwa Spika, pia, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais, Dkt. Philip Isdor Mpango, kwa miongozo mbalimbali anayotupa, na pili, kwa jinsi ambavyo anaendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, vilevile, naomba kutumia nafasi hii kwa fursa ya kipekee, kumshukuru sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa

Majaliwa, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye yeye pia ni kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni kwa ushirikiano mkubwa na miongozo anayonipa ambayo inatuwezesha mimi na wenzangu ndani ya Wizara kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ninaendelea kukuombea Mungu akujalie heri na Wanaruangwa wakusikie na wakuchague tena kwa kura nyingi kwa sababu, nchi na Bunge bado linaendelea kukuamini. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko, Mbunge, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati, naye kwa kuendelea kutuongoza vyema katika majukumu yetu tunayotekeleza.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana kwa ushauri wake, namshukuru sana kwa miongozo yake. Kama ilivyo kwa Waziri Mkuu, naye ninamtakia kila la heri kwa Wanabukombe, kama ambavyo walimleta, naomba wamrudishe tena ili tuendelee kuchapa kazi ya kuendelea kulisukuma mbele gurudumu la maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, niruhusu nikupongeze wewe binafsi, Spika wetu na Rais wa Mabunge Duniani. Kwa hakika, kwa lugha ya mtaani, wanasema mpira unaupiga mwingi sana. Mwenyezi Mungu akujalie heri katika kutekeleza majukumu yako, lakini pia, nataka nikuhakikishie, sisi kama Wabunge wenzako, tutaendelea kuhimizana na wewe kusimamia majukumu yetu na kuhakikisha kwamba, Mbeya inakupendekeza, haikuachi ukaelea.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu nimshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa namna ya pekee wanavyoendelea kuliongoza Bunge letu kwa umahiri mkubwa sana. Nawaombea afya njema, lakini pia, nao nawatakia heri katika hayo yanayokuja hapo mbele.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana Waziri Mwenzangu, *Senior* Wiliam Vangimembe Lukuvi, Mbunge wa Jimbo la Ismani, Waziri wa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimwahidi Mheshimiwa Lukuvi, ushirikiano mzuri wa kutosha katika kumsaidia yeye, na pia, kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kutekeleza majukumu yake, naye pia namshukuru sana na nimtakie kila la heri mzee wa kazi huko jimboni na Wanaismani wajue kwamba, tunaendelea kumhitaji. Amekuwa mwongozo wetu, sisi wengine tumefaidika naye tukiwa umoja wa vijana, tukiwa chipukizi na hata leo tuko ndani ya Bunge tunaendelea kufaidika naye katika miongozo yake. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba uniruhusu nimshukuru Mheshimiwa Patrobas Katambi, Mbunge wa Shinyanga Mjini na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu; yeye pamoja na Mheshimiwa Ummy Hamis Nderiananga, Mbunge wa Viti Maalum, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu kwa ushirikiano mkubwa wanaotupatia mimi na mwenzangu Mheshimiwa Lukuvi katika kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, msaada wao ndiyo ambao unasimamisha mafanikio makubwa unayoyaona leo yanatokea katika ofisi chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tunawashukuru sana. Tunawatakia kila la heri katika michakato inayokuja, lakini sisi ndani ya Wizara tumeridhishwa, tunashukuru na tunaendelea kuwaombea heri wananchi wawarudishe pia, ili muweze kutekeleza majukumu ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kuwashukuru sana Mawaziri wenzangu wa Wizara mbalimbali kwa ushirikiano mkubwa wanaotupatia katika kutekeleza majukumu haya. Pia, nitumie fursa hii kwa kipekee kabisa kumshukuru Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Bibi Marry Maganga, pamoja na Dkt. Jimmy James Onazi, Katibu Mkuu Sera,

Bunge na Uratibu na Naibu Makatibu wetu wawili; Bi. Zuhura Yunusi na Dkt. James Kilabuko pamoja na watumishi wote wa taasisi tunazozisimamia kwa ushirikiano mkubwa wanaotupa katika kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, pia, naomba kuwashukuru wadau wote wa maendeleo tunaoshirikiananao katika kutekeleza majukumu yetu. Hapa naomba niwataje kwa uchache. Kwanza ni Mashirikisho ya Vyama vya Wafanyakazi Tanzania *(TUCTA),* Chama cha Waajiri Tanzania *(ATE),* Baraza la Taifa la Ushauri wa Watu Wenye Ulemavu, Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA), *NGOs* za ndani na za Kimataifa bila kuwasahau wadau wakubwa *ILO, UN Women, UNICEF* na *UNFPA* kwa kuwataja kwa ufupi.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa na kipekee naomba nitumie nafasi hii kuishukuru sana familia yangu, wazazi wangu na hasa mke wangu kipenzi, Mama Aziza, watoto wetu na wananchi wa Jimbo la Chalinze ambao kwa kweli, ushirikiano wao mkubwa wanaotupa umetuwezesha kutimiza majukumu haya vizuri. Nataka tu nitambue uongozi bila kuwataja kwa majina, watu wa Chalinze ambao wapo upande wako wa kushoto pale juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu hoja za Kamati na Waheshimiwa Wabunge, nami naomba niungane na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi wa Maendeleo ya Jamii, ikiongozwa na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum na Mwenyekiti wa Kamati yetu, kwa ushauri na ushirikiano mkubwa aliotupatia wakati wa kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, pia, nataka niipongeze Timu ya *Simba Sports* kwa kufanikiwa kuingia nusu Fainali ya Kombe la Washindi Afrika. Naomba nitumie nafasi hii tu kuwakumbusha, wenzenu walicheza fainali, ninyi mjipange mkachukue kombe. Mpira ni

ushindani, mpira ni uwekezaji, lakini mwisho wa siku mpira ni furaha na mpira ni burudani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwahakikishia kuwa, maoni na ushauri uliotolewa kwa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Fungu 65 na Fungu 15 kwa mwaka 2025/2026 yote tumeyazingatia. Pia, naomba kutoa shukrani za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango na ushauri wao ambao kwa kiasi kikubwa umelenga kuboresha utekelezaji wa majukumu ya ofisi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, naomba kuwatambua na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hotuba ya Waziri Mkuu kwa kuongea na kwa maandishi. Naomba orodha yao iingie kwenye *Hansard* kama ilivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 inayohusu kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara, naomba sasa kwa heshima na taadhima uniruhusu nitoe ufafanuzi wa baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge walizichangia na kutaka ufafanuzi, na hoja nyingine zitafafanuliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuwa anahitimisha hoja yake.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ilikuwa na hoja saba zilizotolewa kwa niaba yao na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu. Nataka kutumia nafasi hii kwanza kuishukuru Kamati, kama nilivyoeleza mwanzo kwa michango yao mizuri, na pili, kwa kumbukumbu na maelekezo ambayo sisi kama Wizara, tumeyachukua. Nataka kulihakikishia Bunge na Kamati yako kuwa, michango yao yote imechukuliwa na itafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, maelezo mengine yalishatolewa mwanzo na Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna maeneo naomba uniruhusu niweze kujazia nyama na mengine kutoa ufafanuzi zaidi ili Bunge lako lisiwe na muda mrefu wa

kusikiliza *repetition* ya maeneo hayo badala ya kuendelea mbele kujadili hotuba ya bajeti iliyo mbele yako.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ya kuhakikisha kwamba, Watanzania wanapata fursa ya kupewa nafasi ya kufanya kazi nje ya nchi; pamoja na maelezo mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri nataka kuelezea kwamba, Serikali imekamilisha mfumo wa *ESMIS* ambao unasaidia kuunganisha taarifa za wenzetu wanaokwenda kufanya kazi nje, ili waweze kuunganishwa na mifumo ya kibenki, ikiwezekana hapa Tanzania, ili zile *remittances* zinazokuja ziweze kujulikana.

Mheshimiwa Spika, leo hii katika moja ya jambo kubwa ambalo Bunge lako katika michango yao limeelezwa kwa sauti ya juu sana ni hesabu ndogo ya marejesho ambayo yanaletwa nchini kwetu. Nataka niwahakikishie, moja ya kipengele ambacho kimekuwa ni changamoto kwetu ni kukosekana kwa mfumo sahihi ambao tunaweza tukapata taarifa ya fedha kiasi gani zinaletwa, na watu wangapi wanafanya nini na kiasi gani kinapatikana?

Mheshimiwa Spika, nataka tuendelee kulihakikishia Bunge lako kwamba, mfumo huu ambao nimeusema hapa utaanza kufanya kazi katika mwaka huu wa fedha. Tumeshakamilisha mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kuendesha mashtaka na kuweka kumbukumbu kwa migogoro ya wafanyakazi. Yaani hapa nazungumzia *OCMS,* ambayo kwa lugha ya Kiingereza…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, dakika mbili,  malizia. Kengele ya pili imeshagonga.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Dakika kumi?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa, dakika mbili.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Dakika mbili! Dakika kumi zimekwisha!

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, nimekuongeza dakika mbili kwa sababu, mbili nilishakupa. Yaani muda wako ulikuwa umekwisha, nikakuongeza dakika mbili na sasa nimekuongeza mbili umalizie.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, sawa. Kwa niaba ya Serikali, naomba yale majibu yetu yote tuliyokuwa tumeyaandaa, yaingie kwenye *Hansard,* ili tusije tukaacha ombwe kwa yale maswali au michango mizuri iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme tena kwamba, naunga mkono hoja iliyotolewa. Baada ya hapo, kwa ruhusa yako, naomba sasa nikae. *(Makofi)*

**MAELEZO YA MHESHIMIWA RIDHIWANI JAKAYA KIKWETE (MB) WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU, AKITOA UFAFANUZI WA MICHANGO YA WAHESHIMIWA WABUNGE, KATIKA KUHITIMISHA HOJA YA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU PAMOJA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kufikia siku hii ambayo tunahitimisha hoja ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2025/26.

**Mheshimiwa Spika,** ninashukuru sana kwa kunipa fursa ya kusimama mbele ya Bunge lako tukufu ili kuchangia pamoja na kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge walizotoa wakati wakichangia Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu hususan katika maeneo yanayohusu masuala ya Kazi, Vijana, Ajira, Hifadhi ya Jamii na Wenye Ulemavu.

**Mheshimiwa Spika,** ninaomba kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka minne tangu aapishwe kuliongoza Taifa letu. Katika kipindi chake tumeshuhudia mambo makubwa ambayo Serikali imeyatekeleza

chini ya uongozi wake. Hakika amethibitisha kuwa ni kiongozi bora, imara, shupavu na mahiri kwa kuliongoza vyema taifa letu na kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika,** Kipekee, ninamshukuru Mhe. Rais kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu. Aidha, ninaahidi kutekeleza majukumu yangu kwa weledi, uadilifu na uzalendo ili Sekta hii iendelee kuchangia maendeleo ya nchi. Ni imani yangu nimetekeleza wajibu wangu kwake na Taifa langu, nikitekeleza majukumu haya. Ahadi yangu kwake sintoisahau imani hii kubwa ambayo Mwanasiasa yeyote chini ya jua, angetarajia kupewa, Mimi ni nani, niache kumshukuru yeye baada ya Mwenyezi Mungu mwenye utukufu.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Taasisi zinazosimamiwa na Ofisi yangu pamoja na Wadau tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu ili amjalie afya njema na kumpatia maono zaidi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** pia nitumie fursa hii kumshukuru Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango kwa miongozo mbalimbali anayonipatia na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile, ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru **Mheshimwa Kassim Majaliwa Majaliwa (MB)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ni Kiongozi Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni kwa ushirikiano na miongozo anayonipatia ambayo inaniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** niendelee pia kumshukuru Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.) Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kuendelea kuniongoza vema katika kutekeleza majukumu yangu.

**Mheshimiwa Spika,** nikupongeze Wewe Binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa namna mnavyoendelea kuliongoza Bunge letu kwa umahiri mkubwa. Ninawaombea afya njema.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile, ninapenda kumpongeza Waziri mwenzangu katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Wiliam Vangimembe Lukuvi (Mb.), Mbunge wa Jimbo la Isimani kwa kuteuliwa kuwa, Waziri wa Nchi - Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu. Ninaahidi kumpa ushirikiano wa kutosha katika kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** Pia, niwashukuru Mheshimiwa Paschal Patrobas Katambi, Mbunge wa Shinyanga Mjini na Naibu Waziri - Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu na Mheshimiwa Ummy Hamis Nderiananga, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Naibu Waziri - Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

**Mheshimiwa Spika,** Ninapenda kuwashukuru Mawaziri wenzangu wa Wizara mbalimbali kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

**Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii pia, kumshukuru Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira, na Wenye Ulemavu, Bibi Mary N. Maganga, na Dkt. Jim James Yonazi – Katibu Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu na Naibu Makatibu Wakuu, Bi. Zuhura Yunus na Dkt. James Henry Kilabuko na Pamoja na Watumishi wote na Taasisi ninazozisimamia kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

**Mheshimiwa Spika,** ninaomba kuwashukuru wadau wote wanaoshirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu katika kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwemo wadau wa Utatu ambao ni Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Chama cha Waajiri Tanzania (ATE); Baraza la Taifa la Ushauri la Watu wenye Ulemavu; na Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA).

**Mheshimiwa Spika,** Ninawashukuru pia Wadau wa Maendeleo wanaochangia utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ambao ni Shirika la Kazi Duniani (ILO), UN – WOMEN, UNICEF na UNFPA.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee na kwa dhati ninaishukuru familia yangu na Wananchi wa Jimbo la Chalinze Mjini kwa kuendelea kuniunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika,** kabla ya kujibu hoja za Kamati na Waheshimiwa Wabunge, nami niungane na Mhe. Waziri Mkuu kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, ikiongozwa na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq Mbunge wa Viti Maalum na Mwenyekiti wa Kamati, kwa ushauri na ushirikiano mkubwa waliotupatia wakati wa kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa mwaka 2025/26.

**Mheshimiwa Spika,** Ninapenda kuwahakikishia kuwa maoni na ushauri katika utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa mwaka 2025/26 utazingatiwa.

**Mheshimiwa Spika,** niombe pia kutoa shukrani za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango na ushauri wao, ambao kwa kiasi kikubwa imelenga kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi yangu. Kwa namna ya pekee ninaomba kuwatambua na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hotuba ya Waziri Mkuu kwa kuongea na kwa maandishi. Ninaomba orodha yao iingie kwenye Hansard kama ilivyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (2) ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 inayohusu kujadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara, ninaomba sasa kwa heshima na taadhima, uniruhusu nitoe ufafanuzi wa baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge walichangia na kutaka ufafanuzi. Hoja

zingine zitafafanuliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuwa anahitimisha hoja yake.

## A. KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII

1. **HOJA:** Serikali iongeze kasi ya kuwaunganisha Watanzania na fursa za ajira nje ya nchi.

**MTOA HOJA:**
Mhe. Fatma Hassan Toufiq (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii.

**UFAFANUZI WA HOJA:** Ushauri umepokelewa. Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu inaendelea kufanya majadiliano na kusaini Hati za Makubaliano na nchi za kimkakati ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa fursa za ajira nje ya nchi. Kuanzia mwaka 2022 hadi Machi, 2025 jumla ya Watanzania 7,204 wameunganishwa na fursa za ajira nje ya nchi. Aidha, Serikali imesaini Hati za Makubaliano na nchi za Qatar, Saudi Arabia, Umoja wa Falme za Kiarabu na Iran. Kwa sasa Serikali inaendelea kufanya majadiliano ya mashirikiano na nchi zifuatazo: - Korea Kusini, Ujerumani, Kanada, Uingereza, Oman, Kuwait, Uturuki, Sweden, Denmark, Norway, na Poland na mazungumzo yanakwenda vizuri ili kufikia makubaliano.

2. **HOJA:** Serikali iongeze kasi ya kufanya maboresho ya mfumo wa huduma za ajira (ESMIS) ili kuwezesha kubadilishana taarifa mbalimbali zikiwemo za kibenki kwa lengo la kurahishishisha upatikanaji wa takwimu za mapato yanayorejeshwa na Watanzania wanaofanya kazi nje ya nchi.

**MTOA HOJA:** Mhe. Fatma Hassan Toufiq (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii.

**UFAFANUZI WA HOJA:** Ushauri umepokelewa. Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye ulemavu inaendelea kufanya maboresho ya Mfumo wa Huduma za Ajira (Employment Services

Management Information System – ESMIS) ili uweze kusomana na mifumo mbalimbali ikiwemo wa kibenki. Maboresho haya yanatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2025/26.

3. **HOJA:** Serikali itoe fedha kwa wakati ili kuwezesha Mradi Na.4954 wa Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu kutekeleza majukumu yake kwa wakati.

**MTOA HOJA:** Mhe. Fatma Hassan Toufiq (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii.

**UFAFANUZI WA HOJA:** Ushauri umepokelewa**.** Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira, Vijana na Wenye ulemavu itahakikisha kiasi cha **Shillingi 1,159,383,821/=** kilichotengwa kwa ajili ya Mfuko wa Taifa wa Watu wenye Ulemavu, kinapatikana kabla ya mwaka 2024/25 kufikia ukomo.

4. **HOJA:** Serikali itoe fedha kuwezesha Mradi Na. 4952, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, kila mwaka na kwa wakati na kuongeza kiasi cha mtaji wa mfuko huu.

**MTOA HOJA:** Mhe. Fatma Hassan Toufiq (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii.

**UFAFANUZI WA HOJA: Ushauri umepokelewa.** Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira, Vijana na Wenye ulemavu itahakikisha kiasi cha **Shillingi 657,252,868/=** kilichotengwa kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, kinapatikana kabla ya mwaka 2024/25 kufikia ukomo.

5. **HOJA:** Serikali itenge theluthi moja ya michango (1/3) inayotozwa kwa waajiri ya kukuza ujuzi kulingana na makubaliano baina ya Serikali na Sekta Binafsi.

**MTOA HOJA:** Mhe. Fatma Hassan Toufiq (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii.

**UFAFANUZI WA HOJA:** Ushauri umepokelewa. Serikali inaendelea kulifanyia kazi suala hili ili kuongeza bajeti ya Programu ya Taifa ya

Kukuza Ujuzi. Wakati wa mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya nusu mwaka 2025/26, Serikali itaangalia uwezekano wa kugharamia mahitaji ya ziada ya uendelezaji wa ujuzi kupitia Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi **(Maelezo ya ziada Kiambatisho Na.1).**

6. **HOJA:** Serikali kukamilisha mfumo wa kieletroniki wa kuendesha mashauri na kutunza kumbukumbu.

**MTOA HOJA:** Mhe. Fatma Hassan Toufiq (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii.

**UFAFANUZI WA HOJA: Ushauri umepokelewa.** Mfumo wa Kielektroniki wa kuendesha mashauri na kutunza kumbukumbu (Online Case Management System-Ocms) umekamilika kwa asilimia 92 na utaanza kutumika rasmi katika Mwaka wa Fedha 2025/26.

7. **HOJA:** Serikali itoe elimu ya matumizi ya mfumo wa kieletroniki wa kuendesha mashauri na kutunza kumbukumbu kwa Waajiriwa, Wasuluhishi na Waamuzi.

**MTOA HOJA:** Mhe. Fatma Hassan Toufiq (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii.

**UFAFANUZI WA HOJA**: **Ushauri umepokelewa.** Katika Mwaka wa Fedha 2025/26, Serikali itaendelea kutoa elimu ya matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa kuendesha mashauri na kutunza kumbukumbu kwa wadau wake na umma kupitia Vyombo vya habari, Mitandao ya kijamii, Maonesho, Matangazo ya redio, Televisheni na Magazeti. Aidha, Mfumo huo utasomana na Mifumo mingine kama vile Mahakama, Mfumo wa Vibali, RITA na NIDA.

### B. USIMAMIZI WA VIWANGO VYA KAZI

8. **HOJA**: Serikali ihakikishe wafanyakazi walioachishwa kazi katika mashamba ya chai Wilayani Rungwe wanalipwa haki zao ikiwemo mafao ya NSSF .

**MTOA HOJA**: Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda – (Viti Maalum)

**UFAFANUZI WA HOJA**: Mashamba ya Chai Wilayani Rungwe, yalifungwa na wafanyakazi wote walilipwa stahiki zao ikiwemo Mafao ya NSSF. Aidha, wafanyakazi 60 hawakuridhika na Stahiki zilizotolewa, hivyo mwaka 2020 walifungua maombi anuai Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA). Maombi hayo yalitupiliwa mbali kutokana na kukosa sababu za msingi kwa mujibu wa sheria. Kwa sasa suala hili lipo katika Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi mkoani Mbeya kwa ajili ya marejeo.

9. **HOJA**: Ni lini Serikali imehuisha pensheni za wastaafu wa vyuo vikuu ili kuendana na hali halisi ya maisha.

**WATOA HOJA:**
Mhe. Saasisha Elinikyo Mafuwe - (Mb. Hai)
Mhe. Issaay Zacharia Paulo – (Mb. Mbulu Mjini)

**UFAFANUZI WA HOJA:** Serikali imeendelea kuboresha pensheni za wastaafu wote katika mifuko ya Hifadhi ya jamii ambapo mnamo mwezi Januari, 2025, Serikali imeongeza kima cha chini cha pensheni kutoka shilingi 100,000 hadi shilingi 150,000 kwa mwezi.

Aidha, kwa mujibu wa Kifungu Namba 11 cha Kanuni ya Mafao ya Wanachama, Serikali imehuisha pensheni ya kila mwezi (Indexation) kwa Wastaafu wote wa mifuko kuanzia mwezi Januari, 2025.

10. **HOJA:** Serikali inashauriwa kusimamia na kudhibiti utoaji wa vibali vya kazi kwa raia wa kigeni ambao hawana vigezo wanaokuja kufanya kazi ambazo zingeweza kufanywa na wazawa.

**WATOA HOJA:**
Mhe. Charles Stephen Kimei – (Mb. Vunjo) na
Mhe. Janejelly Ntate James – (Mb. Viti Maalum)

**UFAFANUZI WA HOJA:** Serikali inaendelea kusimamia na kudhibiti ajira kwa raia wa kigeni na kuwapa fursa wazawa ambapo katika

kushughulikia maombi ya vibali hivyo, Serikali huzingatia vigezo vilivyoanishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Ajira za Wageni Sura 436 **(Maelezo ya ziada Kiambatisho Na. 2).**

**C. HUDUMA ZA AJIRA NA UKUZAJI UJUZI**

**11.** **<u>HOJA:</u>** Serikali inashauriwa kuboresha mafunzo ya ukuzaji ujuzi kwa vijana ili yaendane na muda halisi wa mafunzo husika.

**<u>MTOA HOJA:</u>** Mhe. Sylvia Francis Sigula - (Mb. Viti Maalum)

**<u>UFAFANUZI WA HOJA:</u>** **Ushauri umepokelewa.** Muda wa mafunzo ya kukuza ujuzi yanatolewa kwa kuzingatia aina ya mafunzo ya ujuzi husika. Aidha, Serikali imekuwa ikitoa mafunzo ya ukuzaji ujuzi ya muda mfupi ili kuwawezesha vijana kupata ujuzi unaohitajika katika soko la ajira kupitia Programu ya Taifa ya Ukuzaji Ujuzi.

**12.** **<u>HOJA:</u>** Serikali itenge 1/3 ya Skill Development Levy (SDL) kwenye Programu ya Kukuza Ujuzi kama ilivyo katika makubaliano kati ya Serikali na Waajiri ili kuwawezesha vijana kupata ujuzi kama ilivyobainishwa kwenye Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa kuwa ifikapo mwaka 2025/26 nguvu kazi kuwa na ujuzi, kuendelea na utekelezaji wa afua zinazohusiana na kukuza ujuzi na kuchochea ukuzaji wa fursa za ajira kwa vijana na wenye Ulemavu.

**<u>MTOA HOJA:</u>** Mhe. Ally Hassan Omar King – (Mb. Jang'ombe) na Mhe. Sylvia Francis Sigula - (Mb. Viti Maalum).

**<u>UFAFANUZI WA HOJA:</u>** Ushauri umepokelewa. Serikali inaendelea kulifanyia kazi suala hili ili kuongeza bajeti ya Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi. Wakati wa mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya nusu mwaka 2025/26, Serikali itaangalia uwezekano wa kugharamia mahitaji ya ziada ya uendelezaji wa ujuzi kupitia Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi **(Maelezo ya ziada Kiambatisho Na. 1).**

**13.** **<u>HOJA</u>:** Serikali iongeze kasi ya kuwaunganisha Watanzania na fursa za ajira nje ya nchi.

**WATOA HOJA:**
Mhe. Saasisha Elinikyo Mafuwe (Mb. Hai)
Mhe. Fatma Hassan Toufiq (Mb. Viti Maalum),

**UFAFANUZI WA HOJA:** Ushauri umepokelewa. Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu inaendelea kufanya majadiliano na kusaini Hati za Makubaliano na nchi za kimkakati ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa fursa za ajira nje ya nchi. Kuanzia mwaka 2022 hadi Machi, 2025 jumla ya Watanzania 7,204 wameunganishwa na fursa za ajira nje ya nchi. Aidha, Serikali imesaini Hati za Makubaliano na nchi za Qatar, Saudi Arabia, Umoja wa Falme za Kiarabu na Iran. Kwa sasa Serikali inaendelea kufanya majadiliano ya mashirikiano na nchi zifuatazo: - Korea Kusini, Ujerumani, Kanada, Uingereza, Oman, Kuwait, Uturuki, Sweden, Denmark, Norway, na Poland na mazungumzo yanakwenda vizuri ili kufikia makubaliano.

**Mheshimiwa Spika, NAUNGA MKONO HOJA**

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge na Uratibu, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana tena hapa katika Bunge lako Tukufu tunapoelekea kuhitimisha mjadala wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, vilevile, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu, ili kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge walizotoa wakati wa kuchangia hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Bunge. Kwa sababu hiyo, nafikiri utanipendelea kidogo maana hoja za Bunge ni ngumu hapa.

Mheshimiwa Spika, kipekee nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa mshauri wake, lakini pia, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu. Ni heshima kubwa kwangu kutumikia nafasi hizi, na ni dhamira yangu kuhakikisha kuwa, nafanya kazi kwa weledi, uadilifu, uaminifu na unyenyekevu mkubwa huku nikizingatia maslahi mapana ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutolea ufafanuzi hoja za Waheshimiwa Wabunge, naomba nianze kwa kutoa salamu za pongezi na shukrani kwa viongozi wetu wakuu wa Kitaifa kwa namna wanavyoiongoza nchi yetu kwa ufanisi weledi na dhamira ya kweli ya kuwatumikia Watanzania. Nianze kwa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Sukuhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kutuongoza kwa ustadi mkubwa na kutoa miongozo madhubuti katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya utekelezaji wa Ilani katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita inaonesha kuwa, ilani imetekelezwa kwa zaidi ya 90% katika sekta na nyanja zote za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Huu ni ushahidi wa juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali katika kuwaletea wananchi maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana chini ya uongozi wake na dhamira yake ya dhati ya kuwatumikia Watanzania, ndiyo chachu iliyokifanya Chama cha Mapinduzi kumteua, Rais wetu mpendwa, kuwa mgombea wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uchaguzi wa Mwaka 2025. Tunaendelea kumwombea, Mwenyezi Mungu aendelee kumjalia afya njema, hekima na nguvu tunapoelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2025.

Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu watakubaliana nami kuwa uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan umejikita katika mabadiliko chanya, dhamira ya dhati ya maridhiano yakiongozwa na falsafa ya *4R* na maendeleo ya kweli, kwa kila Mtanzania. Kupitia uongozi wake, Taifa letu

linaendelea kustawi, kuaminika na kusonga mbele kwa kasi, hivyo wote twendeni tukampe kura zote za ndiyo kwenye Uchaguzi Mkuu ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa utendaji kazi wake na kumsaidia Mheshimiwa Rais kutuletea wananchi maendeleo. Mheshimiwa Makamu wa Rais amekuwa kiongozi imara, mnyenyekevu, shupavu, mwenye busara na mchapakazi katika kutekeleza mikakati mbalimbali ya kisera inayolenga kuboresha ustawi wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa juhudi zake za kudumisha Umoja wa Kitaifa na kuleta maendeleo endelevu kwa Wananchi wa Zanzibar. Mheshimiwa Rais Dkt. Mwinyi ni kiongozi thabiti anayefanya kazi kwa bidii na kwa ushirikiano mkubwa.

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuendelea kuaminiwa na Chama cha Mapinduzi, kuwa mgombea wake kwa nafasi ya Urais wa Zanzibar kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025. Uteuzi huu ni ushahidi tosha kwamba ameitekeleza vyema Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa mwaka 2025 kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kumshukuru sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wote ambao 80% mmempongeza humu ndani kwanza, kwa maelekezo na miongozo aliyonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku. Pili, namshukuru na kumpongeza kwa kuongoza shughuli za Serikali hapa Bungeni kwa umahiri na kutoa miongozo yenye manufaa kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, aidha, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ya bajeti ambayo ameiwasilisha kwa weledi na ufasaha mkubwa. Hotuba hiyo imebeba vipaumbele

muhimu vinavyoakisi mahitaji ya Taifa letu na itaendelea kutupatia mwelekeo sahihi katika kutekeleza majukumu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa hotuba kama mnavyojua Mheshimiwa Waziri Mkuu alielekeza Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi iliyosomwa kwenye Mkutano Mkuu itolewe kwa wananchi kwa siku saba mfululizo. Taarifa hii imerushwa kwenye vyombo vyote vya habari ili wananchi waweze kuona na kusikia kabla yeye hajatoa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, vilevile, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko, Mb, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kwa maelekezo na miongozo anayonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Ninyi nyote ni mashahidi, Mheshimiwa Dkt. Dotto Biteko ni kiongozi mpole, mpenda ushirikiano na mnyenyekevu. Waheshimiwa Wabunge wote tunamjua vizuri, Mungu ambariki.

Mheshimiwa Spika, kipekee, nakupongeza wewe binafsi kwa uongozi imara usioyumba wa Bunge letu, pia kwa ufanisi mkubwa unaouonesha katika nafasi ya Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU)*. Nakupongeza na kushukuru sana kwa sababu hata *u-chief whip* wangu bila ushirikiano wako hauna maana. Kwa hiyo, mafanikio yangu yanatokana na ushujaa wako wa kukaa kwenye kiti. Nakushukuru sana, wewe ni Spika bora kabisa.

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Mussa Azan Zungu kwa *style* yake maalum ya kuliongoza Bunge. Pongezi kwa Mheshimiwa Naibu Spika wa Bunge kwa namna anavyokusaidia ipasavyo katika kuliongoza Bunge letu Tukufu na *style* yake, uongozi wenu unahakikisha kuwa majukumu ya Bunge yanafanyika kwa ufanisi na majadiliano yanakuwa ya manufaa kwa maendeleo ya Taifa letu. Tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia afya njema, nguvu na hekima ili mwendelee kulitumikia Taifa letu

Mheshimiwa Spika, aidha, nampongeza sana Ndugu Baraka Leonard, huyu Katibu wa Bunge hana maneno mengi, lakini Bunge limetulia. Pongezi kwa Katibu wa Bunge kwa usimamizi bora wa utendaji wa Bunge, anasimamia vizuri utendaji na Bunge letu limetulia, na ninyi wote ni mashahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge pamoja na Kamati ya Uongozi kwa kazi kubwa ya kumsaidia Mheshimiwa Spika katika kuongoza Bunge hili. Nikisema Kamati ya Uongozi, maana yake ni Wenyeviti wote wa Kamati na Wajumbe wao.

Mheshimiwa Spika, sambamba na salamu hizo za pongezi kwenu viongozi wetu wa Serikali na Bunge, naomba pia nitumie fursa hii adhimu kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Steven Masatu Wassira, mkongwe wa siasa kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, pamoja na Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa CCM kuwa Mgombea Mwenza wa Kiti cha Urais katika uchaguzi Mkuu ujao. Namwomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki viongozi wetu na wagombea hawa.

Mheshimiwa Spika, naungana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hiyo ya Kudumu ya Utawala, Katiba na Sheria; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya Ukimwi; na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa michango yao ambayo imekuwa na msaada mkubwa katika kuboresha bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, pamoja na bajeti ya Mfuko wa Bunge. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote walioshiriki katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa nawashukuru viongozi wenzangu kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu. Napenda kumpongeza sana Mheshimiwa mdogo wangu Ridhiwani Jakaya Kikwete, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Watu wenye Ulemavu, kwa kazi nzuri anayoifanya. Ni mdogo wangu sana, na ninyi watu wa Chalinze mjue kwamba huyu kijana anafanya kazi kubwa sana. Msije mkauza bunduki mkanunua rungu.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mheshimiwa Ummy Hamis Nderiananga, Naibu Waziri wangu katika Ofisi yangu ya Sera, Bunge na Uratibu, pamoja Mheshimiwa Patrobas Paschal Katambi, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Watu Wenye Ulemavu kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Sote tunatoa ushirikiano mkubwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Jim Jonas, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; Mary Maganga, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu; Dkt. James Kilabuko, Naibu Katibu Mkuu na Ndugu Zuhura Yunus Abdallah, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira; Wakurugenzi na Wakuu wa Idara wote wanaotusaidia katika kutekeleza majukumu chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru na wadau mbalimbali ambao wanatusaidia na wanashiriki na sisi katika kutekeleza majuku yetu katika ofisi zetu.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Ismani na Watanzania kwa ujumla kwa imani kubwa wanayoendelea kuwa nayo kwangu na kwa Chama cha Mapinduzi. Pia, nawashukuru kwa kuendelea kuniamini kuwa mwakilishi wao na kuniunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku. Naomba ushirikiano huo uendelee.

Mheshimiwa Spika, naelewa kuwa dhamana waliyonikabidhi ni kuwahudumia na kuwatumikia kwa moyo na uaminifu, uwazi na uwajibikaji. Ninaahidi kuendelea kushirikiana nao kwa karibu kama walivyonizoea kusikiliza changamoto zao na kuzitatua kwa bidii na hekima. Ombi langu kwao ni lile lile, kwamba mwezi Oktoba mwaka huu 2025 tumpatie kura nyingi za "ndiyo" Mgombea Urais aliyedhaminiwa na Chama cha Mapinduzi. Kwa sababu hata mimi Mbunge wao bila yeye nisingesimama hapa.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu kwa familia yangu ambayo imekuwa nguzo imara katika maisha

yangu binafsi na safari yangu ya kisiasa inayoongozwa na mke wangu mpendwa Germina Lukuvi. Natambua kwamba mafanikio yangu yasingewezekana bila uvumilivu, maombi na *support* yao ya hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na Mheshimiwa Waziri Mkuu kutoa pole kwa wananchi walioathirika na majanga mbalimbali, ikiwemo mafuriko yanayotokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini kote.

Mheshimiwa Spika, vilevile nawashukuru wananchi na wadau wote ambao wanashirikiana Serikali katika kukabiliana na majanga hayo na kutoa misaada kwa waathirika. Moja ya eneo lililopata majanga haya hivi karibuni, ni Jimbo la Ismani. Tarafa ya Pawaga, ambapo Mheshimiwa Waziri Mkuu alielekeza Ofisi yangu itoe msaada na iende ikashirikiane na wananchi wa Pawaga.

Mheshimiwa Spika, nadhani mliwaona wasaidizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu wakifika huko na kutoa msaada. Hiyo ndiyo Ofisi inayosimamiwa na Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa. Tumekwenda pia sehemu mbalimbali kama vile Musoma, Hanang na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, baada ya salamu hizo, naomba nitoe ufafanuzi kidogo katika maeneo machache. Kwa Tume ya kudhibiti UKIMWI, *TACAIDS*, kulikuwa na hoja ambazo zimeulizwa na Waheshimiwa Wabunge juu ya Serikali kuongeza kasi ya elimu na kuhamasisha wananchi kupima ili kujua hali zao za maambukizi. Ushauri umepokelewa.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ilisema kwamba Serikali iendelee kutoa elimu kuhusu upimaji wa virusi vya UKIMWI na kuhamasisha matumizi ya dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI hususani kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuchukua hatua Madhubuti za kueleimisha jamii hususan vijana kuhusu VVU na UKIMWI pamoja na matumizi ya dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI. Hizo hatua nadhani wote kwa sasa tunazijua.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Joseph Mhagama (Mwenyekiti), Kamati ilitoa hoja kwamba Serikali ijiwekee malengo ya ukusanyaji maduhuli ambayo yanaakisi uwezo wa ukusanyaji wa hali halisi ya vyanzo vya mapato. Ufafanuzi wa hoja; Ofisi ya Waziri Mkuu ilikadiriwa kukusanya mapato ya shilingi bilioni 12 kwa mwaka huu unaoishia mwezi Juni. Makusanyo hayo yamezingatia uhalisia na uwezo wa vyanzo vilivyopo ikilinganishwa na makadirio ya shilingi bilioni 19 kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Zakaria na Waheshimiwa Wabunge wengine wametoa hoja kuwa, Serikali ihakikishe kwamba fedha za miradi namba 4.4.2.9 (Programu ya Kilimo na Uvuvi unatekelezwa kikamilifu ili kuwa na tija kwa Taifa. Tumetoa semina kwa Kamati, lakini tunakubaliana na hoja hii. Tutaendelea kusimamia hili jambo ili liwe na tija.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hoja hizi zilizotolewa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, sisi wote kama Bunge tunajua kuwa moja ya kazi kubwa tunayoifanya hasa ofisi yangu katika kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu ni uratibu wa shughuli za Serikali na Bunge.

Mheshimiwa Spika, leo mchana tumeshuhudia Waheshimiwa Mawaziri wakitoa hoja na kujibu baadhi ya hoja za kisekta. Sisi kazi yetu ni kuratibu. Kwa hiyo, nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wote kwa michango yao yote waliyoitoa ambayo imepokelewa vizuri sana na Waheshimiwa Wabunge, wananchi na Watanzania. Michango ambayo imeboresha na kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge ambao walikuwa wanachangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, michango yao ndiyo michango yetu katika ofisi yetu kwa sababu sisi kazi yetu hatufanyi, wanafanya wao, lakini sisi tunafanya kazi ya uratibu, nataka kuwahakikishia kuwa mkiona yale mengine hayakujibiwa, watayajibu kwenye hotuba zao kwa sababu wote mtawasikiliza sasa. Baada ya Waziri Mkuu kutoa mwongozo leo, kila Waziri atasimama hapa kueleza

sekta yake, na bado watajibu hoja zenu zilizobaki kutokana na hotuba zao.

Mheshimiwa Spika, nnaomba nishukuru sana ushirikiano wa idara mbalimbali; Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya wanafanya kazi kubwa na ninyi mashahidi. Vilevile, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Bunge, nimeshasema hapa, likiongozwa na Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wake, Wenyeviti wa Kamati na Sekretarieti yake ikiongozwa na bingwa kabisa Katibu wa Bunge, ndugu yetu Baraka. Nawapongeza sana kwa sababu mimi ni sehemu yao.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Kamishina na ninajua Wajumbe wa Kamisheni tunavyofanya kazi, ninawashukuru sana. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Uongozi, najua tunavyowajibika kumsaidia Mheshimiwa Spika. Nawaomba tu tuendelee kumsaidia Mheshimiwa Spika, kama mnavyomjua ili aweze kutimiza majukumu yake, lakini pia tumwombee ili huku Mbeya waendelee kumwelewa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba nihitimishe tu kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote na kuwatakia kila la heri. Huu ni mwanzo tu wa kusoma bajeti, na hii ni bajeti ya kwanza. Kwa hiyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge muwe wavumilivu, sasa kazi imeanza.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa Wizara zitakuja kueleza mafanikio ya Dkt. Samia Suluhu Hassan katika miaka minne ya utekelezaji na kutoa taarifa kwa wananchi wa Tanzania kupitia kwenu. Mtapewa nafasi ya kutoa ushauri kwa Serikali pamoja na haya ambayo yamesemwa leo na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, huu ni mwanzo tu, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu amefungua mlango, na sasa ndiyo kazi imeanza, tunaanza kusikiliza hoja mbalimbali za Wizara. Waheshimiwa Wabunge, mtapata nafasi ya kusikiliza na kutoa michango yenu kwa niaba ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kurudia shukrani zangu tena kwa…

**SPIKA:** Dakika moja, malizia Mheshimiwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** …kwa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na viongozi wote kitaifa pamoja na Waheshimiwa Wabunge. Nataka kuwahakikishia ushirikiano wenu mkubwa katika kutimiza majukumu yenu mkiwa hapa Bungeni na sehemu nyingine, kwa sababu kwa upande wa Serikali, mimi ndiye msaidizi wenu ninayefanya shughuli za Bunge pamoja na shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uvumilivu wa kutuvumilia sana sisi wasaidizi wake, na ninawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge. Shukrani mlizompatia Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni za kweli. Ni mtu msikivu, yuko hivyo hivyo. Huwa naona hapa hata akina Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, wanamuudhi hapa nyuma, lakini hakasiriki. Huwa wanakuja kumchokoza hapa…

**SPIKA:** Haya, ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya maelezo haya mafupi, nakushukuru sana na ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kuipokea vizuri hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja na kuunga mkono. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Mjaliwa Majaliwa, aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana, nawashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutuwezesha kukutana katika siku hii muhimu ya kuhitimisha mjadala wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake na Mfuko muhimu wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2025/2026 tukiwa buheri wa afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku ya tarehe tisa mwezi huu wa Nne nilipokuwa nawasilisha hoja hii, nilikupongeza sana ukiwa haupo. Nirudie leo kukupongeza sana wewe mwenyewe binafsi kwa kazi nzuri unayoifanya ya kuliongoza Bunge hili kwa weledi mkubwa na umahiri mkubwa. Watanzania wanajua, Wanambeya nao wanajua. Nakuombea kila la heri ili uendelee kutekeleza majukumu yako kwa tabia hiyo hiyo, weledi huo huo na umahiri ulionao.

Mheshimiwa Spika, wewe pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge mmefanya kazi nzuri kwa kipindi chote cha miaka minne kuliongoza Bunge hili kwa umahiri mkubwa na weledi mkubwa. Wamesimamia mijadala kuhusu hoja mbalimbali na wamesimamia mjadala juu ya hoja ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, taasisi zake na Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana ndugu yetu Komredi Baraka, Katibu wa Bunge na watumishi wote wa Bunge kwa kazi nzuri ya kutoa huduma zinazowezesha Bunge hili kutekeleza majukumu yake vizuri. Hongera sana na tunamkushukuru sana Komredi Baraka.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru na kuwapongeza Wenyeviti na Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kwa michango yao. Ni ukweli usiopingika kwamba, maoni pamoja na ushauri wao wakati wote umekuwa ukileta manufaa makubwa kwenye hoja ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko, Mbunge, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa usaidizi wake muhimu na mzuri. Hakika yeye pamoja na Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; kwa pamoja na Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Ajira, Vijana na Wenye ulemavu, wameendelea kutumikia vizuri Ofisi yetu ya Waziri Mkuu na ushauri wao umeendelea kuleta masilahi mapana.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuendelea kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Johari Hamza, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushauri wake na miongozo yake ya kisheria ndani ya Serikali yetu. Hakika mpaka sasa tunaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, vilevile namshukuru Mheshimiwa Ummy Nderiananga, Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulia Sera, Bunge na Uratibu kwa pamoja na Mheshimiwa Patrobas Katambi, Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mawaziri wote wa sekta, Naibu Mawaziri kwa kuchangia hoja ya Waziri Mkuu wakati wa mjadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika nawashukuru Makatibu Wakuu. Nianze na Mheshimiwa Dkt. Jim Jonas, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; na Bi. Mary Maganga, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Wameungana pamoja na Naibu Makatibu Wakuu akiwemo Dkt. James Kilabuko anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge na Uratibu na Bi. Zuhura Yunus anayeshughulikia Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu. Wakuu wote wa idara, taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Wakala wa Serikali kwa ushirikiano mkubwa na kujitoa kwao katika kufanikisha majibu ya hoja za Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, watumishi wa taasisi zote na Ofisi ya

Bunge kwa kujituma na kufanya kazi kwa weledi mkubwa kuanzia kipindi cha maandalizi ya hotuba ya bajeti hadi leo tunapohitimisha mjadala huu wa hoja ya Waziri Mkuu. Ahsanteni sana kwa kuifanya kazi yenu vizuri na kuufanya mwenendo shughuli za Ofisi ya Waziri Mkuu kuwa mwepesi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dhati ya moyo wangu, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa michango yenu. Hoja na michango yenu imekuwa muhimu sana kwenye ofisi yetu na kwa hakika inaakisi maeneo yote muhimu yaliyohitaji kuimarishwa zaidi katika suala zima la kuhudumia wananchi na kufanya uboreshaji kwenye utendaji wa Serikali na namna ya kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali imezingatia michango yao na katika utekelezaji itatoa kipaumbele kama ambavyo imeainishwa katika Mpango wa Bajeti wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge 103 walichangia mjadala wa hoja ya Waziri Mkuu. Kati yao 100 walichangia kwa kuzungumza na watatu walichangia kwa maandishi. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja ya Waziri Mkuu. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda, naomba uridhie nisiwataje moja kwa moja kwa majina yao na badala yake majina yao yaingizwe kwenye *Hansard. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati tukiendelea na mjadala wa hoja ya Waziri Mkuu, sote tumewasikia Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri, wakitoa majibu na ufafanuzi wa hoja nyingi zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa baadhi ya hoja zinaendelea kufanyiwa kazi na Waheshimiwa Mawaziri, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali itawasilisha majibu yote ya hoja ambazo zimekuja mbele yenu na wamezitoa kwa maandishi kwa wakati wote tutakapokuwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwanza kwa kutimiza miaka minne ya kuiongoza nchi yetu kwa mafanikio makubwa. Pili, nyote ni mashahidi kuwa katika kipindi Cha miaka minne ya uongozi wake, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi imetekelezwa kwa kiwango kikubwa kama ilivyoelezwa wakati nikiwasilisha hoja ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa pamoja na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kumsaidia vyema Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutekeleza majukumu yake na hasa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (Chama Tawala) ambacho kwa sasa kiko madarakani.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kukumbusha baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hiki cha miaka minne ya uongozi wake na mafanikio hayo ni pamoja na haya yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Sambamba na kudumisha hali ya amani, utulivu, pamoja na mshikamano wa wananchi wa Taifa hili, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amewezesha utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mafanikio makubwa yamepatikana katika utekelezaji wa miradi ya huduma za jamii na miradi ya kimkakati, hususan katika sekta za elimu, afya, maji, kilimo, ujenzi, nishati, mawasiliano na uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, mafanikio hayo tunayoyapata katika utekelezaji wa ilani, ni ya kupigiwa mfano. Bila shaka kila mwananchi ni shahidi wa jambo hili. Kila eneo katika nchi hii limefikiwa na wananchi wamekuwa mashahidi kwa miradi

inayotekelezwa kwenye maeneo yao. Hakika Mheshimiwa Rais anastahili pongezi na tumpongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuboresha sera na sheria mbalimbali ili kuweza kuweka mazingira bora ya kuwawezesha wananchi kiuchumi. Suala la sera na sheria limewezesha kutenga 30% ya manunuzi ya umma kwa wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu. Pia, kuratibu na kuweka mazingira bora kwa vikundi na huduma ndogo za kifedha pamoja na kuongeza ushiriki wa Watanzania katika uwekezaji ikiwemo sekta ya madini, mafuta na gesi.

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa mifuko ya programu mbalimbali za uwezeshaji wananchi unatokana na mahitaji ya kiuchumi kwa maendeleo ya nchi yetu. Mifuko iliyopo imeweza kutoa jumla ya shilingi trilioni 3.5 kwa wanufaika zaidi ya milioni 24. Kati ya wanufaika hao, wanawake ni zaidi ya milioni 11 na wanaume ni zaidi ya milioni 13.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mifuko ya programu hizo ni pamoja na mikopo ya halmashauri ya 10% kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu. Pia, ipo Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora na Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi kwa Vijana. Tunayo Programu za Kukuza Viwanda Vidogo na Kati, Programu ya Kuimarisha Uchumi na Mama Samia na Mfuko wa Dhamana wa Wajasiriamali Wadogo.

Mheshimiwa Spika, mifuko na programu za uwezeshaji wananchi zinazoratibiwa na Serikali zinatoa fursa ya mikopo kwa riba nafuu kwa mtu mmoja mmoja na vikundi na uzalishaji mali. Serikali itaendelea kutekeleza na kusimamia mikakati ya kutoa elimu kwa wananchi kupitia njia mbalimbali ikiwemo maonesho, makala, vyombo vya habari na vituo vya uwezeshaji ili kuongeza uelewa kuhusu fursa zilizopo kwenye mifuko na programu hizo.

Mheshimiwa Spika, la tatu ni mifumo ya utoaji haki. Kama nilivyoelekeza kwenye hotuba yangu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

amekuwa kinara katika kuboresha misingi ya utoaji haki hapa nchini. Aidha, ameimarisha mifumo ya utoaji haki hususan matumizi ya TEHAMA kwenye taasisi za hakijinai.

Mheshimiwa Spika, mifumo hii imerahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati, kupunguza gharama kwa wananchi wanyonge na wasiokuwa na uwezo wa kupata huduma za Kimahakama hasa waliopo kwenye maeneo ya pembezoni. Kwa wakati huu tunaendelea na mkakati wa huduma za kisheria zinazotolewa bure kwa Watanzania kote nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Mheshimiwa Rais ameongeza idadi ya Waheshimiwa Majaji wa Mahakama Kuu pamoja na Mahakama za Rufani. Ongezeko hilo linachangia moja kwa moja katika kupunguza mlundikano wa kesi, hivyo, kurahisisha utoaji haki. Hali kadhalika amefanya maboresho ya miundombinu ya Mahakama kuanzia ngazi ya Mahakama ya Mwanzo hadi Mahakama Kuu ikiwemo ujenzi wa Mahakama pamoja na nyumba za Majaji.

Mheshimiwa Spika, mtakumbuka mnamo tarehe 05 Aprili, mwaka huu 2025 Mheshimiwa Rais aliweka historia kwa kuzindua jengo la kwanza la Makao Makuu ya Mhimili wa Mahakama ya Tanzania kwa kipindi cha miaka 104 tangu kuanzishwa kwake. Uzinduzi huo ni mwendelezo wa dhamira yake njema ya kuboresha miundombinu ya Mahakama hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo la nne ni ukusanyaji wa mapato, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mafanikio yaliyopatikana katika miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Ukusanyaji huo umewezesha utekelezaji wa miradi mbalimbali hapa nchini. Mathalan, katika kipindi cha mwezi Julai hadi Machi mwaka wa fedha 2024/2025 Mamlaka ya Mapato Tanzania imekusanya kiasi cha shilingi trilioni 24.05, sawa na ufanisi wa 103.62% ya lengo letu.

Mheshimiwa Spika, aidha, makusanyo hayo ni ya kiwango cha juu kabisa kufikiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa

kipindi kama hicho tangu kuanzishwa kwake. Kiasi hicho ni sawa na ongezeko la 77% ikilinganishwa na kiasi cha shilingi trilioni 13.59 zilokusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, ufanisi katika makusanyo uliofikiwa ni matokeo chanya ya kutekeleza kwa vitendo maagizo na maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kuboresha mazingira ya ulipaji kodi. Serikali inawapongeza walipakodi nchini kwa kutimiza wajibu wenu, kwa kulipa kodi stahiki kwa wakati bila shuruti na kuendelea kuunga mkono kizalendo juhudi za Serikali za kuleta maendeleo nchini kwani kodi yetu ndiyo maendeleo yetu. Pongezi nyingi kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa wafanyakazi wamekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa letu. Nitumie fursa hii kuwapongeza kwa dhati wafanyakazi wote nchini. Vilevile, nawapongeza waajiri, viongozi, vyama vya wafanyakazi na wadau wote kwa kuendelea kuheshimu haki na utu wa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuwahakikishia kuwa Serikali itaendelea kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania *(TUCTA)* na Chama cha Waajiri Tanzania *(ATE)* katika kuhakikisha kuwa misingi ya haki ya wafanyakazi inazingatiwa. Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba wafanyakazi wataendelea kupata stahiki zao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, hili ninalizungumza kwa sababu mafanikio yote ya Serikali yanatokana na kazi kubwa inayofanywa na wafanyakazi hawa kwenye sekta ya umma na sekta binafsi. Kwa sasa tunafanya maandalizi ya maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) yatakayofanyika siku ya tarehe 01 Mei ambayo yanafanyika kila mwaka, na mwaka huu maadhimisho hayo Kitaifa yanatarajiwa kufanyika Mkoani Singida.

Mheshimiwa Spika, maadhimisho hayo siyo tu kielelezo cha mshikamano na heshima kwa wafanyakazi, bali pia

yanadhihirisha dhamira ya dhati ya kuhamasisha utoaji haki za wafanyakazi, ustawi, mazingira bora ya wafanyakazi na kupokea changamoto za wafanyakazi kupitia maandamano yatakayopita mbele ya mgeni rasmi.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa wafanyakazi wote nchini kuendelea kufanya kazi kwa bidii, weledi, maarifa, uadilifu na kwa moyo wa kujituma katika kuwapokea, kuwasikiliza na kuwahudumia wananchi kwa wakati. Hivyo, nawatakia kila la heri katika kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie ajenda mbili zilizopo mbele yetu kwa sasa. Kwanza, matumizi ya nishati safi, sote tunafahamu kuwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa kinara kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia. Jitihada zake na hatua mbalimbali anazochukua zimeongeza hamasa kwa nchi yetu katika matumizi ya nishati safi. Hakika anastahili pongezi kwa maono yake na sasa tuko kwenye kampeni ya kuhakikisha kwamba Watanzania wanabadilisha matumizi kutoka nishati chafu kwenda nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Spika, tulianza na taasisi na sasa tunaenda mtu mmoja mmoja. Kufikia mwaka 2033 ni matarajio yetu kwamba Watanzania wote watakuwa wanapikia nishati safi kwa 80%. Tumeshuhudia Waheshimiwa Wabunge mkishiriki katika kuhamasisha na kugawa mitungi ya gesi ya kupikia kwa wananchi kwenye maeneo yenu. Hongereni sana Waheshimiwa Wabunge kwa jitihada hizo za kuhamasisha wananchi kutumia nishati safi ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ziara nilizozifanya maeneo mbalimbali nchini, nimeshuhudia baadhi ya taasisi zikitumia nishati safi ya kupikia kama ilivyoelekezwa na Serikali. Hata hivyo, taasisi nyingine hazijatekeleza maelekezo hayo. Hivyo, nitumie nafasi hii kusisitiza taasisi zote zenye kuandaa chakula cha watu zaidi ya 100 kuhamia kwenye matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii ya Bunge lako Tukufu kuwakumbusha wadau wote ikiwemo Wizara za Kisekta, taasisi za

umma, Tawala za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, sekta binafsi na Watanzania wote kuendelea kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mkakati wa matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Spika, vilevile, taasisi za Serikali zihakikishe matumizi ya mapato yanayotokana na uvunaji wa miti, usafirishaji na biashara misitu yanaelekezwa katika kufanikisha mkakati huu wa uhifadhi wa mazingira. Kwa upande mwingine, nitoe wito kwa wananchi kuendelea kuunga mkono jitihada za Serikali kuhamia kwenye matumizi ya nishati safi.

Mheshimiwa Spika, ajenda ya pili, maandalizi ya Uchaguzi Mkuu ambapo Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi imeshakamilisha uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura awamu ya kwanza katika mikoa yote 31 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nitumie nafasi hii kuwapongeza Watanzania, hakika wamejitokeza kwa wingi kwenye zoezi hilo kwa ajili ya kujiandikisha na kufanya maboresho ya taarifa zao.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea na maandalizi hayo, Tume inatarajia kufanya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura kwa awamu ya pili mwezi Mei. Hatua hiyo itaenda sambamba na zoezi la uwekaji wazi wa daftari kwa ajili ya kuwawezesha wapigakura ambao wameandikishwa kukagua taarifa zao kwenye kuta za matangazo.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, nitoe rai kwa Watanzania waliopitiwa na zoezi la awamu ya kwanza kutumia fursa hiyo kwenda kujiandikisha na kuboresha taarifa zao awamu ya pili pindi Tume itakapotangaza.

Mheshimiwa Spika, nawasisitiza wapigakura ambao tayari wameandikishwa waende kwenye vituo vya kuhakiki majina yao kwenye madaftari ambayo wamewekwa wazi. Tume imekamilisha maandalizi ya kanuni za uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka huu 2025.

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Maadili ya Uchaguzi za Mwaka 2025 na maelekezo mbalimbali ya uchaguzi yametolewa. Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa kuna hali ya usalama, amani, utulivu, uwazi na haki katika kipindi chote cha uchaguzi mpaka siku ya upigaji kura.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijibu hoja chache ambazo zimejitokeza na ambazo hazikuguswa na Waheshimiwa Mawaziri. Natambua kuwa Waheshimiwa Wabunge wametoa hoja nyingi na zote ni za muhimu kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Hoja nyingi zimetolewa ufafanuzi na Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri wakati walipokuwa wanachangia hoja zao.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa muda, baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge zitajibiwa kwa maandishi na nyingine zitatolewa ufafanuzi na Waheshimiwa Mawaziri wakati watakapokuwa wanawasilisha bajeti zao za Wizara zao, ambapo pia nao watawajibika kujibu hoja mbalimbali pamoja na zile ambazo hazikupata nafasi kujibiwa kupitia hotuba yangu hapa.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo juu ya utoaji wa fedha kwa wakati. Fedha ambazo zimeenda kufanya maendeleo na matumizi mengi na kuziwezesha Wizara, Taasisi na Idara za Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Serikali yetu imeendelea kutoa fedha ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo na matumizi mengine. Sote tumeshuhudia utekelezaji wa miradi mbalimbali kutokana na fedha zilizotolewa kwenye maeneo yetu ya uwakilishi.

Mheshimiwa Spika, hivyo, nilihakikishie Bunge lako Tukufu kuwa kulingana na mpango kazi, Serikali itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na tumebaki na miezi mitatu ya kukamilisha bajeti yetu. Tutahakikisha robo hii ya mwaka iliyobaki tunamalizia kupeleka fedha kulingana na mahitaji ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili juu ya uharibifu wa miundombinu iliyoharibika kutokana na mvua, kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu kuwa nchi yetu imepata athari kubwa

kutokana na mvua kubwa za *El-Nino* na Kimbunga Hidaya, athari zilizojitokeza ni pamoja na vifo, majeruhi, upotevu na uharibifu wa mali pamoja na miundombinu hususan barabara, madaraja, ma-*culvert*.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilichukua hatua mbalimbali za kurejesha hali ya miundombinu hiyo iliyoharibika ili huduma nyingine ziweze kuendelea. Hatua hizo ni pamoja na kutafuta fedha za dharura, kuweka mfumo wa manunuzi na kutafuta wakandarasi na kuanza ujenzi wa miundombinu iliyoharibika katika mikoa yote hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa shilingi bilioni 72.15 kwa ajili ya kurejesha miundombinu ya dharura. Vilevile, imetoa shilingi bilioni 868.56 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kudumu kwenye wilaya 139 za Tanzania Bara ambapo miundombinu yake iliharibiwa kabisa. Miundombinu hiyo inajumuisha madaraja 63, barabara zenye urefu wa kilometa 827, mitaro yenye urefu wa kilometa 84, na ma-*culvert* 225 yamefanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumeshuhudia mvua kubwa kwenye mikoa mbalimbali hapa nchini. Mvua hizo zimesababisha athari kwenye miundombinu ikiwemo Barabara ya Dar es Salaam hadi Lindi. Miundombinu hiyo ni pamoja na daraja la dharura lililopo kwenye barabara ya mchepuko katika eneo la Somanga ambapo daraja jipya linajengwa.

Mheshimiwa Spika, napenda niwafahamishe Watanzania na Waheshimiwa Wabunge wote wakiwemo Wabunge wa Mikoa ya Kusini kuwa ujenzi wa Daraja jipya la Somanga ambalo litakuwa na urefu wa meta 60 pamoja na barabara unganishi ya kilometa 1.7 unaendelea vizuri na haujaathirika. Hadi sasa mkandarasi amekamilisha ujenzi wa nguzo 27 kati ya 43 wa Daraja hilo na kwa ujumla mradi umefikia 38% ya utekelezaji na unatarajiwa kukamilika ifikapo Septemba, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mkataba, madaraja mengine yanayopitiwa na mikondo ya maji kama vile Matandu, Mavuji, Nakiu na Mto Mbwemkuru yana wakandarasi, pindi mvua

hizi zinazoendelea kunyesha kutoka Mkoani Morogoro na Misitu ya Selous zikishapungua ujenzi utaendelea kwa kasi. Kesho asubuhi saa mbili nitakuwa kule Somanga kukagua hali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kuwahakikishia wananchi kuwa Serikali itaendelea kukamilisha miundombinu iliyoharibiwa ili irejee katika hali yake ya kawaida na wananchi waendelee na huduma zao za kawaida. Vilevile, nitoe rai kwa wananchi wote kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya mvua zinazoendelea kunyesha ili kuepuka athari zinazoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie sherehe za Muungano. Tarehe 26 Aprili, 2025 tutaadhimisha miaka 61 ya Muungano wa nchi yetu ambao umeendelea kuwa chachu ya mafanikio tunayoyashuhudia leo. Nchi yetu iliungana pamoja na viongozi wetu shupavu, yaani Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Sheikh Abeid Amani Karume kuona haja ya kuliunganisha Taifa letu ili kuweza kuipata Tanzania yenye nguvu tunayotaka na tunayoiona leo.

Mheshimiwa Spika, maadhimisho ya mwaka huu yatakuwa na kauli mbiu, "Miaka 61 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Muungano wetu ni Dhamana, Heshima na Tunu ya Taifa; Shiriki Uchaguzi Mkuu mwaka 2025." Hivyo, niungane na Watanzania wenzangu kuliombea heri na fanaka, Taifa letu huku nikiendelea kuwasihi kudumisha umoja, mshikamano na amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawaomba Watanzania wote, kutumia sherehe hizi katika kukumbushana na kuelimishana juu ya umuhimu wa uwepo wa Muungano huu. Tuulinde na tuutetee. Muungano huu unaenda kulinda amani yetu, umoja na undugu wetu kwa pamoja na kufanya kazi kwa bidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo, nchi yetu imeendelea kupiga hatua katika medani za michezo kwa kuweza kufuzu katika mashindano mbalimbali ambayo yameijengea heshima nchi yetu. Kupitia uwekezaji uliofanywa na mwanamichezo nambari moja nchini, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, umeziwezesha timu zetu za Taifa kufuzu katika mashindano mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara yenye dhamana na michezo, Baraza la Michezo Tanzania na vyama vyote vya michezo nchini kwa kusimamia maono ya Mheshimiwa Rais. Maono hayo yamewezesha timu za Taifa kufuzu na kushiriki mashindano mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *Taifa Stars* imefuzu *AFCON* 2025, *Taifa Stars* hiyo hiyo imefuzu michezo ya *CHAN* 2025. *Twiga Stars* imefuzu mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa wanawake inayoitwa *WAFCON*. *Ngorongoro Heroes* chini ya miaka 20 wamefuzu *AFCON* 2025. *Serengeti Boys* chini ya miaka 17 wamefuzu *AFCON* mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, Timu ya Taifa ya Mpira Ufukweni imefuzu *BSFCON* 2024. Kushiriki mashindano ya *Futsal* ya wanawake yanayofanyika nchini Morocco na kufuzu kwa Timu ya Taifa ya *Cricket* chini ya miaka 19 katika mashindano ya Kombe la Dunia. Tujipongeze wenyewe kwa matokeo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ni mafanikio makubwa sana kwa nchi yetu. Sote tunapaswa kujivunia hatua hii na kuendelea kumuunga mkono Rais wetu ambaye ameonesha nia thabiti ya kuhakikisha kwamba Taifa letu linapata heshima kupitia michezo.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu kama ambavyo uliniruhusu siku ya tarehe 9 Aprili, 2025 nilipokuwa nasoma Hotuba ya Bajeti na ilikuwa ndiyo siku Timu ya Simba ilikuwa inacheza mchezo wa robo fainali na niliitakia heri kwenye mchezo wao. Nitumie nafasi hii sasa niwapongeze wawakilishi pekee wa nchi yetu na ukanda wa Afrika Mashariki na Kati waliosalia kwenye michuano mikubwa ya Kimataifa Barani Afrika, *(CAF - Confederation Cup)* timu ya *Simba Sports Club* toka Mtaa wa Msimbazi Jijini Dar es Salaam kwa kufuzu hatua ya nusu fainali kwa kuiondosha timu ngumu ya Al-Masry kutoka nchini Misri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa, naomba nimpongeze mlinda mlango wa Simba Moussa Pinpin Camara kwa kuokoa mikwaju miwili mizito ya penati iliyoiwezesha Simba kushinda. Naipongeza sana Timu ya Simba kwa ushindi huu na tunawatakia heri katika mechi inayofuata ya nusu fainali, na nina imani watafika hatua ya fainali na hatimaye kutwaa ubingwa kwa mara ya kwanza kwa kaulimbiu iliyosema, "Hii Tutavuka" na sasa kauli ya kuingia nayo kwenye mashindano ya nusu inasema, "Hatuishii Hapa." Hiyo ndiyo kaulimbiu mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nitoe shukrani kwa Bunge lako Tukufu. Ninapoelekea kuhitimisha niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuturuzuku rehema ambayo tumeipata ya kujenga utulivu, kusikilizana na kuweza kujadiliana kwa misingi iliyozingatia umoja, mshikamano na kuheshimiana.

Mheshimiwa Spika, Bunge hili limetia fora, limejenga heshima na limejijengea historia kubwa ya kuweza kujadili masuala mbalimbali ya Kitaifa kwa ushauriano mkubwa kwa heshima ya hali ya juu na kuhakikisha kwamba Taifa letu linasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, kipekee narudia tena kukushukuru na kukupongeza wewe mwenyewe, Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kusimamia vema majadiliano na hoja hii. Pia namshukuru Katibu wa Bunge na Watumishi wa Bunge kwa huduma nzuri pia na Waheshimiwa Wabunge wenyewe kwa michango yenu kwa kuishauri Serikali na Serikali pia kupitia Mawaziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wetu ndani ya Serikali kwa kupokea ushauri na kuutekeleza vilivyo na hatimaye kuifanya Serikali kuwa Serikali pendwa. Hakika usimamizi wa miongozo yenu imeweza kuhitimisha mjadala huu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru kwa dhati ya moyo wangu tena Wabunge wenzangu wote kwa namna ambavyo mmeweza kuijadili hoja hii na kujitoa kwenu katika kuishauri Serikali. Maoni na ushauri mlioutoa umepokelewa kwa uzito mkubwa kabisa na Serikali itayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu liridhie na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi zilizo chini yake na Mfuko wa Bunge kama nilivyowasilisha katika hoja yangu ya tarehe 09 Aprili, 2025.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MAELEZO YA MHESHIMIWA KASSIM MAJALIW A MAJALIWA (MB.), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA KUHITIMISHA HOJA YA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU, TAASISI ZAKE NA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA 2025/2026 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**UTANGULIZI**

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana katika siku hii muhimu ya kuhitimisha mjadala wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi zake na Mfuko wa Bunge kwa Mwaka 2025/2026 tukiwa buheri wa afya.

**2.** ***Mheshimiwa Spika***, ninakupongeza sana Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuongoza kwa umahiri na weledi mkubwa mjadala kuhusu hoja ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi zake na Mfuko wa Bunge, kwa mwaka 2025/2026.

**3.** ***Mheshimiwa Spika***, aidha ninawashukuru na kuwapongeza Wenyeviti na wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kwa michango yao. Ni ukweli usiopingika kwamba maoni pamoja na ushauri wao wakati wote umekuwa ukileta manufaa makubwa kwenye Hoja ya Waziri Mkuu.

**4.** ***Mheshimiwa Spika*,** ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.) Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi (Mb.) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete (Mb.), Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu).

**5.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, ninawashukuru Mheshimiwa Ummy Nderiananga, Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu); Mheshimiwa Patrobas Katambi, Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu); na Mawaziri wote wa Sekta na Naibu Mawaziri waliochangia Hoja ya Waziri Mkuu.

**6.** ***Mheshimiwa Spika*,** kadhalika, ninawashukuru Makatibu Wakuu *Dkt*. Jim Yonazi (Sera, Bunge na Uratibu) na Bi. Mary Maganga (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Naibu Makatibu Wakuu *Dkt*. James Kilabuko (Sera, Bunge na Uratibu) na Bi. Zuhura Yunus (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Wakuu wa Idara, Taasisi na Wakala wa Serikali kwa ushirikiano mkubwa na kujitoa kwao katika kufanikisha majibu ya Hoja ya Waziri Mkuu.

**7.** ***Mheshimiwa Spika***, kipekee ninawapongeza Watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi zake na Ofisi ya Bunge kwa kujituma na kufanya kazi kwa weledi mkubwa kuanzia kipindi cha maandalizi ya Hotuba ya Bajeti, hadi leo tunapohitimisha mjadala huu wa Hoja ya Waziri Mkuu. Asanteni sana kwa kuifanya kazi yangu iwe nyepesi.

**8.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa dhati ya moyo wangu ninapenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa michango yenu. Hoja na michango yenu ni muhimu sana, na kwa hakika inaakisi maeneo yote muhimu yanayohitaji kuimarishwa zaidi katika suala zima la kuwahudumia wananchi na kuboresha utendaji wa Serikali. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuwa, Serikali itazingatia michango yenu katika utekelezaji wa vipaumbele kama vilivyoainishwa katika Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/2026.

**WACHANGIAJI**

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** Waheshimiwa Wabunge 103 walichangia mjadala wa Hoja ya Waziri Mkuu. Kati yao, Waheshimiwa Wabunge 100 walichangia kwa kuzungumza na Waheshimiwa Wabunge 3 walichangia kwa maandishi.

**10.** ***Mheshimiwa Spika***, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Hoja ya Waziri Mkuu. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda, ninaomba uridhie nisiwataje mmoja mmoja kwa majina na badala yake majina yao yaingizwe kwenye ***Hansard***.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** wakati tukiendelea na mjadala wa hoja ya Waziri Mkuu, sote tumewasikia Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wakitoa majibu na ufafanuzi wa hoja nyingi zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge. Kwa kuwa baadhi ya hoja zinaendelea kufanyiwa kazi na Waheshimiwa Mawaziri, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuwa, Serikali itawasilisha majibu ya hoja hizo kwa maandishi.

**PONGEZI KWA MHESHIMIWA RAIS KWA MIAKA MINNE**

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka minne ya kuiongoza nchi yetu kwa mafanikio makubwa. Sote ni mashahidi kuwa, katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wake, Ilani ya Uchaguzi imetekelezwa kwa kiwango kikubwa kama nilivyoeleza wakati ninawasilisha Hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kukumbusha baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hiki cha miaka minne ya uongozi wake. Mafanikio hayo ni pamoja na yafuatayo:

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO**

**14.** ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na kudumisha hali ya amani, utulivu pamoja na mshikamano wa wananchi wa Taifa hili,

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amewezesha utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Mafanikio makubwa yamepatikana katika utekelezaji wa miradi ya huduma za jamii na miradi ya kimkakati hususan katika sekta za elimu, afya, maji, kilimo, ujenzi, nishati, mawasiliano na uchukuzi.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio hayo tunayoyapata katika utekelezaji wa Ilani ni ya kupigiwa mfano. Bila shaka, kila mwananchi ni shahidi wa jambo hili. Hakika Mheshimiwa Rais anastahili pongezi na tunampongeza sana.

**UWEZESHAJI WA WANANCHI KIUCHUMI**

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuboresha sera na sheria mbalimbali ili kuweka mazingira bora ya kuwawezesha wananchi kiuchumi. Sera na sheria hizo zimewezesha kutenga asilimia 30 ya manunuzi ya umma kwa wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu; kuratibu na kuweka mazingira bora kwa vikundi na huduma ndogo za kifedha; pamoja na kuongeza ushiriki wa Watanzania katika uwekezaji ikiwemo sekta za madini, mafuta na gesi.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** uanzishwaji wa Mifuko na Programu za uwezeshaji wananchi unatokana na mahitaji ya kiuchumi kwa maendeleo ya nchi yetu. Mifuko iliyopo imeweza kutoa jumla ya shilingi trilioni 3.5 kwa wanufaika zaidi ya milioni 24. Kati ya wanufaika hao, wanawake ni zaidi ya milioni 11 na wanaume ni milioni 13.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya Mifuko na Programu hizo ni pamoja na Mpango wa Mikopo ya Halmashauri wa asilimia 10 kwa Wanawake, Vijana na Wenye Ulemavu; Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT); Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi kwa Vijana; Programu ya Kukuza Viwanda Vidogo na vya Kati; Programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia (IMASA); na Mfuko wa Dhamana wa Wajasiriamali Wadogo.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mifuko na Programu za Uwezeshaji wananchi zinazoratibiwa na Serikali zinatoa fursa ya mikopo kwa riba nafuu kwa mtu mmoja mmoja na vikundi vya uzalishaji mali. Serikali itaendelea kutekeleza na kusimamia mikakati ya kutoa elimu kwa wananchi kupitia njia mbalimbali ikiwemo maonesho, makala, vyombo vya habari na vituo vya uwezeshaji ili kuongeza uelewa kuhusu fursa zilizopo kwenye mifuko na programu hizo.

**MIFUMO YA UTOAJI HAKI**

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa kinara katika kuboresha misingi ya utoaji haki. Aidha, ameimarisha mifumo ya utoaji haki hususan matumizi ya TEHAMA kwenye Taasisi za Haki Jinai. Mifumo hii imerahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati, kupunguza gharama kwa wananchi wanyonge na wasio na uwezo kupata huduma za kimahakama hasa waliopo maeneo ya pembezoni.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Mheshimiwa Rais ameongeza idadi ya waheshimiwa majaji wa Mahakama Kuu pamoja na Mahakama ya Rufani. Ongezeko hilo linachangia moja kwa moja katika kupunguza mrundikano wa kesi na hivyo kuharakisha utoaji haki. Kadhalika, ameboresha miundombinu ya mahakama kuanzia ngazi ya mahakama za mwanzo hadi mahakama kuu ikiwemo ujenzi wa mahakama pamoja na nyumba za majaji.

**22.** ***Mheshimiwa Spika***, mtakumbuka mnamo tarehe 05 Aprili, 2025 Mheshimiwa Rais ameweka historia kwa kuzindua Jengo la kwanza la Makao Makuu ya Mhimili wa Mahakama ya Tanzania kwa kipindi cha miaka 104 tangu kuanzishwa kwake. Uzinduzi huo ni muendelezo wa dhamira yake njema ya kuboresha miundombinu ya mahakama hapa nchini.

**UKUSANYAJI WA MAPATO**

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mafanikio yaliyopatikana katika

miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Ukusanyaji huo umewezesha utekelezaji wa miradi mbalimbali nchini.

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** mathalan, katika kipindi cha mwezi Julai hadi Machi, mwaka wa fedha 2024/2025, Mamlaka ya Mapato Tanzania imekusanya kiasi cha shilingi trilioni 24.05 sawa na ufanisi wa asilimia 103.62 ya lengo. Aidha, makusanyo hayo ni ya kiwango cha juu kabisa kufikiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kipindi kama hicho tangu kuanzishwa kwake. Kiasi hicho ni sawa na ongezeko la asilimia 77 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi trilioni 13.59 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2020/2021.

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** ufanisi katika makusanyo uliofikiwa ni matokeo chanya ya kutekeleza kwa vitendo maagizo na maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuboresha mazingira ya ulipaji kodi. Serikali inawapongeza walipakodi nchini kutimiza wajibu wao kwa kulipa kodi stahiki kwa wakati na kuendelea kuunga mkono kizalendo juhudi za Serikali za kuleta maendeleo nchini kwani "*Kodi Yetu Ndiyo Maendeleo Yetu*".

**PONGEZI KWA WAFANYAKAZI**

**26.** ***Mheshimiwa Spika***, ni dhahiri kuwa wafanyakazi wamekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa letu. Nitumie fursa hii, kuwapongeza kwa dhati wafanyakazi wote nchini. Vilevile, niwapongeze waajiri, viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi na wadau wote kwa kuendelea kuheshimu haki na utu wa wafanyakazi.

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii kuwahakikishia kuwa Serikali itaendelea kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) katika kuhakikisha kuwa misingi ya haki za wafanyakazi inazingatiwa. Serikali itaendelea kuhakikisha wafanyakazi wanaendelea kupata stahiki zao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** maandalizi ya maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani almaarufu "Mei Mosi" yanayofanyika tarehe 01 Mei kila mwaka yanaendelea. Kitaifa, maadhimisho ya mwaka huu yanatarajia kufanyika mkoani Singida. Maadhimisho hayo siyo tu kielelezo cha mshikamano na heshima kwa wafanyakazi bali pia yanadhihirisha dhamira ya dhati ya kuhamasisha utoaji haki za wafanyakazi, ustawi, na mazingira bora ya wafanyakazi nchini.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe wito kwa Wafanyakazi wote nchini kuendelea kufanya kazi kwa bidii, weledi, maarifa, uadilifu na kwa moyo wa kujituma katika kuwapokea, kuwasikiliza na kuwahudumia wananchi kwa wakati. Hivyo, ninawatakia heri katika kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi duniani.

**MATUMIZI YA NISHATI SAFI**

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** sote tunafahamu kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa kinara wa kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia. Jitihada zake na hatua mbalimbali anazochukua zimeongeza hamasa kwa nchi yetu katika matumizi ya nishati safi. Hakika anastahili pongezi kwa maono yake hayo na sasa tuko kwenye kampeni ya kuhakikisha Watanzania wanaacha kutumia nishati chafu, wanahamia kwenye nishati safi. Tumeanza na taasisi, na sasa hivi tunenda kwa mtu mmojammoja.

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kazi kubwa aliyoifanya. Wakati wote amekuwa akitafsiri vema maelekezo ya Serikali na kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee, nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kuwa mstari wa mbele kuhamasisha wananchi kutumia nishati safi ya kupikia. Tumeshuhudia waheshimiwa wabunge wakihamasisha na kugawa mitungi ya gesi ya kupikia kwa wananchi katika maeneo yao. Hongereni sana.

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika ziara nilizofanya maeneo mbalimbali nchini, nimeshuhudia baadhi ya taasisi zikitumia nishati safi ya kupikia kama ilivyoelekezwa na Serikali. Hata hivyo, taasisi nyingine hazijatekeleza maelekezo hayo, hivyo nitumie fursa hii kusisitiza taasisi zote zenye kuandaa chakula cha watu zaidi ya 100 kuhamia kwenye matumizi ya nishati safi ya kupikia.

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, nitumie Bunge lako tukufu kuwakumbusha wadau wote ikiwemo Wizara za kisekta, Taasisi za Umma, Tawala za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Sekta Binafsi na Watanzania wote kuendelea kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Mkakati wa matumizi ya nishati safi ya kupikia. Vilevile, Taasisi za Serikali zihakikishe matumizi ya mapato yanayotokana na uvunaji wa miti, usafirishaji na biashara ya misitu yanaelekezwa katika kufanikisha mkakati huo na uhifadhi wa mazingira.

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande mwingine, nitoe wito kwa wananchi kuendelea kuunga mkono jitihada za Serikali kwa kuhamia kwenye matumizi ya nishati safi ya kupikia. Hakika tukiungana pamoja tunaweza kufikia malengo ya kutumia nishati safi ya kupikia ikiwemo kuimarisha utunzaji wa mazingira pamoja na kuboresha afya na ustawi wa jamii.

**MAANDALIZI YA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2025**

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi imekamilisha Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura awamu ya kwanza katika mikoa yote 31 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nitumie nafasi hii kuwapongeza Watanzania waliojitokeza kwa wingi kwenye zoezi hilo kwa ajili ya kujiandikisha na kuboresha taarifa zao.

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea na maandalizi hayo Tume inatarajia kufanya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura awamu ya pili Mei, 2025. Hatua hiyo itaenda sambamba na zoezi la uwekaji wazi wa Daftari kwa ajili ya kuwawezesha wapiga kura ambao wameandikishwa kukagua taarifa zao.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** hivyo, nitoe rai kwa Watanzania waliopitwa na zoezi la awamu ya kwanza, kutumia fursa hiyo kwenda kujiandikisha na kuboresha taarifa zao ili waweze kutimiza haki yao ya kupiga kura. Aidha, nawasisitiza wapiga kura ambao wameandikishwa tayari kwenda vituoni kuhakiki taarifa zao wakati wa zoezi la uwekaji wazi Daftari.

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imekamilisha maandalizi ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za mwaka 2025, Kanuni za maadili ya Uchaguzi za mwaka 2025 na maelekezo mbalimbali ya uchaguzi. Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa kuna hali ya usalama, amani na utulivu katika kipindi chote cha uchaguzi.

**MAJIBU YA HOJA**

**40.** ***Mheshimiwa Spika***, ninatambua kuwa Waheshimiwa Wabunge wametoa hoja nyingi na zote ni za muhimu kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Hoja nyingi zimetolewa ufafanuzi na Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wakati wakichangia Hoja ya Waziri Mkuu. Kutokana na ufinyu wa muda, baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge zitajibiwa kwa maandishi na nyingine zitatolewa ufafanuzi na Waheshimiwa Mawaziri wakati wakiwasilisha bajeti za Wizara zao.

**41.** ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kutoa maelezo kuhusu hoja kama ifuatavyo:

***Mosi:Utoaji kwa wakati Fedha za Maendeleo na Matumizi Mengineyo ili kuwezesha Wizara, Taasisi na Idara za Serikali kutekeleza majukumu yake kwa wakati na kwa ufanisi.***

**42.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kutoa fedha ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo na matumizi mengineyo. Sote tumeshuhudia utekelezaji wa miradi mbalimbali kutokana na fedha zinazotolewa kwenye maeneo yetu ya uwakilishi. Hivyo, nilihakikishie Bunge lako tukufu kuwa kulingana na mpango kazi, Serikali itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya

utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na matumizi ya kawaida katika robo ya nne ya mwaka 2024/2025.

**Pili: Miundombinu iliyoharibiwa na mvua**

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu kuwa, nchi yetu iliathirika na mvua kubwa za EL-NINO na Kimbunga Hidaya. Athari zilizojitokeza ni pamoja na vifo, majeruhi, upotevu na uharibifu wa mali na miundombinu hususan barabara, madaraja na makalavati.

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ilichukua hatua mbalimbali ili kurejesha hali ya miundombinu iliyoharibika. Hatua hizo ni pamoja na kutafuta fedha za dharura; kuweka mfumo wa manunuzi wa kutafuta wakandarasi; na kuanza ujenzi wa miundombinu iliyoharibiwa katika mikoa yote nchini.

**45.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali ilitoa **shilingi bilioni 72.15** kwa ajili ya kurejesha miundombinu kwa dharura. Vilevile, imetoa **shilingi bilioni 868.56** kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kudumu kwenye wilaya 139 za Tanzania Bara ambazo miundombinu yake iliharibiwa. Miundombinu hiyo inajumuisha madaraja 63, barabara zenye urefu wa kilomita 827, mitaro yenye urefu wa kilomita 84 pamoja na makalavati 225.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** hivi karibuni tumeshuhudia mvua kubwa kwenye mikoa mbalimbali hapa nchini. Mvua hizo zimesababisha athari kwenye miundombinu ikiwemo barabara ya Dar es Salaam hadi Lindi. Miundombinu hiyo ni pamoja na daraja la dharura lililopo kwenye barabara ya mchepuko katika eneo la Somanga ambapo daraja jipya linajengwa.

**47.** ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda niwafahamishe Watanzania na Waheshimiwa Wabunge kuwa, ujenzi wa daraja jipya la Somanga ambalo litakuwa na urefu wa mita 60 pamoja na barabara unganishi ya kilomita 1.7 unaendelea vizuri na haujaathirika. Hadi sasa, Mkandarasi amekamilisha ujenzi wa nguzo 27 kati ya 43 za daraja hilo. Kwa ujumla mradi umefikia

asilimia 38 ya utekelezaji na unatarajiwa kukamilika ifikapo Septemba, 2025 kwa mujibu wa mkataba.

**48.** ***Mheshimwa Spika***, nitumie fursa hii kupitia Bunge lako tukufu, kuwahikikishia wananchi kuwa Serikali itaendelea kukamilisha miundombinu iliyoaharibiwa ili irejee katika hali yake ya kawaida. Vilevile, nitoe rai kwa wananchi wote kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya mvua zinazoendelea kunyesha ili kuepuka athari zinazoweza kujitokeza.

**KUMBUKIZI MUHIMU**

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 26 Aprili, 2025 tutaadhimisha miaka 61 ya Muungano wa nchi yetu ambao umeendelea kuwa chachu ya mafanikio tunayoyashuhudia leo. Nchi yetu iliungana baada ya viongozi wetu shupavu yaani Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Shekhe Abeid Aman Karume kuona haja ya kuliunganisha taifa letu ili kuweza kuipata Tanzania yenye nguvu tunayoiona leo.

**50.** ***Mheshimiwa Spika***, maadhimisho ya mwaka huu yatakuwa na kaulimbiu isemayo*:* ***Miaka 61 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: "Muungano Wetu ni Dhamana, Heshima na Tunu ya Taifa; Shiriki Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025"***. Hivyo, niungane na Watanzania wenzangu kuliombea heri na fanaka taifa letu, huku nikiendelea kuwasihi kudumisha umoja, mshikamano na amani ya nchi yetu. Aidha, ninawaomba Watanzania wote kutumia sherehe hizi katika kukumbushana na kuelimishana juu ya umuhimu n6a uwepo wa muungano, kulinda amani, umoja na undugu wetu pamoja na kufanya kazi kwa bidii.

**MICHEZO**

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu imeendelea kupiga hatua katika medani za michezo kwa kuweza kufuzu katika mashindano mbalimbali ambayo yameijengea heshima nchi yetu. Kupitia uwekezaji uliofanywa na mwanamichezo namba moja nchini, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, umeziwezesha Timu zetu za Taifa kufuzu katika mashindano mbalimbali.

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** niipongeze Wizara yenye dhamana na michezo, Baraza la Michezo Tanzania na Vyama vyote vya michezo nchini, kwa kusimamia maono ya Mheshimiwa Rais. Maono hayo yamewezesha Timu za Taifa kufuzu na kushiriki kwenye mashindano mbalimbali yakiwemo:

(i) Taifa Stars kufuzu AFCON 2025;
(ii) Taifa Stars kufuzu CHAN 2025;
(iii) Twiga Stars kufuzu Mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (WAFCON);
(iv) Ngorongoro Heroes (U20) kufuzu AFCON 2025;
(v) Serengeti Boys (U17) kufuzu AFCON 2024;
(vi) Timu ya Taifa ya Mpira wa Ufukweni kufuzu BSAFCON 2024;
(vii) Kushiriki Mashindano ya Futsal ya wanawake yanayofanyika nchini Morocco; na
(viii) Kufuzu kwa Timu ya Taifa ya Kriketi U19 katika mashindano ya Kombe la Dunia.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** haya ni mafanikio makubwa sana kwa nchi yetu. Sote tunapaswa kujivunia hatua hii na kuendelea kumuunga Mkono Rais wetu ambaye ameonesha nia thabiti ya kuhakikisha taifa letu linapata heshima ya michezo.

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** siku nilipokuwa nasoma hotuba ya bajeti ni siku timu ya Simba ilikuwa inacheza mchezo wa robo fainali na niliitakia kheri kwenye michezo wao. Nitumie nafasi hii sasa, niwapongeze Wawakilishi pekee wa nchi yetu na ukanda wa Afrika Mashariki na Kati waliosalia kwenye michuano mikubwa ya kimataifa Barani Afrika (CAF Confederation Cup), timu ya Simba Sports Club kwa kufuzu hatua ya nusu fainali kwa kuiondosha timu ngumu ya Al Masry kutoka Misri kwa kuweza kushinda kwa njia ya mikwaju mahiri ya penati.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nimpongeze mlinda mlango wa Simba, Mousa Pinpin Camara kwa kuokoa mikwaju miwili mizito ya penati na kuiwezesha Simba kushinda. Ninaipongeza sana timu

ya Simba kwa ushindi huo na tunawatakia heri katika mechi inayofuata ya nusu fainali na nina imani mtafika hatua ya fainali na hatimaye kutwaa ubingwa kwa mara ya kwanza kwa kaulimbiu isemayo "HII TUTAVUKA".

**HITIMISHO**

**Shukrani kwa Bunge**

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapoelekea kuhitimisha, niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuturuzuku rehema hii iliyotupa nafasi ya kujenga utulivu, kusikilizana na kuweza kujadiliana kwa misingi inayozingatia umoja, mshikamano na kuheshimiana. Bunge hili limejijengea historia kubwa ya kuweza kujadili masuala mbalimbali ya kitaifa na kuwa mshauri mkubwa wa Serikali katika kuhakikisha taifa letu linasonga mbele.

**57.** ***Mheshimiwa Spika***, kipekee, nirudie tena kukushukuru na kukupongeza wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kusimamia vema majadiliano ya hoja hii. Hakika usimamizi na miongozo yenu imewezesha kuhitimisha mjadala huu.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru kwa dhati ya moyo wangu Waheshimiwa Wabunge kwa namna ambavyo mmeweza kuijadili hoja hii na kujitoa kwenu katika kuishauri Serikali. Maoni na ushauri mlioutoa umepokelewa kwa uzito mkubwa na Serikali itafanyia kazi.

**59.** ***Mheshimiwa Spika***, baada ya maelezo hayo, sasa, naomba Bunge lako tukufu liridhie na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi zilizo chini yake na Mfuko wa Bunge kama nilivyowasilisha katika hoja yangu ya tarehe 09 Aprili, 2025.

**60.** ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na naona imeungwa mkono na Wabunge walio wengi kabisa. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaendelea na utaratibu wetu.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD - KATIBU WA BUNGE:** Kamati ya Matumizi.

**SPIKA:** Kamati ya Matumizi.

## KAMATI YA MATUMIZI

## KITABU CHA PILI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 15 - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……………………………Sh. 2,064,862,684
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……………Sh. 330,886,300
Kifungu 1003 – *Planning, M & E Unit*………………………Sh. 332,109,880
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*…………………………Sh. 248,560,000
Kifungu 1005 – *ICT Unit*…………………………………………Sh. 278,391,400
Kifungu 1006 – *Procurement Management* Unit………Sh. 174,358,000
Kifungu 2001 – *Mediation*……………………………………Sh. 1,969,492,286
Kifungu 2002 – *Arbitration*…………………………………Sh. 1,691,848,535
Kifungu 2003 – *Dodoma Regional Office*…………………Sh. 13,561,815
Kifungu 2004 – *Lindi Regional Office*………………………Sh. 3,240,000
Kifungu 2005 – *Morogoro Regional Office*…………………Sh. 3,000,000
Kifungu 2006 – *Ruvuma Regional Office*……………………Sh. 3,240,000
Kifungu 2007 – *Kigoma Regional Office*……………………Sh. 3,000,000
Kifungu 2008 – *Iringa Regional Office*………………………Sh. 5,040,000
Kifungu 2009 – *Njombe Regional Office*……………………Sh. 3,600,000
Kifungu 2010 – *Geita Regional Office*………………………Sh. 3,000,000

Kifungu 2011 – *Mara Regional Office*..............................Sh. 3,600,000
Kifungu 2012 – *Singida Regional Office*...........................Sh. 3,000,000
Kifungu 2013 – *Kagera Regional Office*...........................Sh. 3,960,000
Kifungu 2014 – *Shinyanga Regional Office*.....................Sh. 4,800,000
Kifungu 2015 – *Katavi Regional Office*.............................Sh. 3,240,000
Kifungu 2016 – *Tabora Regional Office*...........................Sh. 3,240,000
Kifungu 2017 – *Mbeya Regional Office*.........................Sh. 14,161,815
Kifungu 2018 – *Arusha Regional Office*..........................Sh. 22,271,815
Kifungu 2019 – *Mtwara Regional Office*..........................Sh. 3,000,000
Kifungu 2020 – *Pwani Regional Office*.............................Sh. 6,480,000
Kifungu 2021 – *Tanga Regional Office*.............................Sh. 4,440,000
Kifungu 2022 – *Mwanza Regional Office*.......................Sh. 20,871,815
Kifungu 2023 – *Songwe Regional Office*..........................Sh. 3,120,000
Kifungu 2024 – *Manyara Regional Office*........................Sh. 3,240,000
Kifungu2025-*Dar es Salaam Regional Office*.............Sh. 231,184,655
Kifungu 2026 – *Rukwa Regional Office*........................... Sh. 3,000,000
Kifungu 2028 – *Kilimanjaro Regional Office*.....................Sh. 3,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 25 - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*..................................Sh. 29,746,914,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*.....................................Sh. 1,135,767,596
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts* Unit.................Sh. 502,073,552
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*.............................Sh. 436,033,758
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*................................Sh. 444,861,435
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*.......................................................Sh. 331,742,435

Kifungu 1006 – *ICT Unit*…………………….............………. Sh. 425,402,365
Kifungu 1007 – *Communication and Civic Education Unit*.....................................Sh. 323,300,118
Kifungu 1008 – *Registration of Political Parties Unit*……….................…….Sh. 915,785,695
Kifungu 1009 – *Election expenses and Civic Education*………….....................Sh. 24,439,536,698
Kifungu 1010 – *Monitoring of Political Parties Unit*……….....................…Sh. 1,586,662,000
Kifungu 1011 – *Zanzibar Office*.....................................Sh. 479,784,621
Kifungu 1012 – *Legal Services Unit*................................Sh. 316,518,727

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*..................................Sh. 12,458,982,000
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*..............Sh. 2,605,230,000
Kifungu 1003 - *Policy &Planning Unit*.........................Sh. 6,925,179,000
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*.................................Sh. 480,744,000
Kifungu1005 - *Government Comm. Unit*.......................Sh. 465,955,000
Kifungu 1006 - *Procurement Mgt. Unit*…....................…Sh. 692,888,000
Kifungu 1007- *Legal Services Unit*................................Sh. 457,135,000
Kifungu 1008 - *Management Information System Unit*……...................................…Sh. 455,936,000
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*.......................................................Sh. 444,640,000
Kifungu 2001- *Civil Affairs and Contingencies*……...........…………..Sh. 3,282,957,000
Kifungu 2002 - *National Festivals*...............................Sh. 1,532,591,000
Kifungu 3001- *Parliamentary and Political Affairs*……………………..........Sh. 1,459,964,000
Kifungu 4001-*Private Sector Development and Economic Empowerment*…..............…Sh. 8,240,939,000
Kifungu 5001- *Coordination of Government Business*…….................…Sh. 1,791,607,000

Kifungu 5002 - *Performance, Monitoring and Evaluation Division*…...............Sh. 1,669,236,000
Kifungu 7001- *Government Printer*……….........……………… Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 42 – Mfuko wa Ofisi ya Bunge**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*……........…Sh. 18,309,510,696
Kifungu 1002 – *Library and Research Division*……..Sh. 1,233,129,000
Kifungu 1003 – *Information and Communication Technology Unit*……………………...…Sh. 4,629,446,000
Kifungu 2001 – *Budget Division*………………………Sh. 4,132,701,000
Kifungu 2002 – *Table Office Division*……………….Sh. 99,243,936,000
Kifungu 2003 – *Parliamentary Committees Division*……………………………….Sh. 14,340,333,000
Kifungu 2004 – *Hansard Unit*…………………….…… Sh. 2,589,668,000
Kifungu 2005 – *Legal Services Division*….………… Sh. 2,856,930,000
Kifungu 3001 – *Private Office of The Speaker*……..Sh. 3,402,921,000
Kifungu 3002 – *Private Office of The Deputy Speaker*…………………...………..Sh. 1,383,268,000
Kifungu 3003 – *Office of The Leader of Opposition*……………….....……....Sh. 822,596,000
Kifungu 3004 – *Private Office of The Clerk*……….. Sh. 1,796,938,000
Kifungu 3005 – *Finance and Accounts Unit*……… Sh. 1,559,132,412
Kifungu 3006 – *Communication and International Relations Unit*……………....……….Sh. 6,643,589,892
Kifungu 3007 – *Information, Education and Communication*…………....……….Sh. 2,015,541,000
Kifungu 3008 – *Internal Audit Unit*……….…………… Sh. 989,903,000
Kifungu 3009 – *Procurement Mgt. Unit*……….……..Sh. 1,444,769,000
Kifungu 3010 – *Defense and Security Unit*…...……..Sh. 1,438,866,000
Kifungu 3011 – *Estate Management*…………..……Sh. 5,711,363,000
Kifungu 3012 – *Zanzibar Office*………………………Sh. 415,762,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 61 – Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi**

Kifungu 1001 – *Administartion and Human Resources Management*…………………….…Sh. 4,332,377,000
Kifungu 1002 – *Planning Monitoring & Evaluation* ……………………..……...Sh. 697,561,000
Kifungu 1003 – *Finance and Planning Unit* .……..…. Sh. 763,084,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit* ………………..….Sh. 456,269,000
Kifungu 1005 – *Legal Services* ……………………..….Sh. 602,032,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management & Logistics Unit* ………………………….Sh. 760,494,000
Kifungu 1007 – *Zanzibar Office* ………………………. Sh. 368,446,000
Kifungu 2001 – *Election Management Division*.…….Sh. 780,710,000
Kifungu 2002 – *National Voters Registration & Information Communication Technology Division*...............................................Sh. 1,008,178,000
Kifungu 2003 – *Voters Education & Public Information Division*……….………….Sh. 895,170,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 65 – Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu**

Kifungu 1001 – *Administration & Human Resources Management*….............................Sh. 4,901,191,233
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…….……Sh. 543,103,415
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*……………Sh. 1,168,562,275
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*………..……………Sh. 491,523,198
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*……Sh. 347,615,656
Kifungu 1006 – *Government Communication Unit*…Sh. 211,843,994
Kifungu 1007 – *Information and Comm. Tech. Unit*...Sh. 269,368,798
Kifungu 1008 – *Legal Services Unit* …………………… Sh. 307,187,708
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*….…Sh. 518,863,901
Kifungu 2001 – *Labour Division*.…………………… Sh. 10,871,583,064
Kifungu 2002 – *Employment Division* ….……………Sh. 1,016,853,630
Kifungu 2003 – *Registrar of Trade Unions* …….………Sh. 434,667,322
Kifungu 2004 – *Arusha Regional Labour Office*……..Sh. 105,500,708

Kifungu 2005 – *Dodoma Regional Labour Office*...… Sh. 93,872,904
Kifungu 2006 – *Geita Regional Labour Office*…………Sh. 39,126,649
Kifungu 2007 – *Iringa Regional Labour Office*..……….Sh. 88,782,219
Kifungu 2008 – *Kagera Regional Labour Office*..……..Sh. 69,861,493
Kifungu 2009 – *Kigoma Regional Labour Office*……..Sh. 77,340,731
Kifungu 2010 – *Kilimanjaro Regional Labour Office*… Sh. 81,302,981
Kifungu 2011 – *Lindi Regional Labour Office*..…………Sh. 53,299,796
Kifungu 2012 – *Manyara Regional Labour Office*……Sh. 59,367,782
Kifungu 2013 – *Mara Regional Labour Office*..……….Sh. 62,051,705
Kifungu 2014 – *Mbeya Regional Labour Office*…….Sh. 130,769,395
Kifungu 2015 – *Morogoro Regional Labour Office*…..Sh. 92,*365,152*
Kifungu 2016 – *Mtwara Regional Labour Office*..……Sh. 97,455,840
Kifungu 2017 – *Mwanza Regional Labour Office*...…Sh. 178,760,195
Kifungu 2018 – *Njombe Regional Labour Office*..……Sh. 54,151,072
Kifungu 2019 – *Pwani Regional Labour Office*………Sh. 135,468,209
Kifungu 2020 – *Rukwa Regional Labour Office* ………Sh. 73,258,113
Kifungu 2021 – *Katavi Regional Labour Office*………. Shs 51,951,579
Kifungu 2022 – *Ruvuma Regional Labour Office*..……Sh. 73,823,745
Kifungu 2023 – *Shinyanga Regional Labour Office* …Sh. 92,249,200
Kifungu 2024 – *Simiyu Regional Labour Office*..………Sh. 61,253,822
Kifungu 2025 – *Singida Regional Labour Office*……… Sh. 82,999,877
Kifungu 2026 – *Tabora Regional Labour Office*……. Sh. 102,106,917
Kifungu 2027 – *Tanga Regional Labour Office*..……..Sh. 105,056,686
Kifungu 2028 – *Temeke Regional Labour Office*……Sh. 127,375,603
Kifungu 2029 – *Kinondoni Regional Labour Office*…Sh. 113,169,089
Kifungu 2030 – *Ilala Regional Labour Office*…………Sh. 121,027,634
Kifungu 2031 – *Social Security Division* ……………… Sh. 962,*037,967*
Kifungu 2032 – *Youth Development*………………... Sh. 2,436,649,501
Kifungu 2033 – *Employment Services Unit*………… Sh. 1,136,450,650
Kifungu 2034 – *Persons with Disability Unit* ………... Sh. 1,725,991,684
Kifungu 2035 – *Productivity Promotion Unit* ……… Sh. 484,065,908

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 91- Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**

Kifungu 1001 – *Corporate Services Division*………Sh. 4,519,675,054

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…………Sh. 759,333,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……..………………Sh. 523,615,500
Kifungu 1005 – *Legal Services Unit* …………………..Sh. 1,095,493,120
Kifungu 1006 – *Procurement Mgt. Unit*………………. Sh. 485,000,000
Kifungu 1007 – *Government Comm. Unit*…………....Sh. 523,553,876
Kifungu 2001 – *Intelligence Division* …...................Sh. 2,014,165,800
Kifungu 3001 – *Operations & Investigation Div*……Sh. 3,239,090,000
Kifungu 4001 – *Prevention and Treatment Div*……Sh. 2,037,919,500
Kifungu 5001 – *Inspection and Forensic Sciences Division*…………..Sh.1,289,220,000
Kifungu 6001 – *Zonal Offices* ……………………..… Sh. 6,624,315,150

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 92 – Tume ya Uratibu na Udhibiti wa UKIMWI**

Kifungu 1001 – *Planning, Research and Innovation Division*……..…………..Sh. 1,065,388,000
Kifungu 1002 – *Corporate Services Division*………..Sh. 1,560,114,000
Kifungu 1003 – *Monitoring and Evaluation Unit*…......Sh. 312,200,000
Kifungu 1004 – *Advocacy Division*……………….……Sh. 560,396,000
Kifungu 1005 – *National Response Division*…..…..…..Sh. 709,720,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*….…Sh. 360,748,000
Kifungu 1007 – *Legal Services Unit*…..........…...…… Sh. 546,112,000
Kifungu 1008 – *Information & Communication Technology Unit*……….........…..…... Sh. 360,700,000
Kifungu 1009 – *Internal Audit Unit*……….…………... Sh. 406,033,000
Kifungu 1010 – *Special Programs Unit* …...........….……….…….Sh. 0
Kifungu 1011 – *Government Communication Unit*….Sh. 305,633,000
Kifungu 1012 – *Epidemic Surveillance Units*…..………Sh. 370,120,000
Kifungu 1013 – *Central Zone*…....................................Sh. 255,552,000
Kifungu 1014 – *Eastern Zone*………………..……..…...Sh. 262,872,000
Kifungu 1015 – *Southern Highland Zone*…….…...……Sh. 255,552,000
Kifungu 1016 – *Northern Zone*……………..……..…...Sh. 207,552,000
Kifungu 1017 – *Lake Zone*…………………..………….Sh. 254,808,000

Kifungu 1018 – *Southern Zone*…………..………………..Sh. 237,180,000
Kifungu 1019 – *Western Zone*……..…………………...Sh. 250,152,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahamia kwenye Kitabu cha Nne cha Matumizi ya Maendeleo.

## KITABU CHA NNE

## MIPANGO YA MAENDELEO

### Fungu 15 – Tume ya Usuluhishi na Uamuzi

Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring & Evaluation Unit*…………………………………...Sh. 56,046,000
Kifungu 1005 – *Information, Communication & Technology Unit*………………………….Sh. 61,000,000
Kifungu 2001 – *Mediation*…………………………….....Sh. 81,000,000
Kifungu 2002 – *Arbitration*……………………..……..Sh. 78,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### Fungu 27 – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa

Kifungu 1011 – *Zanzibar Office* ……………………….. Sh. 564,000,000

*(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu

Kifungu 2001 – *Civil Affairs and Contingencies*……Sh. 200,600,000
Kifungu 4001 – *Private Sector Development & Economic Empowerment*…..........................……Sh. 0

Kifungu 5001 – *Coordination of Government Business*……………….....……………Sh. 6,566,179,000
Kifungu 7001 – *Government Printer*……………………Sh. 741,381,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 42 – Mfuko wa Ofisi ya Bunge**

Kifungu 1001 – *Administration & Human Resources Management Division*……..................................Sh. 0
Kifungu 1003 – *Information and Communication Technology Unit*…………….....………Sh. 6,000,000,000
Kifungu 2001 – *Budget Division* ………………………….Sh. 569,450,000
Kifungu 3004 – *Private Office of The Clerk*…….……Sh. 2,000,000,000
Kifungu 3011 – *Estate Management*………..………Sh. 3,223,882,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi**

Kifungu 1001 – *Administration & Human Resources Management*……..........................Sh. 35,522,461,000
Kifungu 1002 – *Planning, Monitoring and Evaluation Division*…………………...Sh. 3,154,918,000
Kifungu 1003 – *Finance and Accounts Unit*………..… Sh. 466,790,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……..……………..…Sh. 598,609,000
Kifungu 1005 – *Legal Services Unit*…………………. Sh. 3,213,331,000
Kifungu 1006 – *Procurement Mgt. and Logistics Unit*…………………….……………. Sh. 9,898,083,000
Kifungu 1007 – *Zanzibar Office*…....………………… Sh. 351,351,000
Kifungu 2001 – *Election Mgt Division*……………..Sh. 305,502,064,000

Kifungu 2002 – *National Voters Registration & Information Communication Technology Division*.............................................Sh. 2,620,411,000
Kifungu 2003 – *Voters Education and Public Information Division*……………………Sh. 6,289,800,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 65 – Ofisi ya Waziri Mkuu, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*..…..................Sh. 720,000,000
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*………………………..…................Sh. 200,000,000
Kifungu 2001 – *Labour*……………..................……………..…......Sh. 0
Kifungu 2002 – *Employment Division*……..................Sh. 7,522,975,401
Kifungu 2003 – *Registrar of Trade Unions*......................................Sh. 0
Kifungu 2031 – *Social Security Division*……...................................Sh. 0
Kifungu 2032 – *Youth Development*……...................Sh. 1,509,732,000
Kifungu 2033 – *Employment Services Unit*…............Sh. 2,369,398,599
Kifungu 2034 – *Persons with Disability Unit*…............Sh. 1,000,000,000
Kifungu 2035 – *Productivity Promotion Unit*...................................Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 91 – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**

Kifungu 4001 – *Prevention & Treatment Division*......Sh.1,314,506,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania**

Kifungu 1001 – *Planning, Research and Innovation Division*...........................Sh. 6,287,186,260

Kifungu 1002 – *Corporate Services Division*……..........Sh. 541,630,000
Kifungu 1003 – *Monitoring and Evaluation Unit*…......Sh. 839,859,300
Kifungu 1004 – *Advocacy Division*…………..................Sh. 963,322,150
Kifungu 1005 – *National Response Division*.............Sh. 10,987,509,251
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*…......Sh. 16,230,000
Kifungu 1007 – *Legal Services Unit*…………..................Sh. 770,763,039
Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*……..................……Sh. 144,030,000
Kifungu 1009 – *Internal Audit Unit*……….......................Sh. 22,540,000
Kifungu 1010 – *Special Programs Unit*……....................................Sh. 0
Kifungu 1011 – *Government Communication Unit*.......................................................Sh. 119,650,000
Kifungu 1012 – *Epidemic Surveillance Unit*..................Sh. 122,110,000
Kifungu 1015 – *Southern Highland Zone*…....................Sh. 53,148,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kuwa, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Mtoa hoja, Taarifa. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mtoa Hoja, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, na kwa mujibu wa Kanuni ya 123, Kanuni Ndogo ya 3(a) na (b) ya Kanuni Ndogo za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kutoa Taarifa

kwamba, Bunge lako likikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake. Naomba sasa Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Kwa mujibu wa kanuni zetu nitawahoji.

Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026, waseme Ndiyo. Wasioafiki waseme Siyo.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Wote mmeafiki. Baada ya kuwahoji, sasa Bunge limepitisha rasmi Makadirio na Mapato ya Matumizi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Kwa kupitisha huku nitumie fursa hii kumtakia kila la heri Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pia, Waheshimiwa Mawaziri wawili ambao wanamsaidia kazi, Manaibu Mawaziri na Makatibu Wakuu wote. Pia, Watendaji wa chini ya Wizara hii. Tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa hii bajeti. *(Makofi)*

Pamoja na kwamba, wakati tunaanza utekelezaji huo utakuwa ni sehemu ya yale ambayo mmeyasema sana wakati mkisema kwenye hotuba zenu, kumtakia kila la heri kila mmoja wetu uchaguzi mwema. Pia, tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa bajeti hii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia, nitumie nafasi hii kuwashukuru sana ninyi nyote, kila mmoja wenu ameshiriki kwa namna ambayo amepewa hayo majukumu. Wengine wameshiriki ngazi ya Kamati, ambapo Kamati zinazoshughulika na Ofisi ya Waziri Mkuu zimefanya kazi nzuri, Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe wote. *(Makofi)*

Pia sisi Wabunge kwa ujumla wetu tumeshiriki mjadala huu kikamilifu kabisa. Kwa hiyo, kama mlivyowasikia wakati wakihitimisha hoja, wameonesha kwamba, yale yote ambayo mmeyasema, ambayo hayakuwemo kwenye hotuba na pia, pengine hayajapata nafasi ya kufafanuliwa wakati wa kuhitimisha hoja zenu Waheshimiwa Wabunge, lakini yote wameyachukua.

Kwa hiyo, yale ambayo yalikuwa ni hoja zinazohitaji ufafanuzi, watatoa ufafanuzi kwa maandishi, lakini yale ambayo wanahitaji kuyafanyia kazi, basi wameshawaambia hapa kwamba, wameyachukua na wanaenda kuyafanyia kazi. Msiwe na wasiwasi kwamba, kipindi hiki labda wanawaza uchaguzi, hapana. Ndiyo maana hapa tumewataja Makatibu Wakuu wao, wapo. Kwa hiyo, wataendelea kufuatilia hoja zenu Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Sasa, baada ya kusema hayo, na kuwatakia kila la heri katika utekelezaji wa bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu, pamoja na kiongozi wetu mwenyewe, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninayo matangazo mawili hapa mbele. Kwanza, ni tangazo la wageni.

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, ambao ni Walimu kutoka Wilaya ya Mbulu, Mkoa wa Manyara. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo kutoka kwa Katibu wa Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi Bungeni. Mnakumbushwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama Cha Mapinduzi kwamba, leo mara baada ya kuahirisha Shughuli za Bunge mnatakiwa kuelekea *White House*, kwa ajili ya Kikao. Kwa hiyo, mnakumbushwa kwamba, mkitoka hapa mwelekee *White House* kwa ajili ya kikao. (Makofi)

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 12.48 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 16 Aprili, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*